# Nipashe

Jumanne Desemba 10, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580097

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

CEFA

215544702




Juisi ya tende yahusishwa unyanyasaji, ukatili kijinsia

UK. 23

## MIAKA 58 YA UHURU:

# Wapinzani, wanasiasa waibua mambo mazito

**Wataka** uhuru wa demokrasia, kufufuliwa Katiba mpya, maridhiano na umoja wa kitaifa

... *Uk. 2& 3*




*MBOWE*

**"Nimekuja kushiriki sherehe kama uthibitisho wa ulazima wa kuwapo maridhiano katika taifa letu"**




*SUMAYE*

**"Bado tuna kazi kubwa ya kupata uhuru wa kiuchumi"**



*LOWASSA*

**"Kama Magufuli akiachiwa akapiga miaka yake 10, nchi hii itakuwa na maendeleo makubwa"**



*PROF. LIPUMBA*

**"Rais ana jukumu la kujenga demokrasia katika nchi yetu, hasa tunapoelekea uchaguzi mkuu".**



Rais John Magufuli akiwasili katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza kuongoza sherehe za maadhimisho ya miaka 58 ya Uhuru jana. **PICHA: IKULU**

## DAWA YA MADALALI VISHOKA YAIVA

UK.4

# JPM asamehe wafungwa 5,000

UK. 2

MICHEZO **YANGA YAISHTUKIA SIMBA KWA LAMINE** UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Wapinzani, wanasiasa waibua mazito

**Na Waandishi Wetu,**
MWANZA

MAADHIMISHO ya miaka 58 ya Uhuru jana katika Uwanja wa Kirumba jijini hapa yalitekwa na tukio adimu la kuwakusanya wanasiasa na viongozi wa kitaifa, ambao si kawaida kupatikana katika sehemu moja kwa wakati mmoja.

Viongozi watatu wa kisiasa, Freeman Mbowe, Edward Lowassa na Frederick Sumaye, ambao walikuwa pamoja ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) lakini sasa wametawanyika katika kinachoonekana sintofahamu ya kimyakimya, walikutanishwa katika tukio hilo.

Aidha, maudhui na wazo kuu la hotuba zao jana walipopewa fursa, yalifanana kwa baadhi ya wanasiasa na viongozi wenye nyendo sawa, wakiweka msimamo unaoangukia katika ujumbe wa jozi moja.

Sura moja ya wanasiasa ni waliokuwa mawaziri wakuu, Sumaye na Lowassa, ambao walijiengua kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) na sasa hawako huko walikohamia, kwa mara ya kwanza walionekana hadharani kuungana katika tukio hilo la kitaifa.

Maalim Seif Sharif Hamad, aliyewahi kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pia mwasisi na Katibu Mkuu wa muda mrefu wa Chama cha Wananchi (CUF), alikuwapo.

Kwa kipindi cha karibuni tangu kujiengua toka CUF kutokana na misuguano ya kisiasa, Maalim Seif amekuwa adimu katika hadhira kama hiyo, jambo lililoongeza mvuto wa aina yake jana.

Vilevile, viongozi wakuu wa vyama vya upinzani ambao katika sura tofauti wana misukosuko ya kisiasa ndani ya vyama vyao, pia dhidi ya wapinzani wao wakuu CCM, Prof. Ibrahim Lipumba na Freeman Mbowe, walihudhuria.

Hiyo ilienda sambamba na hadhira ya viongozi wakuu wa nchi wastaafu, Marais Ali Hassan Mwinyi na Benjamin Mkapa, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais, John Malecela na Waziri Mkuu Mizengo Pinda.

Katika kile kilichoonekana kupamba shughuli ya jana, mara baada ya kupewa fursa, Lowassa, aliyewahi kuwa Waziri Mkuu katika awamu iliyopita, aliweka msimamo wake wazi kwa kumsifu Rais John Magufuli kuwa utendaji wake unampa haki ya kukaa madarakani kwa awamu zote mbili.

"Mheshimiwa Rais, kwa kweli sina la kusema, nimependezwa sana na hadhara hii, nimependezwa sana na hotuba yako. Mwalimu Nyerere ilipotimia miaka 10 ya Azimio la Arusha, aliwaambia Watanzania 'akija mtu jeuri akakuuliza ninyi Watanzania mna nini? mjibu kiungwana mna na amani'.

"Amani hiyo ndiyo msingi anaoutumia Mheshimiwa Rais Magufuli leo kuongoza nchi yetu, mshikamano na umoja wa nchi yetu. Nampongeza sana, anafanya kazi nzuri sana.

"Kama akiachiwa akapiga miaka yake kumi. Kumi mheshimiwa... nchi hii itabadilika na itakuwa nchi ya ajabu yenye maendeleo makubwa. Kwa hiyo, naomba tumuunge mkono, tumsaidie nchi yetu iende mbele," alisema.

Ni kauli iliyoendana na kuiga mbwembwe za jukwaani za Rais Magufuli, ambazo ziliufanya umma mara tu baada ya kuhitimisha, kuamsha shangwe na vigelegele kumshangilia.

Vivyo hivyo, Sumaye aliyemwachia ofisi Lowassa, pia ana siku sita tangu ajiengue Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) alikokuwa Lowassa, sasa akitangaza 'hana chama chochote', aliendeleza dhana ileile ya mwenzake kumsifu Rais Magufuli kuinyanyua nchi kiuchumi.

"Mheshimiwa Rais, ninakushukuru kwa kutukaribisha hapa ili tuweze kusema neno moja au mawili kuhusu sikukuu ya leo. Leo (jana) tunasherekea uhuru ambao tuliupata wakati huo.

"Lakini, kama alivyoeleza Rais, bado tuna kazi kubwa ya kupata uhuru wa kiuchumi ili taifa lisiwe tegemezi, bado kuna tatizo la utegemezi.

"Naamini kwamba kwa kazi inayofanywa na serikali ya awamu ya tano na zingine zote za awamu ya nyuma zilizofanya, ninaamini kabisa tutakuwa tunakaribia sana kupata uhuru wa uchumi. Mheshimiwa Rais tunakupongeza

INAENDELEA UK. 8



Mwonekano wa Uwanja wa CCM Kirumba, jijini Mwanza, wakati wa sherehe za miaka 58 ya Uhuru na 57 ya Jamhuri zilizoongozwa na Rais John Magufuli jana. **PICHA: IKULU.**

# JPM asamehe wafungwa 5,533

**Na Elizabeth Faustine,**
MWANZA

MAADHIMISHO ya miaka 58 ya Uhuru na miaka 57 ya Muungano yameacha kicheko kwa wafungwa 5,533 kusamehewa wakiwamo wa uhujumu uchumi.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, alitoa msamaha kwa wafungwa hao waliopo katika magereza mbalimbali ambao wamebakiza muda wa siku moja hadi miezi 12 na waliotumikia kifungo cha muda mrefu na kubakiza muda usiozidi mwaka moja.

Miongoni mwa wafungwa waliopewa msamaha huo ni pamoja na mahabusi 345 na wenye kesi za makosa ya uhujumu uchumi 256.

Msamaha huo wa Rais Magufuli unatokana na mrundikano wa wafungwa katika magereza mengi nchini kufuatia ziara yake aliyoifanya katika baadhi ya magereza likiwamo la Butimba.

"Mnakumbuka miezi michache iliyopita nilitembelea baadhi ya magereza likiwamo Gereza la Butimba, kweli nilishuhudia kuwapo kwa mrundikano wa wafungwa, nikaelezwa hali kama hiyo haipo Butimba peke yake bali ni kwa magereza yote nchini na mpaka sasa tunavyozungumza leo kuna wafungwa 17,547, mahabusi 18,256, hivyo wafungwa na mahabusi tulionao katika magereza yetu ni 35,803," alisema Magufuli.

Ameeleza kuwa kama mwanadamu hali aliyoishuhudia alipotembelea Gereza la Butimba, Julai 16, mwaka huu ilimsikitisha na kwa kuwa Mwenyezi Mungu anasamehe na kwa kuwa dini zote zinafundisha kusamehe, kwa mamlaka aliyonayo amewasamehe wafungwa hao.

"Kwa mujibu wa madaraka niliyopewa katika ibara ya 45 ibara ndogo ya kwanza kifungu cha 'a' mpaka 'e' cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara hii imeandika mamlaka ya kusamehe au kufuta adhabu ya mtu aliyetiwa hatiani na mahakama, ibara hiyo ikisomwa pamoja na kifungu cha 49 cha Sheria ya Magereza, sura ya 58 ,ndugu zangu nimeguswa na nimeamua leo tarehe 9 Desemba, 2019 katika kusherehekea miaka 58 ya Uhuru wetu nasamehe idadi kubwa sana ya wafungwa jumla ya wafungwa 5,533," alisema Rais Magufuli.

"Najua ni idadi kubwa na watu wanashangaa, lakini nimeguswa na moyo wangu ninasamehe

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# Butiku awapa wasomi mtihani wa katiba mpya

**Na Gwamaka Alipipi**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere (MNF), Joseph Butiku, amesema kuna haja kwa wanataaluma nchini kuanza kuzungumzia mchakato wa katiba mpya kuliko kukaa kimya, kwani ulitumia fedha nyingi.

Aliyasema hayo jana, wakati wa kumbukizi ya Siku ya Uhuru wa Tanzania Bara katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, uliondaliwa na Jumuiya ya Wanataaluma wa chuo hicho (Udasa).

"Lazima wanataaluma waendelee kuzungumza kuhusu mchakato wa katiba mpya, zoezi lilikuwa kubwa na lilitumia fedha nyingi, lakini wanataaluma tumekaa kimya, tena nasikitika kusema kuwa mojawapo wa watu waliokuwapo katika mchakato huo ni mimi na mzee Warioba, leo tukipita mitaani tunatemewa mate na kuonwa hatuna jipya," alisema Butiku.

Butiku ambaye alikuwa akizungumzia mada isemayo 'mchango wa wanataaluma katika ujenzi wa taifa', pia alisema wanataaluma wanapaswa kuwa watu wa kutafuta ukweli, kuwa wajasiri na kutambua nchi ilipotoka na inapokwenda.

"Kutafuta ukweli ni wajibu wa kwanza wa wanataaluma, pia wanapaswa kuwa wajasiri wa mioyo na ubongo, hatutaki mtu anakuja kusoma hapa UDSM anakuwa muoga, anapaswa kuwa jasiri," alisema Butiku, ambaye alikuwa mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

Kuhusu ajira, Butiku alishangazwa na idadi kubwa ya wahitimu wa vyuo vikuu nchini, lakini upatikanaji wa ajira unakuwa mdogo.

Alisema kila mwaka kunakuwa na idadi kubwa ya wahitimu katika vyuo vikuu, lakini wengi wao wanaishia mitaani, huku wengine wanakuwa wababaishaji.

"Kwa nini wanataaluma mnaandaa wanataaluma wasioweza kujiajiri?" Alihoji na kuendelea:

Tunatoa wahitimu kila mwaka, wanavaa majoho na kofia wanazipeperusha, lakini mmewahi kujiuliza wanakwenda wapi? "Wengi wanakwenda kuishia mitaani bila ajira."

Butiku aliwataka wanataaluma nchini kuzungumza na kukemea masuala yanayotokea katika uchaguzi nchini, na kueleza kuwa kukaa kimya kutasababisha kasoro hizo kuendelea kutokea kila mwaka.

Naye mwanazuoni kutoka UDSM, Prof. Issa Shivji, akiwasilisha mada ya 'Nafasi ya wanataaluma katika maendeleo ya taifa: Enzi zilizopita na zilizopo', alisema enzi za zamani kulikuwa na uhuru wa kitaaluma, walimu walikuwa wanapata ajira, utawala wa chuo ulikuwa unaheshimu wanataaluma, watawala walikuwa wanawalinda wanataaluma, lakini zama za sasa imekuwa kinyume.

# Sungusungu, makomandoo JWTZ waacha gumzo Mwanza

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

SHEREHE za miaka 58 ya Uhuru na miaka 57 ya Jamhuri, zimeacha historia katika Jiji la Mwanza na vitongoji vyake baada ya kutokea Jeshi kubwa la Ulinzi la Sungusungu lenye idadi ya watu 1,200 kuonyesha ukakamavu wa aina yake.

Tukio hilo lilikuwa la kipekee kwa wakazi hao na wengine waliokuwa katika maadhimisho hayo yaliyofanyika katika uwanja wa CCM Kirumba jijini hapa.

Sambamba na jeshi hilo la jadi, kundi la makomando wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) nalo lilionyesha umahiri kwa kutumia helikopta iliyokuwa imeganda angani.

Wengi walishangaa kutokea kwa kundi hilo kubwa la Sungusungu kutoka katika Wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza, ambalo limeacha historia ya kipekee kwenye maadhimisho hayo ambayo yamekuwa ya aina ya kipekee tofauti na miaka mingine.

Jeshi hilo limeelezwa kuwa lilianza katika wilaya hiyo mwaka 1983, wakati wa serikali ya awamu ya kwanza na aliyekuwa Waziri Mkuu Edward Sokoine (sasa marehemu).

Askari hao wa Sungusungu, wakiwa wamevalia mavazi ya kijadi ya Kisukuma, waliingia uwanjani kutumbuiza huku wakiwa na silaha za jadi, ikiwamo mishale na upinde.

Licha ya silaha hizo, walitoa ujumbe kwa Rais John Magufuli, aliyekuwa mgeni rasmi, pamoja na mambo mengine pongezi kwa kazi za maendeleo anazozifanya kwa wananchi wanyonge.

Kundi hilo lilisisimua na kuburudisha zaidi uwanjani pamoja na kuwapo kwa makundi mengine ya burudani na kama kawaida yake majeshi ya ulinzi na usalama yakisherehesha maadhimisho hayo kwa gwaride.

Aidha, askari wa kikosi cha makomandoo cha JWTZ nao walionyesha umahiri wao kwa kutumia helikopta iliyokuwa imeganda angani huku wao wakishuka kwa kamba.

Walifanya hivyo kwa kutoa mfano wa mapambano ya kuwaokoa wenzao waliotekwa mateka wa kivita kutoka kwa maadui.

Maadhimisho hayo yalipambwa na gwaride lililojumuisha vikosi vya ulinzi na usalama vikiongozwa na JWTZ ambavyo vilipita mbele ya Rais kwa mwendo wa pole na wa haraka na kutoa heshima.

Vikosi hivyo vikiwa na askari wanaume na wanawake na bendi iliyojumuisha majeshi yote ya ulinzi na usalama, vikitanguliwa na kikosi cha bendera, viliundwa na JWTZ kwa upande wa kikosi cha nchi kavu, ulinzi wa anga na majini, Jeshi la Kujenga Taifa, Polisi na Magereza.

**Licha ya silaha hizo, walitoa ujumbe kwa Rais John Magufuli, aliyekuwa mgeni rasmi, pamoja na mambo mengine pongezi kwa kazi za maendeleo anazozifanya kwa wananchi wanyonge.**




HABARI KITAIFA




Meneja Mawasiliano na Elimu kwa Umma wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Gaudensia Simwanza, akiwapatia maelezo wadau waliotembelea kupata huduma katika maonyesho ya nne ya bidhaa za viwanda vya Tanzania, yanayofanyika Viwanja vya Julius Nyerere Sabasaba jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

# Dawa ya madalali matapeli yaandaliwa




**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Kampuni ya Unadishaji Tanzania (TACA), kimesema katika kuhakikisha sekta hiyo inabaki na watu wanaotambulika kisheria na kuondokana na utapeli, kitapita kanda zote kukagua madalali kama wamejisajili.

Mwenyekiti wa chama hicho, Phidel Katundu, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa kila dalali anayefanya shughuli hiyo anatakiwa kujisajili na kutambulika.

"Hii ni kazi kama zilivyo nyingine, tunataka madalali wote wajisajili kwenye chama chao ili tuondokane na madalali kanjanja ambao wamekuwa wakichukua fedha za wateja na kukimbia nazo na mwisho wa siku madalali wote wanachafuka kuwa ni makanjanja," alisema.

Katundu alisema TACA kimepata usajili wake mwezi Julai, mwaka huu na tayari baadhi ya mikoa kuna ofisi zake.

Aliwataka wananchi ili kuepukana na changamoto ya kutapeliwa wawatumie madalali wanaotambulika kisheria.

"Tutapita ofisi zetu zote za kanda kukagua madalali waliopo na uhalali wao wa kufanya kazi hiyo kama upo kisheria," alisema.

Pia alisema upo mwingiliano wa sheria inayowaongoza wao na ofisi za wilaya, hivyo kusababisha isitekelezwe ipasavyo.

"Mwingiliano huu kati yetu na ofisi ya wilaya umekuwa ni changamoto kubwa kwetu na kusababisha baadhi wakati wa utekelezaji wa majukumu kuwekwa ndani licha ya kuwa na nyaraka muhimu za utendaji kazi zilizotolewa na mamlaka au taasisi yoyote kwa ajili ya udalali," alisema.

Alisema lengo la kuwatambua madalali ni ili walipe kodi na kulinda kazi hiyo na kuwasaidia wanapopata changamoto ziweze kutatuliwa kisheria.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Elieza Mbwambo, alisema sheria inayowaongoza ni ya mwaka 1913, iliyotungwa enzi za ukoloni ambayo inasema msimamizi wa shughuli hiyo ya udalali ni Rais.

"Sheria hii ni ya zamani na ilitungwa kwenye mazingira ambayo wakati huo madalali walikuwa hawana ofisi, hivyo dalali ili atekeleze kazi yake anatakiwa aripoti ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

"Kwa sasa hii ni sekta rasmi na inatoa ajira na kulipa kodi inahitaji mambo mengi yaboreshwe, ndiyo maana tunawataka madalali wote watambulike kisheria ili kuondokana na madalali kanjanja," alisema.

# Waozesha watoto wa kike kwa pombe

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa kijiji cha Penzi katika Halmashauri ya Mji wa Kahama, wamesema ongezeko la mimba za utotoni na ukatili wa kijinsia vinachangiwa na wazazi kuwaozesha kwa jagi moja la pombe vilabuni.

Hayo waliyabainisha juzi kwenye maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, yaliyofanyika katika kijiji cha penzi yaliyodhaminiwa na shirika lisilo la kiserikali la World Vision chini ya mradi wa Enrich.

Angelina Selemani, mkazi wa kijiji hicho alisema kinababa wamekuwa wakiwaozesha watoto wao wa kike bila kuwajulisha kwa kubadilishana na jagi moja la pombe au ng'ombe wawapo vilabuni.

Alisema kulingana na mila na desturi za Kisukuma, hawaruhusiwi kuhoji, hivyo inabidi mtu akubali mwanawe aolewa japo anasoma na makubaliano yanakuwa yamefanyika kwenye vilabu wakati wanakunywa pombe na wanapokataa wanaambulia vipigo.

Naye Maria Emmanuel alisema: "Wakati mwingine unakuta mtoto anafanya vizuri kwenye masomo yake lakini baba yake anamtaka kufanya vibaya kwenye mitihani yake kwa kisingizio hana fedha ya kumsomesha na unapofuatilia unakuta ameshakula mahari."

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Shinyanga, Tedson Ngwale, alisema ili kukomesha vitendo hivyo, wameanzisha utaribu wa mtoto wa kike anayefanya vizuri kwenye masomo, mzazi anatakiwa kufunga mkataba na mwalimu mkuu wa shule anayosoma na atakapofanya vibaya, mzazi atawaajibika kisheria.

Ngwale pia alisema hakuna ndoa yoyote itakayofungwa kuanzia ngazi ya kijiji, kata hadi wilaya bila kuwa na cheti cha kuzaliwa ambacho kitaonyesha umri wa anayekwenda kuolewa na akiwa chini ya miaka 18, wazazi wa pande mbili watashtakiwa.

# TPA yajivunia mapato kupaa

**Na Elizabeth Zaya,**

MWANZA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari (TPA), imesema inajivunia kuongezeka kwa mapato yake kutokana na mfumo na mikakati mipya ya kuongeza shehena na ufanisi katika utoaji wa huduma zake.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Deusdedit Kakoko, alisema jijini Mwanza mwishoni mwa wiki kuwa mafanikio hayo yametokana na mfumo mpya wa upimaji utendaji kazi na ukusanyaji wa mapato kwa kila bandari na kwa kila mfanyakazi.

"Mfumo huu umechangia kufanya kazi kwa ufanisi na kukusanya mapato kwa wingi na hata shehena zimezidi kuongezeka kila wakati, tofauti na ilivyokuwa katika kipindi cha nyuma," alisema.

Alisema mwaka 2015/2016, walikuwa na ongezeko la asilimia sita hadi saba, lakini kwa sasa wamepanda hadi kufikia ongezeko la asilimia tisa hadi 11.

Kakoko pia alisema mapato yamekuwa yakipanda mwaka hadi mwaka, akibainisha kuwa katika kipindi cha kuanzia mwaka jana hadi mwaka huu wamefanikiwa kukusanya Sh. bilioni 940.

"Kwa upande wa shehena tumekuwa tukipanda mwaka hadi mwaka, huko nyuma tulikuwa tukipanda kwa asilimia sita hadi saba, sasa hivi tumekwenda hadi asilimia tisa hadi 11.

"Na kwenye fedha tumekuwa tukienda hivyo hivyo, tulikuwa tukipata Sh. bilioni 300 hadi Sh. bilioni 320 kila mwaka, lakini sasa tuna ongezeko kubwa.

"Kwa hiyo baada ya kuingia menejimenti iliyopo sasa hivi na bodi, tulijiwekea malengo tukaanza kwa kuongeza mapato ya Sh. bilioni 608 (wakati wanaingia), lakini tulipoboresha mikakati zaidi, tulipanda zaidi Sh. bilioni 940, na mpaka hivi tunapozungumza, tumekwenda zaidi ya Sh. bilioni 100 kwa mara moja na mipango yetu ni kufikia Sh. trilioni 1.40," alitamba.

Pia Kakoko alikiri kwamba miaka ya 2015 na 2016 bandari ilipitia kipindi kigumu ambacho ilifikia wakati baadhi ya watu kuanza kubeza kutokana na kupungua kwa shehena na mizigo.

"Mwaka 2015/16 kilikuwa ni kipindi kigumu, kilikuwa ni kipindi ambacho baadhi ya watu walipiga picha wakisema bandari imebaki magofu, kwa hiyo tunajivunia mpango tuliouweka wa kuongeza shehena ambayo haipungui tani milioni moja kwa mwaka," alisema.



Magari yakipishana kwa shida kutokana na taka zilizotelekezwa barabarani na kuleta usumbufu katika Mtaa wa Matumbi Tabata, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Serikali kuboresha sheria ya uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeanza kufanya maboresho ya sheria na sera ambazo zitachochea kuwapo kwa mazingira mazuri kwa wafanyabiashara na wawekezaji, hivyo kufikiwa kwa wakati azma ya uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

Akizungumza wa mkutano wa majadiliano baina ya serikali na sekta binafsi uliolenga kuangazia changamoto mbalimbali za wafanyabiashra na wawekezaji nchini mwishoni mwa wiki Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, alisema serikali ya Rais John Magufuli imejielekeza kuzifanyia kazi sera na sheria za uwekezaji.

"Azma ya serikali ni kujenga uchumi wa kati na viwanda, hatuwezi kufika huko kama wadau wa maendeleo kutoka sekta binafsi wanakuwa waathirika wa sheria zetu. Serikali imekusudia kuleta mabadiliko hayo ili kupunguza kiwango cha tozo, kodi na kiwango cha usajili katika Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC)," alisema na kuongeza:

"Mapendekezo ya maboresho ya sheria ya uwekezaji yanategemewa kuwasilishwa mapema kwenye bunge lijalo."

Waziri Kairuki alisema amefarijika kwa namna ambavyo wawekezaji na wafanyabiashara walivyoitika wito wa kuja kwa wingi katika majadiliano

hayo katika mikoa yote waliyopita mpaka sasa jambo ambalo limewapa mawanda mapana katika kushughulikia changamoto za wawekezaji.

"Mwitikio ni mkubwa jambo ambalo linaonesha ni kwa namna gani Tanzania tumepiga hatua katika kuwavutia wawekezaji, tutazifanyia kazi changamoto zote ambazo zimeibuliwa na wadau wa sekta binafsi hali ambayo itaongeza idadi ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi," alieleza.

Katika hatua nyingine Waziri Kairuka aliagiza mabaraza ya biashara ya mikoa na taasisi zote zinazohusika na uwekezaji kutoka maofisini na kufika kwa wananchi ili kuendelea kutoa elimu juu ya

mambo mbalimbali ambayo yamekuwa changamoto kwa wawekezaji na

wafanyabiashara.

"Hatuwezi kufika popote kama wataalamu wetu watabaki maofisini, huku

wawekezaji na wafanyabiashara wakihangaika kwa namna wanazojua wao,

natoa maagizo kwa idara zote za serikali zinazohusika na uwekezaji

kuwafikia walengwa popote walipo ili kuwarahisishia ufanyaji wa

shughuli zao hapa nchini," alieleza.

Waziri Kairuki alielezea kulidhishwa na kazi zinazofanywa na Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) hasa katika kuratibu na kuyasimamia mabaraza ya biashara ya mikoa na wilaya kwani yana mchango mkubwa kwa maendeleo na ustawi wa uchumi.

Waziri Kairuki aliongeza kuwa changamoto kubwa waliyokutana nayo kwa wafanyabiashara ni kutokuwa na ufahamu juu ya uwasilishaji wa changamoto wanazokumbana nazo kwenye shughuli zao jambo ambalo linaitia doa serikali wakati taasisi zinazosimamia uwekezaji zipo.


**HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

**MNADA WA UUZAJI WA VIWANJA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote kuwa zoezi la uuzaji wa Viwanja kwa njia ya Mnada litafanyika tarehe **14 Disemba, 2019** siku ya Jumamosi. Mnada utafanyika katika eneo la wazi la Manispaa ya zamani (karibu na Sabasaba) kuanzia saa 4:00 Asubuhi.

Viwanja vinavyouzwa ni Maeneo ya:

| ENEO | MATUMIZI NA BEI TSHS KWA (SQM1) |
|---|---|
| IYUMBU (New Town Centre) | • Viwanja vya Nyumba za kupangisha (Apartments)<br>• Viwanja vya Biashara<br>• Viwanja vya Viwanda Vidogo |
| NALA (Industrial Area) | • Viwanja vya Viwanda vya aina mbalimbali |
| NJEDENGWA (Investment Centre) | • Viwanja vya Nyumba za kupangisha (Apartments)<br>• Viwanja vya Biashara |
| NZUGUNI (Jirani na Uwanja wa Mpira, Soko Kuu na Stendi kuu mpya ya mabasi) | • Viwanja vya Hoteli<br>• Viwanja vya Biashara<br>• Viwanja vya Maduka makubwa (Shopping Malls) |

**NB**:

- Asilimia 50 ya Malipo italipwa siku ya Mnada
- Asilimia 50 inayobaki italipwa ndani ya siku 14 baada ya Mnada.

Tangazo hili limetolewa na:

**Mkurugenzi wa Jiji,**
**DODOMA**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Upendo, mshikamano daima mbele*

**MAADHIMISHO** ya miaka 58 ya Uhuru yaliyofanyika jijini Mwanza jana yameonyesha mshikamano wa hali ya juu kwa viongozi wa vyama mbalimbali vya siasa kuhudhuria na kuketi pamoja bila kujali itikadi zao.

Watanzania wameshuhudia sherehe hizo ambazo kwa mara ya kwanza zimefanyika Kanda ya Ziwa na kupambwa kwa maonyesho mbalimbali ya majeshi ambayo yalikonga nyoyo za wengi.

Tofauti na miaka ya nyuma kwa baadhi ya wanasiasa kususia sherehe hizo, mwaka huu zilipata mwamko wa hali ya juu kwa kuhudhuriwa na viongozi wengi wa kisiasa.

Viongozi hao pamoja na kushuhudia sherehe hizo lakini pia walipata nafasi ya kutoa salamu na ombi kubwa lilikuwa kuwapo na mshikamano wa kitaifa.

Wakati wa kutoa salamu kwa viongozi wa vyama vya siasa, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, alisema amehudhuria maadhimisho hayo kama uthibitisho wa ulazima wa kuwapo maridhiano yenye upendo na mshikamano katika taifa.

Katika salamu hizo amemuomba Mwenyezi Mungu akafungue milango na Watanzania wakaishi kama taifa linalopendana, kuvumiliana, kukosoana na kuruhusu demokrasia ili kujenga taifa lenye upendo na mshikamano.

Kadhalika katika salamu hizo amemuomba Rais John Magufuli kuweka historia ya maridhiano katika taifa kwa kuwa baadhi ya watu wanalalamika na wengine wanaumia kwa kuonekana kama kuna utengamano.

Mbali na Mbowe kiongozi mwingine wa chama cha upinzani ambaye alipata nafasi ya kutoa salamu zake katika maadhimisho hayo ni Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Pro. Ibrahim Lipumba, ambaye aliomba kuwapo na uhuru wa demokrasia katika kuelekea uchaguzi wa ujao wa mwaka 2020.

Licha ya kumpongeza Rais Magufuli kwa kazi nzuri anazofanya za kuimarisha uchumi, kujenga miundombinu, kufufua viwanda, ujenzi wa reli ya kisasa na mambo mengine mengi aliyoyafanya katika kipindi chake cha miaka mine akiwa madarakani, amemuomba kukumbuka jukumu la kujenga demokrasia nchini hasa nchi inapoelekea katika uchaguzi mkuu, mwakani.

Ni dhahiri kwamba salamu hizi za viongozi wa vyama vya siasa ni mwanzo mzuri wa kufikia maridhiano ya mshikamano wa pamoja na kuwa taifa lenye nguvu ya pamoja na upendo.

Mshikamano ulioonyeshwa kwenye sherehe za Uhuru ni wazi kuwa Watanzania ni watu wanaopenda amani, upendo na umoja na hawapendi nchi ikiingia katika machafuko kwa sababu ya vitu ambavyo vinaweza kuzungumzwa na kufikia maridhiano ya pamoja.

Fursa hii iliyotumiwa na wanasiasa hao ambao hapo awali ilikuwa ikiachwa inaonyesha kuwa Watanzania wanajitafakari sio tu kwa faida ya vyama wanavyotoka bali ni kwa faida ya wananchi ambao wanaongoza. Ni matumaini yetu kuwa tuendako mambo yataendelea kuwa mazuri na Watanzania wafaidike na matunda ya uhuru wao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# *Wazazi na walezi kazi ya kujenga madarasa ni yenu*



Na Sabato Kasika

**MATOKEO** ya mtihani wa darasa la saba mwaka 2019, yameshatangazwa, huku wanafunzi 701,038, ambao ni sawa na asilimia 92.27, wakiwa wamefaulu kuanza kidato cha kwanza mwaka 2020.

Katika ufaulu huo, kuna mikoa 13 ya Geita, Morogoro, Dodoma, Njombe, Katavi, Singida, Ruvuma, Tabora, Kilimanjaro, Kagera, Mwanza, Shinyanga na Mtwara ambayo wanafunzi wake wote wamefaulu kwenda sekondari.

Pamoja na ufaulu huo, kuna tatizo kidogo ambalo ni muhimu kulijadili na ikiwezekana lipatiwe ufumbuzi wa kudumu, badala ya kujirudia kila mwaka kana kwamba hakuna uwezekano wa kulimaliza.

Ninasema hivyo, kwa sababu wanafunzi 701,038, waliofaulu, wenzao 58,699 wamekosa nafasi, kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa, na serikali imeagiza ujenzi wa vyumba hivyo ufanywe haraka, ili waanze masomo.

Hii ni kwa mujibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ambaye alikaririwa na vyombo vya habari akisema hayo hivi karibuni.

Lakini, pamoja na hayo, ipo haja wazazi kumaliza tatizo la uhaba wa madarasa kwenye shule za umma, bila kusubiri wakati wote mkono wa serikali, kutokana na ukweli kwamba shule hizo ni zao.

Ushiriki wao uende mbali hadi kwenye uboreshaji wa miundombinu ya shule, ili kupunguza tatizo hilo ambalo linajitokeza kila mwaka.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari mwaka jana, Jafo alisema wanafunzi 133,747, sawa na asilimia 18.24 ya waliofaulu mtihani darasa la saba mwaka huo walichelewa kuanza kidato cha kwanza kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Sasa tatizo kama hilo limejirudia tena katika taarifa yake ya mwaka huu, hali ambayo inaonyesha kuwa kuna haja ya kuhimiza umma wa Watanzania kuona umuhimu wa kushiriki kwenye maendeleo ya shule za umma.

Ushirikiano wa wazazi usiishie kufuatilia kwa karibu maendeleo ya watoto wao shuleni bali washiriki katika kuboresha miundombinu ya shule ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, ili kumaliza kero hiyo.

Bodi za shule ziweke mikakati ya kusaidia kumaliza tatizo hilo, kwa kushirikisha wazazi kwa kutambua kuwa shule ni mali ya wazazi hawana budi kuzihudumia kwa hali na mali badala ya kuichia serikali tu.

Inawezekana kuwa wapo baadhi ya wazazi ambao hawataki kushiriki katika shughuli za maendeleo ya shule wakiamini kwamba kwa sasa jukumu lote ni la serikali, kwa vile imetangaza kugharamia elimu.

Mawazo ya aina hiyo hayaendelezi taifa kwa yeyote anayeju umuhimu wa elimu, hivyo wasiotambua hilo wasaidiwe ili wabadilike na hatimaye wachangie maendeleo ya shule hizo, ambazo ni mali yao.

Uzoefu unaonyesha kuwa hata zilipoanzishwa kambi za kitaaluma, baadhi ya wazazi waligoma kushiriki kutoa vyakula kwa ajili ya watoto wao, wakidai kwamba serikali imetangaza kutoa elimu bure.

Wazazi wa aina hiyo ndiyo hao, ambao hawaoni na wala hawatambui kuwa shule za umma ni zao, wana wajibu wa kuzihudumia ili kuhakikisha wanapunguza matatizo yanayozikabili bila kusubiri serikali.

Kimsingi ni kwamba wazazi wanapaswa kutambua kuwa shule za umma zinawategemea wao pia, wasikwepe kuzihudumia kwa visingizio kuwa serikali imeshatangaza kutoa elimu bure.

Elimu bure haijazuia wazazi na walezi kuchangia maendeleo ya shule kama, ambavyo baadhi ya watu wamekuwa wakidhani na kukwepa majukumu yao kwa ajili ya maendeleo ya shule na watoto wao kwa ujumla.

Kwa ujumla maendeleo ya shule na wanafunzi vinategemea wadau wote wa elimu wakiwamo wazazi na walezi, kwani wana wajibu wa kushirikiana na serikali kuhakikisha wanamaliza.

Julai mwaka huu Naibu Waziri Tamisemi anayeshughulikia elimu, Mwita Waitara, alisema serikali haijakataza michango shuleni, isipokuwa ya kulazimisha.

Alikuwa akifungua bwalo la chakula lililojengwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (CDTF), katika Shule ya Msingi Mlimwa, jijini Dodoma.

Alisema wapo watu wanapita mitaani na kutoa tafsiri potofu kuwa serikali imepiga marufuku michango yote shuleni jambo ambalo si kweli.

Kwa maelezo hayo ni wazi kwamba wazazi na walezi wanahusika kikamilifu kuzisaidia shule kupitia kamati na bodi za shule, kwa ajili ya kumaliza changamoto zinazozikabili ikiwamo uhaba wa madarasa.

## HABARI PICHANI

# SHAMRASHAMRA ZA MIAKA 58 YA UHURU



Sungusungu 1,200 kutoka wilayani Kwimba, Mkoa wa Mwanza, wakiwa katika sherehe za miaka 58 ya Uhuru na miaka 57 ya Jamhuri katika uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza jana.
**PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS**



Kikundi cha ngoma ya Ritungu kutoka mkoani Mara wakitumbuiza katika sherehe hizo.



Makomando wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) wakionyesha umahiri wa kupambana na maadui katika sherehe za miaka 58 ya Uhuru na miaka 57 ya Jamhuri katika uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.




Viongozi mbalimbali kutoka Tanzania Bara na Zanzibar katika maadhimisho hayo.



Wanajeshi wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) wakiwa katika gwaride la sherehe za miaka 58 ya Uhuru na miaka 57 ya Jamhuri katika uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.



Askari wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) wakiwa katika gwaride la sherehe za miaka 58 ya Uhuru na miaka 57 ya jana jijini Mwanza.

## HABARI KITAIFA

# Wapinzani, wanasiasa waibua mazito

INATOKA UK.2

sana kwa kazi njema, asante sana," alisifu.

**MBOWE, LIPUMBA**

Mwenyekiti wa Chadema, Mbowe, aliingia uwanjani hapo akifuatana na Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Kati, Lazaro Nyalandu, aliyewahi kuwa waziri katika serikali ya awamu iliyopita, pia walikuwapo baadhi ya wabunge wa chama hicho waliovaa sare zao za kombati.

Viongozi wa Chadema walisusia sherehe hizo kwa miaka iliyopita baada ya Rais Magufuli kuingia madarakani.

Baada ya kupewa fursa ya kuzungumza, Mbowe alitumia nafasi hiyo kueleza kuwa chama chake kimeamua kushiriki sherehe hizo kama ishara ya kurejesha umoja, upendo na mshikamano kwa Watanzania.

Mbowe alitoa rai kwa Rais Magufuli kuhakikisha anarejesha utangamano wa maelewano na maridhiano huku pia akiomba uhuru wa demokrasia.

"Nimekuja kushiriki sherehe za miaka 58 ya uhuru kama uthibitisho wa ulazima wa kuwapo maridhiano, kuwapo upendo na kuwapo mshikamano katika taifa letu.

"Nawapongeza sana Watanzania kwa siku hii ya leo na ninamwomba Mwenyezi Mungu siku ya leo ikafungue milango, tuweze kuishi kama taifa linalopendana, tuvumiliane, tukosoane, turuhusu demokrasia. Tukajenge taifa lenye upendo na mshikamano.

"Na Mheshimiwa Rais, una nafasi ya kipekee kuweka historia ya maridhiano katika taifa kwani kuna wengine wanalalamika, wengine wanaumia. Basi, Mheshimiwa Rais, tumia nafasi hiyo ukaliweke taifa katika hali ya utangamano. Nakushukuru sana. Asante sana!" Mbowe alihitimisha.

Awali, Mwenyekiti wa CUF, Prof. Lipumba, alidai haja ya alichokitafsiri kuwa uhuru wa demokrasia kuelekea uchaguzi mkuu mwakani.

"Nampongeza Rais kwa kazi aliyoifanya. Namwomba pia ajue kuwa ana jukumu la kujenga demokrasia katika nchi yetu, hasa tunapoelekea uchaguzi wa mwaka 2020," alisema.

Sherehe hizo pia zilihudhuriwa na maelfu ya wananchi na viongozi mbalimbali wakiwamo Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ali Mohamed Shein, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Spika wa Bunge, Job Ndugai, Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma, Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid na Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu.

Sherehe za maadhimisho hayo zilipambwa kwa gwaride rasmi lililoandaliwa na majeshi ya ulinzi na usalama, maonyesho ya ndege za vita, chopa, zimamoto na burudani za kwaya, ngoma za asili, dansi na bongofleva.

**HOTUBA YA RAIS**

Katika hotuba yake, Rais Magufuli aliwapongeza Watanzania wote kwa kuadhimisha miaka 58 ya tangu Tanzania Bara ipate uhuru na akawashukuru waasisi wa taifa wakiongozwa na Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere kwa juhudi kubwa walizozifanya kupigania uhuru.

Rais Magufuli alisema Watanzania wana kila sababu ya kujipongeza kwa kuendelea kudumisha amani, umoja na mshikamano katika kipindi chote cha miaka 58, akiwapongeza marais wa awamu zote nne zilizotangulia kwa kuiongoza Tanzania kwa mafanikio.

Aliyataja baadhi ya mafanikio ambayo Tanzania imeyapata baada ya uhuru kuwa ni kuongezeka kwa barabara za lami kutoka kilometa 1,360 hadi kilometa 12,679.55 na nyingine zaidi ya 2,000 ziko katika ujenzi, kuongezeka kwa vituo vya tiba (hospitali, vituo vya afya na zahanati) kutoka 1,098 hadi 7,293, kuongezeka kwa shule za msingi kutoka 3,100 hadi 17,379 na kuongezeka kwa shule za sekondari kutoka 41 hadi kufikia 4,817.

Maendeleo mengine ni kuongezeka kwa vyuo vikuu kutoka kimoja hadi kufikia 48, madaktari waliosajiliwa kutoka 403 (Watanganyika wakiwa 12) hadi kufikia 9,400, wahandisi kutoka wawili hadi 19,164, makandarasi kutoka wawili hadi kufikia 9,350 na pia wastani wa umri wa mtu kuishi kuongezeka kutoka miaka 37 hadi kufikia miaka 61.

Rais Magufuli alisema katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo serikali ya awamu ya tano anayoiongoza imedhamiria kuimarisha zaidi uchumi kwa kujenga viwanda ambavyo kwa miaka minne vimejengwa zaidi ya 4,000, kuimarisha miundombinu kwa kufufua reli na kujenga reli ya kisasa.

Pia, kujenga barabara, kupanua na kuboresha bandari, kujenga na kukarabati meli tano, kununua ndege 11, kujenga viwanja vya ndege 11, kujenga Bwawa la Nyerere litakalozalisha megawati 2,115 za umeme, kusambaza umeme katika vijiji vyote vya Tanzania, kuongeza hifadhi za taifa, kuinua uvuvi na kuimarisha usimamizi wa maliasili hasa madini.

Aliwashukuru Watanzania wote na wadau mbalimbali wa maendeleo kwa kuiunga mkono serikali katika juhudi hizo na akaahidi kuwa serikali itaendelea kuhakikisha uchumi wa Tanzania unakua, huduma za kijamii zinaboreshwa na Watanzania wananufaika na rasilimali za nchi yao.

# JPM asamehe wafungwa 5,533

INATOKA UK.2

wafungwa 5,533," alisisitiza.

Alitaja mikoa ambayo wafungwa wao wamesamehewa na idadi yake kwenye mabano ikiongozwa na Mkoa wa Kagera (713), ikifuatiwa na Dodoma (385), Morogoro (365), Dar es Salaam (293), Mara (260), Mbeya (259) na Kigoma (252).

Mingine ni Tanga (245), Geita (230), Rukwa (214), Arusha (208), Manyara (207), Tabora (207), Mwanza (190), Ruvuma (181), Singida (139), Simiyu (136), Lindi (129), Pwani (128), Iringa (110), Songwe (96), Katavi (74) Shinyanga (74) na Njombe (70).

Wananchi waliohudhuria maadhimisho hayo walionyesha kufuruhishwa uamuzi huo wa Rais na kuibua shangwe, vigelegele, na makofi.

Maadhimisho ya miaka 58 ya Uhuru yamefanyika jijini Mwanza kwa mara ya kwanza tangu kupatikana kwa Uhuru na kuhudhuriwa na idai kubwa ya watu, baadhi yao wakiamua kwenda uwanja wa Furahisha na Rock City Mall kufuatilia kupitia matangazo mubashara yaliyorushwa na vyombo mbalimbali vya habari baada ya kukosa nafasi ya kuingia ndani.

Baadhi ya wananchi waliohojiwa na Nipashe walieleza kufurahishwa na maadhimisho hayo.

"Leo ni siku ya historia kwangu, niliisubiri kwa muda hatimaye imefika na nimekuja hapa mapema alfajiri saa kumi na nimekuta baadhi ya watu wameshaingia," alisema, Lidya Erro, mkazi wa Ilemela.

"Mimi nimelala hapa ndugu yangu, ninakaa kule Ndagalu Wilaya ya Magu na niliona nikilala nyumbani usafiri wa kunifikisha hapa asubuhi na mapema hakuna, nisingewahi, ningekuta geti zimefungwa kwa hiyo nimekuja hapa jana, nikalala hapa 'uwanjani', asubuhi sijasumbuka kufuata usafiri wala sehemu ya kukaa," alisema Shihologanya Maliganya, mkazi wa Ndagalu, Wilaya ya Magu.

Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo viongozi wa serikali, waliostaafu, mabalozi wanaoziwakilisha nchi mbalimbali nchini na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama.

Maadhimisho ya mwaka huu yalikuwa na kaulimbiu 'Miaka 58 ya Uhuru na Miaka 57 ya Jamhuri, Uzalendo, Uwajibikaji na Ubunifu ni Msingi wa Ujenzi wa Uchumi wa Taifa Letu'.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Amina Shaban (wa pili kushoto), akikabidhi tuzo ya mshindi wa tatu katika kitengo cha benki kubwa za Mwasilishi Bora wa Hesabu zinazotolewa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Mahesabu (NBAA) kwa Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Fedha ya Benki ya Barclays Tanzania, Bernard Tesha, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Kulia ni Meneja wa Kitengo cha Usimamizi wa Fedha wa benki hiyo, Muhsin Kaye na kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya NBAA, Prof. Isaya Jairo.

# Wananchi wahimizwa kujiandikisha daftari la kudumu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk. Wilson Charles, amewataka wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandisha kwenye daftari la kudumu la wapiga kura ili wapate fursa ya kuchagua viongozi wanaowataka katika uchaguzi mkuu 2020.

Dk. Charles aliyasema hayo juzi wakati alipokuwa katika ziara ya kukagua uboreshaji wa uandikishaji wananchi kwenye daftari la kudumu la wapigakura mkoani hapa.

Alisema wananchi wanatakiwa kujitokeza kuitumia fursa hiyo ili kushiriki katika uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani unaotarajiwa kufanyika mwakani.

Alisema wananchi wanaotakiwa kushiriki kujiandikisha ni wale waliohama maeneo ya awali ya uchaguzi ambao watatakiwa kwenda katika vituo vya uandikishaji ili kubadili taarifa zao.

"Wengine ni wale ambao wamepoteza kadi zao za mpigakura waje wapatiwe nyingine, lakini ambao wamefikisha umri wa kupiga kura mwaka huu au watafikisha umri huo mwakani wakati uchaguzi utakuwa unafanyika," alisema.

Vile vile, alisema ambao majina yao yamekosewa wanatakiwa kwenda kufanya marekebisho, na waliojiandikisha lakini hivi sasa ni marehemu ndugu zao wanatakiwa kwenda kutoa taarifa ili waondolewe katika daftari la wapigakura la kudumu.

Alisema wameshaenda katika mikoa 15, kwa ajili ya kuandikishaji wananchi katika daftari hilo.

"Hivi sasa tupo katika Mkoa wa Dodoma kwenye wilaya za Dodoma, Bahi, Chamwino na Kongwa na tutamaliza mwezi huu tarehe 12, baada ya hapo Desemba 17 tutahamia Mpwapwa na wilaya za Chunya, Mbarali, Rungwe na Iringa wajiandae, baada ya hapo ni Ruvuma na Songea," alisema.

Pia alisema wanatarajia hadi mwezi Machi 2020, kuwa uandikishaji utakuwa umekamilika na daftari hilo kubandikwa katika maeneo mbalimbali.

HABARI MIKOANI

# Wafundwa kusaidia sekta ya gesi

**Na Mary Geofrey**

WAHITIMU 14 wa Shahada ya Uzamili katika masomo ya Uhandisi wa Mafuta na Uendeshaji Miradi na Uhandisi wa Sayansi ya Jiografia, waliofadhiliwa masomo na Kampuni ya Equinor, wametakiwa kutumia taaluma waliyopata kusaidia maendeleo ya sekta muhimu ya gesi nchini.

Wito huo, ulitolewa mwishoni mwa wiki na Makamu wa Rais Mwandamizi wa Equinor nchini, Dk. Mette Halvorsen Ottøy, katika hafla ya mahafali ya tano kwa wahitimu hao waliofadhiliwa masomo hayo yaliyofanyika jijini Dar es Salaam mwisho wa wiki.

"Equinor ina furaha kufanya kazi kwa kushirikiana na vyuo vikuu ili kufikia lengo lake la kujenga uwezo katika maendeleo ya sekta muhimu ya gesi nchini. Lengo letu ni kuona Watanzania wanapata mafunzo ili kuwa na sifa stahiki ili kutoa mchango wao katika ukuaji wa sekta hii kwa namna zote, moja kwa moja na isivyo moja kwa moja," alisema Dk. Mette.

Balozi wa Norway nchini, Elisabeth Jacobsen, alisema kupitia wahitimu hao wameweka historia nyingine kupitia mpango wa ANTHEI wa kuwawezesha wanafunzi wa Tanzania kusoma ndani ya nchi na Norway kwa masomo ya sayansi na jiolojia.

"Nadhani hili ni jambo zuri kwa ushirikiano baina ya Norway na Tanzania ndani ya miaka 15 hadi sasa, tumeshirikiana kuhakikisha tunafanya kazi pamoja kwenye sekta hii ya nishati," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya DTB-Tanzania, Viju Cherian, akiwa ameambatana na Mkuu wa Kitengo cha Uendeshaji wa Benki hiyo, Madhava Murthy, wakikagua kliniki ya utoaji huduma ya afya kwa wananchi wa eneo la Mbagala Mbande, jijini Dar es Salaam. Zoezi hili liliendeshwa na Klabu ya Lions kwa udhamini wa Benki ya DTB-Tanzania, Desemba 8, 2019. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chuo Kikuu Iringa chamtunuku Mkapa

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

CHUO Kikuu cha Iringa (UoI), kimemtunuku nishani ya heshima Rais mstaafu, Benjamin Mkapa na mkewe, Anna Mkapa kwa utumishi uliotukuka.

Walitunukiwa nishani hiyo katika mahafali ya 22 ya chuo hicho yaliyofanyika Jumamosi.

Mkuu wa Chuo hicho, Jaji mstaafu Augustino Ramadhani, alimtunuku nishani hiyo ikiwa ni kuthamini mchango wake katika kuanzisha vyuo vikuu binafsi nchini.

Alisema chuo chicho kimemtunuku nishani ya heshima Mkapa kwa kuthamini mchango wake wa kuanzisha vyuo vikuu binafsi nchini wakati wa utawala wake.

Jaji Ramadhani iliongeza kuwa UoI kimekuwa chuo kikuu binafsi cha kwanza kuanzishwa wakati wa utawala wake.

Wadau wengine waliotunukiwa nishani ya heshima ni Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela katika kuimarisha ulinzi, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM)Mkoa wa Iringa, Salim Abri, kwa kusaidia ujenzi wa mabweni na kuleta maziwa chuoni na aliyekuwa Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa chuo hicho (UoI-SO), Toima Lekeni kwa uongozi bora na kuimarisha usalama chuoni.

Katika mahafali hayo pia chuo kilitoa shahada ya juu ya heshima ya Sheria kwa Jaji Augustino Ramadhani na Shahada ya juu ya heshima ya Usimamizi na Utawala wa Biashara kwa Balozi wa Heshima wa Tanzania nchini Finland, Dk. Vesa Visa Viitanieni.

Zaidi ya wahitimu 1,600 walihitimu katika mahafali ya 22 ya UoI ngazi mbalimbali, ambapo mgeni maalum alikuwa Mkapa.

Mkapa alikishukuru chuo hicho kwa kumpa heshima hiyo, na kuwaasa wahitimu wote wa chuo hicho kwa kuwataka kutafakali kwa baadaye watakayoijenga Tanzania mtakayoijenga kuanzia sasa kwa kuzingitia hoja ya upendo, mshikamano na utaifa kwa maendeleo endelevu.

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa Chuo cha Iringa Prof. Ndelilio Urio, aliipongeza serikali kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma vyuo vikuu binafsi nchini.

Alisema serikali imetoa mikopo kwa wanafunzi waliopo katika vyuo vikuu binafsi na kuongeza kuwa serikali hiyo haijabagua wanafunzi wanaosoma katika vyuo vikuu vya serikali na binafsi.

Prof. Urio alisema chuo hicho ni moja ya vyuo vikuu ambapo wanafunzi wake wamenufaika na mikopo ya elimu na kuwataka pia wanafunzi hao kulipa mikopo yao watakapopata kazi.

# Watoto 1,000 kunufaika bima ya afya bure

**Na Joseph Mwendapole**

WATOTO zaidi ya 1,000 wanaoishi kwenye mazingira magumu wanatarajiwa kunufaika na bima ya afya ya bure ambayo watatakatiwa na Taasisi ya Time To Help.

Neema hiyo ilitangazwa mwishoni mwa wiki na Meneja Uhusiano wa Taasisi hiyo, Mbwana Kitendo, wakati alipokwenda kukabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwenye kituo cha kulelea watoto wenye ulemavu wa viungo na akili cha Baba Oleste Bunju A.

Taasisi hiyo iliandaa matembezi ya hisani ya kilomita mbili kwa ajili ya kuhamasisha jamii kuwajali watoto wenye ulemavu mbalimbali, kaulimbiu ikiwa ni watoto wote wana haki ya kuthaminiwa utu wao kama watu wengine.

Alisema taasisi hiyo imeona ni muhimu kuwakatia bima ya afya ili kuwaondolea usumbufu wanapoumwa kama sehemu yao ya mchango kwa jamii kwa kuwa watoto hao wanahitaji upendo na faraja kutoka kwa jamii.

"Mwakani tumepanga kuwakatia bima watoto 1,000 na kipaumbele chetu kitakuwa kwa watoto wanaolelewa katika kituo hiki cha Baba Oreste maana tunaamini hawa wanaweza kufanya kila kitu kama tutawajali na kuwawezesha," alisema.

Alisema taasisi hiyo pia imewapa bima zaidi ya watoto 50 visiwani Zanzibar ambao wanalelewa kwenye vituo mbalimbali vya yatima ili wasisumbuke wanapoumwa na 67 wanaolelewa kwenye kituo cha kulelea yatima cha Dogodogo Center cha jijini Dar es Salaam.

Alisema Time To Help ni taasisi ya kimataifa iliyoanzishwa mwaka 2006 nchini ikiwa na lengo la kuwasaidia wahitaji katika elimu, afya, chakula na malazi na kwamba wamekuwa wakisaidia upatikanaji wa maji kwa familia na shule mbalimbali nchini.

Naye Ismal Abdala, alisema jamii haipaswi kuwapuuza watoto wenye ulemavu kwa kuwa wakiwezeshwa na kuwekewa mazingira mazuri wanaweza kuja kuwa watu wakubwa kwenye jamii na kufanya mambo makubwa ya kushangaza.

"Ndugu zangu tusiwafiche majumbani watoto hawa kwa sababu kuna baadhi ya familia wanaona kama uchuro, hapana waleteni kwenye vituo kama hiki ambapo wanafundishwa mambo mbalimbali," alisema.

Kadhalika, alisema ni jambo la ajabu kuona baadhi ya watu kwenye jamii wakiwanyanyapaa watu wenye ulemavu kwani nao wana haki sawa na wanastahili kutunzwa, kupendwa na kuthaminiwa utu wao kama wengine.

"Jiulize kama wewe ndio ungekuwa kama hawa halafu wenzako wanakunyanyapaa kwa kukutenga ungejisikiaje? Kwa hiyo si jambo jema kuwatenga bali tuwapende na kuwawezesha ili wapate ujuzi na maarifa," alisema.

# Wakulima wakaidi pamba kukamatwa

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, ameagiza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Igunga kuwachukulia hatua za haraka wakulima wote wa pamba ambao wamekataa kung'oa miti ya pamba ya msimu uliopita.

Wakulima hao wamekaidi kufanya hivyo kwa madai kuwa hadi walipwe fedha zao za mauzo ya pamba.

Alisema kampuni za ununuzi wa pamba kuchelewa kuwalipa fedha zao hakuwezi kuwa sababu ya wao kuvunja sheria na kanuni zinazosimamia zao la pamba.

Mwanri alitoa kauli hiyo jana wilayani Igunga wakati wa ziara yake ya kuhamasisha kilimo cha pamba na kukuta baadhi ya mashamba kando kando ya barabara yakiwa na mabaki ya miti ya pamba ya msimu uliopita ikiwa imeanza kuchipua upya.

Alisema baadhi ya wakulima wamekata miti ya pamba bila kung'oa na wengine hawakung'oa wala kukata na kuifanya ianze kuchipua baada ya mvua kunyesha, kitendo ambacho ni uvunjivu wa sheria ya pamba na kanuni zake.

Aliongeza kuwa kibaya zaidi wengine wameanza kupalilia mabaki ya miti ya msimu uliopita iliyochipua, kitendo kinachoonyesha kuwa wanataka kuiacha ili ionekane kama pamba mpya.

Mwanri alisema vitendo hivyo ni hatari kwa maendeleo ya zao hilo kwa kuwa vinaweza kusababisha wadudu na magonjwa ya pamba ya msimu uliopita kuhamia katika pamba inayopandwa hivi sasa.

Aliwataka viongozi kuanzia ngazi ya wilaya hadi kitongoji katika Wilaya ya Igunga kuhakikisha wanafanya ukaguzi wa mashamba yote ili kuhakikisha wanaondoa mabaki ya pamba iliyopita.

Aidha, Mwanri alisema atarudi mara nyingine kuhakikisha kama hatua zimechukuliwa na kama akikuta hali ni kama ilivyo hivi sasa atalazimika kumchukulia kumsimamisha kazi kiongozi wa eneo husika na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria mkulima.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Igunga, John Mwaipopo, alisema wakulima wa pamba wa maeneo yote ambayo hawajalipwa fedha za pamba ya msimu uliopita wataanza kulipwa fedha zao.

Aliwataka kutumia fedha watakazozipata kwa ajili ya shughuli za maendeleo ikiwamo kufanya maandalizi ya kuwapeleka shule watoto wao na kuboresha kilimo cha pamba na mazao mengine. 0000000




Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Aidan Komba, akimkabidhi mkazi wa Arusha, Elizabeth Makala, mfano wa hundi ya Sh. milioni 5, baada ya kuibuka mshindi katika promosheni ya Tigopesa ya Kishindo cha Kufunga Mwaka, jijini, humo mwishoni mwa wiki. **PICHA:**

# Watakiwa kutunza fukwe za bahari

**Na Beatrice Shayo**

WANANCHI wameshauri kutunza mazingira na kufanya usafi katika fukwe za bahari.

Ushauri huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Mchungaji wa Kanisa la Christ Embassy, Ken Igini, akizungumza na wanahabari wakati wakifanya usafi ufukwe wa Kawe.

Mchungaji Igini alisema wameamua kufanya usafi katika eneo hilo ikiwa ni sehemu ya kusherehekea kuzaliwa kwa mchungaji wao.

Alisema kufanya usafi katika eneo hilo ni kuunga mkono jitihada za Rais John Magufuli kwenye utunzaji wa mazingira ya fukwe za bahari na kuwa nzuri kiusafi.

"Watu wanakuja kwenye hizi fukwe kwa ajili ya kupumzika na mazingira yake sio mazuri na ndio maana tupo hapa kwa ajili ya kufanya usafi. Rais Magufuli amekuwa akihimiza suala la usafi na jamii pia inatakiwa kutunza mazingira," alisema.

Naye Mchungaji Edwin Nyella alisema mazingira ni jambo muhimu katika afya ya kijamii na ndiyo maana wamekuja kufanya usafi ili kutoa mchango wao kwa serikali.

Alisema wameamua kufanya hivyo kwa sababu ni siku ya kimataifa kufanya chochote katika jamii ulimwenguni ikiwa ni sehemu ya kuzaliwa kwa mchungaji wao.

"Wito wetu ni kwamba jamii inahusika katika kuhakikisha mazingira yetu yanakuwa katika hali nzuri ili kuwe na maeneo mazuri ya kupumzika, hivyo ni muhimu kwa jamii kuunganisha nguvu na kuyalinda maeneo hayo kuwa katika hali nzuri.

**Watu wanakuja kwenye hizi fukwe kwa ajili ya kupumzika na mazingira yake sio mazuri na ndio maana tupo hapa kwa ajili ya kufanya usafi. Rais Magufuli amekuwa akihimiza suala la usafi na jamii pia inatakiwa kutunza mazingira**

# Serikali kukarabati shule aliyosoma Mwalimu Nyerere

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeamua kuifanyia ukarabati mkubwa Shule ya Msingi Mwisenge aliyosoma Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ili iwe sehemu ya historia ya Tanzania.

Akizungumza baada ya kutembelea shule hiyo juzi, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, amesema serikali imeamua kuifanya shule hiyo iliyopo kwenye Manispaa ya Musoma iwe sehemu ya historia ya Mwalimu Nyerere pamoja na historia ya Tanzania kwa ujumla.

"Shule hiyo haiwezi kubeba historia ya Mwalimu Nyerere, endapo majengo na miundombinu ya shule hiyo haitakarabatiwa na kujengwa upya," alisema na kuongeza kuwa: "Mipango ya kuifanya shule hiyo iwe sehemu ya historia ya Tanzania inaendelea serikalini; na kwamba historia ya Baba wa Taifa itapatikana shuleni hapo."

Alisema baada ya mchakato huo kukamilika, shule hiyo itaubeba Mkoa wa Mara na Tanzania kwa ujumla.

Alisema uamuzi wa kufanya shule hiyo kuwa yenye historia ya Tanzania unatokana na viongozi mbalimbali wa Tanzania kusomea shuleni hapo na kuwataja Waziri Mkuu mstaafu wa Tanzania, Jaji Joseph Warioba na Joseph Butiku kuwa miongoni mwa viongozi wa kitaifa waliosoma kwenye shule hiyo. Aliwapongeza viongozi wa Mkoa wa Mara kwa kusimamia matumizi ya fedha zilizotolewa na serikali kwa ajili ya shule hiyo na kuwataka viongozi wengine wa umma waige mfano huo.

Mapema, akitoa taarifa ya ukarabati wa shule hiyo, Mkurugenzi wa Manispaa ya Musoma, Fidelica Myovela, alisema manispaa yake inahitaji zaidi ya Sh. milioni 161 ili kukamilisha ukarabati wa shule hiyo ambao tayari umeanza.

Alisema hadi sasa wamepokea zaidi ya Sh. milioni 772.6 kutoka Tamisemi kwa ajili ya ukarabati huo na hadi sasa wamekwishafanya ukarabati kwa asilimia 85 ya kazi yote.

Alisema kati ya fedha hizo, jumla ya Sh. milioni 20 zilitolewa na Rais Magufuli, Septemba, mwaka jana ambaye pia aliagiza tathmini ya gharama za ujenzi na ukarabati wa miundombinu shuleni hapo ianze mara moja.

# RC ataka mfumo kidigitali Polisi kuwabaini wahalifu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, amelitaka Jeshi la Polisi kitengo cha usalama barabarani mkoani hapa, kutumia mfumo wa kidigitali katika kubaini makosa ya barabarani ili kurahisisha kuwabaini madereva wasiozingatia sheria.

Kauli hiyo, aliitoa jana wakati akizungumza na wadau wa usalama barabarani, askari polisi, wanasiasa na wanafunzi katika kongamano la usalama barabarani lililoandaliwa na Kamati ya Usalama Barabarani Mkoa wa Arusha.

Kauli mbiu katika kongamano hilo ni 'paza sauti, zuia ajali, okoa maisha'.

Gambo alisema lazima Mkoa wa Arusha uendeshwe kwa mfumo wa kidigitali kwa kufungwa kamera za kisasa maeneo muhimu ya barabara ili kurekodi matukio ya uvunjifu wa sheria za barabarani na kuweka kumbukumbu za taarifa za dereva wasiozingatia sheria.

"Tuna taarifa watu wanapata leseni kiujanja ujanja bila kupitia vyuo vya udereva, na kusababisha ajali ni vizuri Jeshi la Polisi likatumia mfumo wa kidigitali kubaini taarifa za madereva wasiotaka kutii sheria, " alisema Gambo.

Aidha, mkuu huyo wa Mkoa alilipongeza jeshi hilo kitengo cha usalama barabarani kwa kupunguza ajali za vifo kwa asilimia 10, jambo ambalo linatia moyo, huku akilitaka jeshi hilo kuweka mkakati wa mwaka ujao wa kupunguza zaidi ajali ili kufikia chini ya asilimia 50.

Pia Gambo alitoa onyo kwa madereva wa utalii wanaosafirisha wageni wakiwa wamelewa ambapo aliliagiza Jeshi la Polisi mkoani hapa kuwachukulia hatua kali za kisheria.

Awali, Katibu wa Kamati ya Usalama Barabarani Mkoa wa Arusha, Mary Kipesha, alisema ajali na vifo katika Mkoa wa Arusha zimepungua kwa asilimia 10, huku ajali za majeruhi zikiongezeka kwa asilimia mbili.

Akisema kwa kipindi cha Januari hadi Oktoba mwaka 2019, kulikuwa na ajali 47 zilizosababisha vifo vya watu 32 ukilinganisha na kipindi cha mwaka 2018, ambapo jumla ya ajali 52, zilitokea na kusababisha vifo vya watu 41.

Kipesha alisema tatizo linalosababisha ajali hizo, ni kutokuwapo kwa alama za barabarani, utambuzi wa vituo vya maegesho kwa daladala, machinga kufanyabiashara barabarani na kusababisha usumbufu kwa watumiaji wa barabara.

Aliziomba mamlaka zenye dhamana ikiwamo Halmashauri ya Jiji la Arusha, Tanroads na Tarura kuweka na kuchora upya alama za barabarani ambazo kwa kiasi kikubwa zimefutika, hatua hiyo itasaidia kupunguza ajali zisizokuwa na tija.

Katika hatua nyingine kamati ya usalama barabarani imekabidhi gari aina ya Land Cruise V8 kwa Mkuu wa Usalama Barabarani, (RTO) Mary Kipesha, kwa ajili ya kusaidia ofisi yake kutekeleza majukumu ya kikazi.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha, Baraka Simon, akiongea katika kikao cha kawaida cha madiwani cha kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya kwanza ya Julai –Septemba, 2019. **PICHA: WOINDE SHIZZA.**

# DC kuwapeleka watoto kupata elimu vyuoni

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WANANCHI wametakiwa kuwapeleka watoto vyuoni kupata elimu ambayo itazalisha wasomi na wataalamu waliobobea wakati nchi ikielekea kwenye uchumi wa kati na viwanda.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, wakati wa mahafali ya Chuo cha Veta cha mafunzo ya hotelia na utalii, na wanafunzi 89 walihitimu.

Muro alisema katika kipindi hiki cha kuelekea uchumi wa viwanda, ni lazima wazazi kuwapeleka watoto vyuoni na baada ya kuhitimu mafunzo watapata ajira ambayo itaisaidia serikali kufikia malengo ya kiuchumi.

"Tatizo linalowakabili wananchi wengi baada ya kuona viwanda na hoteli zimejengwa kwa wingi ndio wanaanza kupeleka watoto vyuoni, na hii imesababisha ajira nyingi katika viwanda na hoteli kuchukuliwa na watu kutoka nchi za nje kwa kuwa wao huwa walijiandaa mapema," alisema Muro.

Alisema serikali imejipanga kuwekeza katika uchumi wa viwanda na mpango huo utasaidia kuzalisha ajira kwa vijana nchini.

Mkuu wa Chuo hicho, Christopher Ayo, alisema chuo kimekuwa kikizalisha idadi kubwa ya wanafunzi ambao wamefanikiwa kupata ajira katika maeneo mbalimbali pamoja na kujenga mahusiano mazuri na vyuo vya ndani na nje ya nchi hususan vya utalii.

Ayo alisema kupitia ushirikiano huo, wamejenga uwezo mkubwa kwa wafanyabiashara hususani wakufunzi na utawala kwa kuandaa mitaala ya mafunzo ya uongozaji wa watalii na utoaji wa huduma.

Alisema chuo hicho, kupitia mradi wa ISTEP uliofadhiliwa na nchi ya Canada wamenunua vifaa vya utalii ikiwamo mahema, viwanda, vifaa vya kielektroniki na kompyuta 20, vitu vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 63.

Ayo alitaja matatizo yanayoikabili chuo ni upungufu wa kumbi za mihadhara na madarasa, hiyo imetokana na ongezeko la wanafunzi wengi.

"Chuo chetu tumejipanga kukabiliana na matatizo hayo, pamoja na kuongeza udahili wa kufikia 500 kwa mwaka wa masomo," alisema Ayo.

# Angalizo ung'oaji wa gugu karoti

**Na Daniel Sabuni,** ARUMERU

WATANZANIA wametakiwa kuwa makini wakati wa kung'oa gugu vamizi linalofahamika kwa jina la gugu karoti kitaalamu (Parthenium hysterophorus) kwani lina madhara ya kiafya kwenye mwili wa binadamu na wanyama.

Akizungumza na Nipashe, mwathirika wa gugu karoti, Ulinuru Palangyo anayeishi katika eneo la Meru wilayani Arumeru, alisema gugu hilo lilitokea shambani baada ya kuotesha karoti katika shamba lake mwaka 2018.

Alisema kadiri siku zilivyokuwa zinaenda, karoti zilikuwa zinakosa rutuba na gugu hilo linalofanana na karoti likazidi kustawi na lilipokomaa ndipo akaamua kung'oa kwa mikono na kuwalisha ng'ombe.

Palangyo alisema gugu hilo lilileta madhara makubwa kwake yeye kiafya kwa kupoteza fahamu na kutokana na mzio na mifugo kwani ng'ombe watatu walikufa.

"Mimi nilipelekwa hospitali nikadungwa sindano ya mshipa nikazinduka, mwanzo sikujua ni kitu gani kilichokuwa kinaendelea baada ya kutafakari na kuuliza wataalamu nikaelezwa kuwa jani karoti ndilo limesababisha mzio na ng'ombe kufa," alisema Palangyo.

Alisema bado hali ya muwasho wa ngozi bado haijaisha huwa inamrudia mara kwa mara na wakati mwingine kifua humbana kutokana na madhara ya gugu hilo.

Aidha, amewashauri Watanzania kuwa makini na gugu karoti kuliondoa shambani kwa kufuata ushauri wa wataalamu kwani madhara yake ni makubwa kwa afya ya mwanadamu.

"Mimi nimeshakuwa mhamasishaji wa kutokomeza gugu karoti, ukiliona shambani uliwahi kabla halijakomaa au kutoa mbegu, unatakiwa uling'oe kwa "gloves" na kulichoma moto mara litakapokauka, vinginevyo linaweza kukuathiri hata taratibu kimwili na hata mifugo," alisema Palangyo.

Charles Boniventure, bwanashamba katika Shirika la ECHO, alisema gugu hilo hutoa sumu za aina nne ambazo kwa kitaalamu ni "Parthenin, hymenin, hystenin na abrosin ambazo zina uwezekano mkubwa wa kudhuru wanyama na mifujo japokuwa bado utafiti unaendelea.

Hata hivyo Boniventure alisema kesi nyingi ambazo zimekuwa rikiripotiwa kuhusu madhara ya gugu karoti ni vifo kwa kondoo tofauti na ng'ombe na mbuzi.

Alimwomba Mkemia Mkuu wa Serikali kuwasiliana na wataalamu na hata wakulima na kupima madhara yanayodaiwa kusababishwa na gugu karoti kwa wanyama na mifugo ili kuchukua tahadhari na njia ya elimu zaidi ya usalama wa kupambana na udhibiti wa gugu hilo.

Utafiti unaonyesha kwamba asili ya gugu hilo ni Amerika Kusini, Kaskazini na India Magharibi na linaweza kuenea kwa kasi sana katika Bara la Ulaya na nchi za Canada, Australia na India.

Barani Afrika gugu hilo vamizi limeonekana kuleta adhari mbalimbali nchi za Afrika Kusini, Ethiopia na kusambaa kwa kasi kubwa Uganda Kenya na hatimaye Tanzania.

# Mali za KNCU zaanza kurejeshwa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MALI za Chama Kikuu cha Ushirika mkoani Kilimanjaro (KNCU) zilizokuwa zinadaiwa kuuzwa kinyemela, zimeanza kurejeshwa yakiwamo mashamba makubwa.

Taarifa iliyothibitishwa na Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini, Dk. Titus Kamani, inaeleza uamuzi wa kurejeshwa kwa mali hizo ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli.

“Kurejeshwa kwa mali hizo ni utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais John Magufuli la kutaka kurejeshwa kwa mali zote za wanachama wa vyama vya ushirika nchini, ambavyo vingi vimekufa kutokana na ubadhirifu mkubwa wa mali na mamilioni ya fedha za vyama vya ushirika nchini,” alisema.

Ingawa hakuyataja mashamba hayo kwa majina, Dk. Kamani alisema mali zilizorejeshwa mpaka sasa ni mashamba makubwa yaliyokuwa yakitumika kwa ajili ya uwekezaji na baadhi ya majengo yaliyokuwa yameuzwa kinyume cha taratibu za ushirika.

Akiwa katika Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI), Dk. Kamani alieleza lengo la serikali ni kuhakikisha vyama vyote vya ushirika ambavyo vimekufa kutokana na ubadhirifu uliofanya na viongozi, vinafufuliwa na kufanya kazi.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, wakulima wa kahawa katika mkoa wa Kilimanjaro katika miaka ya 1980, uchumi wao uliimarika kutokana na zao la kahawa.

Awali Mkurugenzi wa TaCRI, Prof. Deusdedit Kilambo, alimweleza Dk. Kamani kuwa hivi sasa kuna mwamko mkubwa wa wakulima kupitia vyama vya ushirika kutumia miche iliyofanyiwa utafiti na ambayo inakaa kwa muda mfupi na kuhimili magonjwa.

Prof. Kilambo alieleza zaidi kuwa tatizo kubwa linalojitokeza kwa sasa ni uhitaji mkubwa wa miche hiyo kwa wakulima ukilinganishwa na uzalishaji.

Mwenyekiti wa Bodi ya KNCU, John Boshe ambaye ni Mwenyekiti wa chama hicho kikuu cha ushirika cha Manushi/ Sinde, alieleza kuwa imani ya ushirika kwa wananchi imeanza kurejea na kwamba tatizo linalowakabili wakulima ni pamoja na athari za mabadiliko ya tabiachi ambayo wameanza kuyafanyia kazi kwa kufufua mifereji ya asili kwa ajili ya umwagiliaji.

## Dawa ya ulawiti, ubakaji Rombo

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

VITA dhidi ya watu wanaomaliza kienyeji mashauri yanayohusu masuala ya ulawiti na ubakaji katika Wilaya ya Rombo inazidi kushika kasi, baada ya kamati ya mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kuazimia kuundwa kwa sheria ndogo ya kudhibiti matumizi ya jani la ‘sale’ kwenye kesi hizo.

Uamuzi huo umepata baraka za Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo, baada ya kugunduliwa kwamba kesi nyingi za ulawiti, ubakaji na mimba za utotoni zinamalizwa kimila kwa kutumia majani hayo, badala ya kupelekwa mahakamani.

Hokororo alithibitisha kamati hiyo kutaka kuundwa kwa sheria ndogo ili kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia pamoja na ukwamishwaji wa haki pale ambapo wananchi wanauchezea uwanja wa utafutaji wa haki kisheria.

“Yaani unakuta kesi nyingi za ulawiti na ubakaji katika Mahakama ya Wilaya zimeshindwa kuendelea kutokana na mzazi hasa mama, anapoitwa kutoa ushahidi wamekuwa wanaficha ukweli, hivyo kufifisha haki za watoto wao hasa pale wanapoamua kukubaliana na kumalizana na watuhumiwa kwa kuombana msamaha kwa majani ya masale,” alisema.

Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo, Mrakibu Msaidizi (SSP), Ali Kitole, ambaye ni mjumbe wa kamati hiyo, alieleza hakuna kitu kinachomshangaza kama kesi za jinai kutatuliwa kimila hasa kwa kutumia majani ya sale.

“Watu hawaelewi tu kwamba haki jinai haitegemei mtu mmoja kupatikana, na wananchi ndio wamekuwa wakichangia kukwamisha mchakato mzima wa kupata haki, kwa kuwa mwathirika mwenyewe ndio anakuwa wa kwanza kutotoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi,” alisema Kitole.

Alipotafutwa kuzungumzia uamuzi huo wa kamati ya mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (Mtakuwwa), Mwenyekiti Jukwaa la Vuguvugu la Ukombozi wa Mwanamke Kimapinduzi (Tapo) Wilaya ya Rombo, Euphemia Masika, alisema kwa imani za Kichaga mtu yeyote aliyekosea akienda kuomba msamaha na jani la sale, huwa anasamehewa bila kujua kuna sheria za nchi zinavunjwa.



Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto anayeshughulikia Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu (kulia), akifungua kisanduku kuashiria uzinduzi wa kikoba cha kikundi cha wanawake cha Tuinuane, mbele ya Mwenyekiti wake, Anna Lusoloi (kushoto) wakati alipotembelea kujionea shughuli zinazofanywa na kikundi hicho kilichopo wilayani Monduli mkoani Arusha. **PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

## Viongozi wa dini waeleza umuhimu wa bima afya

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

VIONGOZI wa madhehebu ya dini wanaounda kamati ya dini mbalimbali, wamesema kama taifa hatuwezi kufikia kiwango cha uchumi tunachokitarajia iwapo mamlaka husika hazitaweka nguvu zaidi ya Watanzania kuelimishwa ipasavyo umuhimu wa kujiunga na bima ya afya.

Katibu Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Arthur Shoo, akizungumzia umuhimu wa bima hiyo jana, alisema ni lazima viongozi wa dini wajitose kuanzia sasa kuwahimiza waumini wao kutambua umuhimu wa kuwa na bima na siyo kuiachia mzigo huo serikali peke yake.

Shoo alikuwa akichangia mada kuhusu mchango wa bima ya afya kwa taifa, wakati mafunzo kwa viongozi wa dini yaliyoendeshwa na Shirika la Misaada la Makanisa ya Norway (NCA) mjini Moshi.

“Kwa hivyo ukiangalia matibabu ya sasa hivi yalivyo na gharama kubwa unapata wapi nguvu ya kukataa kujiunga na bima ya afya, mimi nasema ni lazima tuhamasishe wananchi wajiunge haraka na bima ya afya na tusiruhusu kona kona.

“Kuna kitu unaambiwa nenda kafanye MRI (vipimo vya uchunguzi vya Magnetic Resonance Imaging), unatakiwa sijui ukafanye nini mara nenda dialysis (uchunguzi wa damu) na huko utatumia pesa nyingi tu, na hizo pesa haiwezekani ukawa umeziweka mahali pengine ukawa unangojea uugue ndio uende.

Zaidi Shoo alisema: “Sasa unapokuwa na bima ya afya, ndiyo unakuta kwamba inakusaidia, utaenda hospitalini mapema kabla hujazidiwa sana. Tuiunge mkono serikali katika kuhamasisha wananchi kiunga na bima ya afya na nadhani hii ya sasa imeboreshwa zaidi.”

Mratibu wa Kamati za Dini mbalimbali, Edmund Matutai, alieleza kuwa katika utafiti walioufanya mwaka 2017/2018, waligundua kwamba ni Watanzania asilimia 32 tu wenye bima ya afya.

“Kamati ya dini mbalimbali inaendesha mambo yake kupitia utafiti, tulifanya utafiti mwaka 2017/2018 tukagundua kwamba ni Watanzania asilimia 32 tu ndio wenye bima ya afya. Asilimia 68 ya Watanzania hawana bima ya afya na katika hao, asilimia 28 ni watu maskini kabisa wale ambao hawawezi kupata milo mitatu ya chakula kwa siku moja. Hiyo ni sawa na kaya milioni tatu,” alisema Mtutai.

Kutokana na utafiti huo, NCA iliamua sasa viongozi wa dini watachukua jukumu la kusaidia hasa watu maskini kujiunga na bima ya afya, licha ya kwamba uwezo wao ni mdogo. Alisema iliwabidi watengeneza utafiti iliyoitwa ‘making possible’ kwa maana ya kwamba tufanye bima ya afya ni jambo linalowezekana.

Kaimu Shekhe Mkuu wa Baraza la Waislamu Tanzania (Bakwata) mkoa wa Kilimanjaro, Shaamban Mlewa, alisema Watanzania wengi wamekuwa hawafahamu umuhimu wa bima na hasa umuhimu wa bima ya afya, na ndiyo maana Bakwata pia imelazimika kuomba semina ya mafunzo kwa Maimamu wao ili wao wawe wawakilishi wazuri juu ya bima na wawape uelewa huo waumini wao.

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 10, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




Ukurasa 19

## Utolewe ufafanuzi zaidi kuhusu mahakama Afrika



Ukurasa 14

## Afrika kurudishiwa mali kale zilizoporwa

Ukurasa 18



Bila urafiki na mazingira majanga, maafa hayataisha



# Kigoma ilivyosheheni mbinu kutokomeza ukatili kijinsia

Ukurasa 16

ELIMU KUTOKA POLISI

# Shughuli za Jeshi la Polisi katika picha

KAMISHNA wa Operesheni na Mafunzo ya Jeshi la Polisi, Liberatus Sabas, amefanya ziara ya kikazi katika vituo vya polisi vya Newala na Tandahimba na baada ya hapo alizungumza na wananchi wa maeneo hayo ili kujua hali ya usalama kwa sasa.



Kamishna wa Operesheni na Mafunzo ya Jeshi la Polisi, Sabas, akipokelewa na maofisa na wakaguzi baada ya kuwasili katika kituo cha Polisi Newala mkoani Mtwara, katika ziara yake ya siku moja iliyokuwa na lengo la kuzungumza na askari wa kituo hicho. **PICHA: ZOTE NA JESHI LA POLISI.**



Kamishna wa Operesheni na Mafunzo, Sabas, akizungumza na wananchi pamoja na wakazi wa Newala katika ziara yake ya siku moja aliyoifanya maeneo hayo, lengo la ziara hiyo ilikuwa ni kuwashukuru wananchi kuwa ushirikiano wao wanaoutoa kwa vyombo vya ulinzi na usalama juu ya kukabiliana na uhalifu katika maeneo hayo.



Kamishna wa Operesheni na Mafunzo, akizungumza na wananchi pamoja na wakazi wa Tandahimba mkoani Mtwara katika ziara ya maeneo hayo, lengo la ziara hiyo ilikuwa ni kuwashukuru wananchi kuwa ushirikiano wao.

# Afrika kurudishiwa mali kale zilizoporwa

JOGOO mwenye historia yenye utata ambaye amesafiri kutoka Nigeria na kuhifadhiwa London sasa anatarajiwa kurudishwa nyumbani.

Jogoo 'okukor' alikuwa amehifadhiwa katika jumba la makumbusho la chuo hicho hadi 2016 , wakati wanafunzi waliposhinikiza aondolewe na kurudishwa Nigeria alikotoka.

Chuo cha Cambridge kilisema katika taarifa yake kwamba, sanamu hiyo ya jogoo iliibiwa kutoka mahakama ya Benin na kupewa chuo hicho 1905 na mwanafunzi wa Chuo cha Father of Jesus.

Kiliongezea kwamba saamu hiyo ni ya mahakama ya Benin wanakokuza utamaduni ya watu wa Edo.

Tangazo hilo limechochea wito zaidi ya vito vya zamani vilivyopo katika majumba ya makumbusho ya Uingereza kurudishwa katika mataifa vinakotoka baada ya kuibwa. Chuo Kikuu cha Cambridge kimetangaza kwamba kitarudisha shaba ya Benin, zilizoibwa kutoka mji mkuu wa Benin ambao ndiyo Nigeria ya leo. Amali hizo ziliibwa zaidi ya karne moja iliopita wakati wa uvamizi wa Uingereza.

'Tunazungumzia kuhusu shaba ya Benin, kutoka Afrika na Asia. Viliibwa', Alisema Profesa Kehinde Andrews kutoka chuo kikuu cha Birmingham.

Mjadala unaoendelea Uingereza uko sawa na wito unaoendelea kushika kasi katika maeneo mengine ya bara Ulaya , husussan nchini Ufaransa , ambapo Rais Emannuel Macron ameagiza kurudishwa kwa vito vya Afrika katika miaka michache ijayo.

Katika hafla moja iliofanyika mji mkuu wa Senegal Dakar, taifa hilo lilirudisha chombo kimoja- upanga uliokuwa ukimilikiwa na Omar Saidou Tall, ambaye alitawala maeneo ambayo yanajulikana kama Guinea, Senegal na Mali katika nusu ya pili ya karne ya 19.

Kwa sasa upanga huo umewekwa katika jumba la makumbusho la ustaarabu wa watu weusi katika mji mkuu wa Senegal Dakar.

Umehifadhiwa kwenye jumba la makumbusho kwa mkopo kutoka Ufaransa, lakini wabunge wa Ufaransa watapiga kura ya kuamua iwapo wataurudisha kabisa upanga huo pamoja na vito vingine.

Wakoloni wa Ufaransa waliiba hazina zilizokuwepo katika maadara ya Segou, Thiam alisema. "Ni matumaini yangu kwamba vitabu vyetu vilivyoko Ufaransa vitarejeshwa."

Wakati wa ukoloni Afrika, maelfu ya mabaki ya vitu vya kale vilivyoibwa kwa sasa vinaonyeshwa katika makumbusho ya Ulaya.

Lakini kuna baadhi ya taasisi ambazo zimekubali kurejesha vitu hivyo vya kale ikiwamo Shaba za Benin. Shaba kutoka Benin zinajumuisha michongo na mabamba ya kale hasa yaliyotengezwa kwa shaba ambayo yalipamba jumba la kifalme la Oba, Ovonramwen Nogbaisi, kwenye ufalme wa Benin, uliojumuishwa katika enzi za ukoloni wa Uingereza nchini Nigeria.

Wakati wa ukoloni wa Uingereza, inasemekana kwamba vitu vya kale 1,000 viliishia katika makumbusho mbalimbali kote duniani.

Mwaka jana, taasisi zilikubaliana kurejesha baadhi ya vitu hivyo kwa makumbusho mpya ya Kifalme huko Nigeria, inayotarajiwa kufunguliwa mwaka 2012.

**SIMBA WA TSAVO**

Simba wawili eneo la Tsavo nchini Kenya, waliowaua na kuwala wafanyakazi kadhaa wa shirika la reli mwishoni mwa karne ya19.

Mabaki ya watu hao, yalihifadhiwa na kupelekwa katika jumba la makumbusho la Chicago. Mamlaka nchini Kenya inataka irejeshewe mabaki hayo ya binadamu.

**JIWE LA ROSETTA**

Moja ya vitu muhimu vya kale vilivyopo kwenye makumbusho ya Uingereza, ni jiwe la zamani kama ubao lililochongwa ujumbe uliotoa taarifa muhimu kwa wataalam kufunza maandishi ya michoro ya Wamisri ya zamani.

Jiwe hilo lilichongwa mwaka 1801 baada ya jeshi ya Uingereza kushinda jeshi la Napoleon nchini Misri.Kwa miaka mingi, makumbusho ya Misri yamekuwa yakitaka jiwe hilo lirejeshwe.

**MALKIA WA BANGWA**

Malkia wa Bangwa ni mchongo wa mbao wenye urefu wa sentimita 81 kutoka Cameroon, unawakilisha nguvu na afya ya watu wa asili ya Bagwa.

Wajerumani walipewa sanamu hiyo au waliiba mwishoni mwa karne ya 20. Ni watu wengi waliokuwa nayo na hatimaye ikaishia katika makumbusho ya Dapper,Paris.

Ripoti rasmi ya Ufaransa imependekeza kwamba sanamu hiyo irejeshwe ilikochukuliwa nchini Cameroon. Kati ya asilimia 80 na 90 ya vitu vya makumbusho ya Afrika vipo kwenye makumbusho za kigeni, kulingana na ripoti rasmi ya Ufaransa iliyotolewa mwaka jana.

Inakadiriwa kuwa angalau karibia vitu vya kale 90,000 vilivyochukuliwa katika nchi za Afrika, hususan, za Kusini mwa Jangwa la Sahara na kwamba zipo kwenye makumbusho ya Ufaransa.

Makumbusho ya Quai Branly nchini Ufaransa pekee inasemekana kuwa na vitu vya kale 46,000 vilivyochukuliwa kimabavu.

Tangu ripoti hiyo ilipotolewa, baadhi ya vitu vya kale vilivyoibwa vinatarajiwa kurejeshwa kutoka nchi za Ulaya .

Mei mwaka huu, Ujerumani ilitangaza kwamba itarejesha alama ya jiwe kama msalaba iliyokuwa ikitumiwa na mabaharia ambayo iliwekwa katika pwani ya Afrika na Wareno mwaka 1496 hadi Namibia.

Vitu vya kale vya jamii ya wenyeji wa asili wa Australia pia vimerejeshwa. Hivi karibuni makumbusho ya Manchester yalirudisha vitu 12 kwa wenyeji hao. **BBC**

ELIMU

NA SABATO KASIKA

MCHAWI NI MLEZI

# Ni madereva wa boda, daladala, wageuka watetezi wa mabinti

KWA muda mrefu lawama za kuwarubuni mabinti kuanzia watumishi wa ndani, wanafunzi na wasichana kwa ujumla zimekuwa zikielekezwa kwa madereva na makondakta.

Wanaolaumiwa ni madereva na makondakta wa daladala mijini na vijijini, mabasi ya abiria mikoani tuhuma nyingi zaidi zinaelekezwa kwa bodaboda.

Hawa ndiyo ambao kutokana na kuwa na usafiri wakati wote, fedha za papo na kujiona kuwa wana umuhimu wa kipekee katika jamii kutokana na huduma wanazozitoa, wamekuwa chanzo cha kuwalaghai wasichana na kuwatumia kingono hata kuwapa mimba.

Lakini kama wahenga walivyosema "mchawi mpe mwanao amlee", wakimaanisha kuwa kufanya hivyo kutasababisha mchawi aogope kumdhuru mtoto huyo.

Ataogopa kumloga kwa sababu ya kuhofia kwamba atajulikana kuwa yeye ndiye aliyehusika katika tukio hilo, hivyo akikabidhiwa, atahakikisha mtoto anakuwa salama na kulindwa muda wote.

Msemo huo unaweza kulinganishwa na kile sasa kinachofanywa na baadhi ya madereva wa bodaboda na daladala, ambao wamekuwa wakituhumiwa kuwarubuni wanafunzi kwa lefti zinazolenga kufanya nao ngono ambazo huishia kuwapa ujauzito, ndoa za utotoni na maradhi , yote hayo yakikatisha ndoto za wasichana kusoma na kuhitimu kitaalamu.

Jijini Dar es Salaam, madereva takribani 800 wakiwamo pia makondakta wa daladala wamegeuka kuwa walezi na wanaotekeleza jukumu la kuwaelimisha na kuwalinda mabinti hasa wanafunzi dhidi ya uharibifu wowote unaotokana na ngono.

Wanawahamasisha, madereva wenzao na jamii kwa ujumla ili kuwalinda na kuepuka kuwarubuni wanafunzi na kufanya nao mapenzi.

Kazi hiyo wanaifanya chini ya taasisi ya kijamii ya Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (Wajiki) ya jijini ambayo imejikita kwenye wilaya za Kinondoni na Temeke.



Madereva wa bodaboda na daladala, wakiwa na mabango yenye ujumbe wa kupiga vita rushwa ya ngono. **PICHA: SABATO KASIKA**

### JUKUMU JIPYA

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Janeth Mawinza, aliyewaibua madereva hao, anasema, kabla kuwapa majukumu, alianzia kwa kuunda klabu za wanafunzi wa kike kwenye baadhi ya shule za msingi wilayani Kinondoni.

"Lengo lilikuwa ni kutaka kujua matatizo yanayowakabili wanafunzi wa kike kuanzia nyumbani, mitaani na hata shuleni, ndipo wengi wao wakaeleza kuombwa rushwa ya ngono madereva wa bodaboda na daladala," anasema.

> Lakini pia broo nikwambie, wapo baadhi ya watoto wa kike wameshindikana kwao, hao wanaweza kukuambia macho makavu kuwa uwape lifti halafu mtamalizana, sasa ukiwa mwepesi utakubali.

Anasema, klabu hizo zilianza mwaka 2015, na alipobaini hilo, yeye na timu yake waliandaa utaratibu wa kutembelea vijiwe mbalimbali vya madereva wa bodaboda na daladala ili kuwaelimisha.

"Elimu yetu ilikuwa ni kuhusu madhara ya rushwa ya ngono ambayo mwisho wake inaweza kuwa ni mauti kwa mwanafunzi au hata kwa dereva mwenyewe, hivyo tukawaomba waache tabia hiyo," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema, baadhi ya madereva waliipokea elimu hiyo na kuanzia kuwa mabalozi wa wenzao na kuanza rasmi kazi ya kuelimisha wenzao mwaka 2018 chini ya Wajiki.

"Hadi sasa wapo zaidi ya 800 wakifanya kazi kwenye Kata ya Makumbusho, wilayani Kinondoni na Mbagala Wilaya ya Temeke na tunatarajia kuingia Wilaya ya Ilala, Machi mwa kesho," anasema.

Anasema, madereva hao wameunda kamati zao za ulinzi ambazo huwa kwenye vituo vya mabasi, wakiwaona wanafunzi wanazagaazagaa wanawafuata na kuwauliza ili kujua matatizo yao. Mawinza anasema, iwapo mwanafunzi atakuwa ana tatizo la nauli au anazuiliwa kupanda gari, wanamsaidia ili awahi nyumbani, na kama hana sababu za msingi, wanamkamata na kumpeleka kituo cha polisi.

"Yaani kinachofanyika ni sawa na usemi wa "mchawi mpe mwanao amlee", kwani wale ambao wamekuwa wakilalamikiwa kuwarubuni wanafunzi, ndiyo wanafanya jukumu la kuwalea, na wamesaidia sana, " anasema.

Anasema, wiki iliyopita kulikuwa na mwendelezo wa mafunzo ya kuwajengea uwezo madereva hao ili kuwa mabalozi katika kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, ambazo zinamalizika wiki hii, ili wafanye kazi hiyo kwa ufanisi.

### KUJITAMBUA

Mkurugenzi Mawinza anasema, taasisi yake imechukua hatua hizo, ili kuhakikisha pande hizo mbili zinajitambua na kuvunja ukimya na kuwafanya wanaomba rushwa ya ngono waache, na waombwaji nao wabadilike na kutoa taarifa.

"Ikumbukwe kuwa rushwa ya ngono ina madhara mengi kwa wanafunzi ikiwamo udhalilishaji utu wa mtu na pia inauma na kuondoa nguvukazi ya taifa ambayo ni vijana, kwa kuambukizwa magonjwa ukiwamo Ukimwi," anasema.

Anasema, rushwa na ngono hasa kwa mabinti ni hatari kwa kuwa wengine hujikuta wakipata mimba zisizotarajiwa na hivyo kupata madhara makubwa wakati wa kujifungua kwa kuwa viungo bado havijakomaa.

"Wanaopata mimba za utotoni pia huathirika kisaikolojia, hivyo ni muhimu kuwalinda, ndiyo taasisi yetu inashirikiana na madereva hawa, ambao kwa muda mrefu wanalalamikiwa kuwarubuni wanafunzi," anasema.

Anasema, Sera ya Elimu Bure inayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano, ambayo imetoa fursa kwa watoto wengi wa kike kuandikishwa shuleni, ni muhimu jamii kusaidia kuitekeleza kwa kumlinda mtoto wa kike.

"Umbali mrefu na tatizo la usafiri kwa wanafunzi ni mojawapo ya sababu zinazochangia kuendeleza ukatili wa kingono kwa watoto wa kike wakiwamo wanafunzi, hivyo ni muhimu kuwa na mbinu za kusaidia," anasema.

### KWA MADEREVA

Dereva wa bodaboda ambaye pia ni mjumbe kutoka Wajiki, Khalfan Chusi, anasema baada ya kupata elimu, sasa wanaisambaza kwa madereva wenzao ili kuhakikisha wanafunzi wa kike hawarubuniwi.

Ukweli ni kwamba mchezo wa baadhi ya madereva kuwarubuni wanafunzi na kuwageuza kuwa wapenzi wao kwa sababu ya lifti ulikuwepo sana, lakini ninaamini unaanza kupungua," anasema Chusi.

Chusi anasema, hiyo inatokana na wao ambao wako chini ya Wajiki kwenda kwenye vijiwe na mitaani kutoa elimu ya kumnusuru mtoto wa kike dhidi ya rushwa ya ngono.

"Lakini pia broo nikwambie, wapo baadhi ya watoto wa kike wameshindikana kwao, hao wanaweza kukuambia macho makavu kuwa uwape lifti halafu mtamalizana, sasa ukiwa mwepesi utakubali," anasema.

Naye dereva wa daladala inayofanya ruti zake kati ya Mbagala na Kawe, Albert Shoo anasema, wanawake na wanafunzi ni waathirika wakubwa wa rushwa ya ngono, kutokana na shida ya usafiri jijini Dar es Salaam.

"Unaweza kuwakuta bado wanasota kituoni unampakia mmoja, hawezi kukataa, unamsomesha unaenda kufanya naye mapenzi kirahisi, lakini biashara hiyo haifai kufanywa na watu wanaojitambua," anasema Shoo.

Kwa upande wa Salum Hamza ambaye pia ni dereva wa daladala inayofanya ruti zake kati ya Makumbusho na Bunju, anasema mwanafunzi anapofika shuleni kwa wakati na kusoma kwa wakati ni jambo la msingi.

"Sisi hapa Makumbusho tumejiwekea utaratibu kwamba ni lazima kila daladala ichukue wanafunzi wanne, hatutaki wanyanyasike na wanaoshangaa vituoni bila sababu tunawakamata," anasema Hamza.

Anafafanua kuwa wakiwapo wanafunzi wa aina hiyo, huwafikisha kwenye ofisi za serikali za mitaa au polisi, lengo kuu likiwa ni kusaidia kuwaepusha na mambo ya rushwa ya ngono na hata vitendo vya ulawiti.

"Elimu hii ya Wajiki tuliopata imetusaidia sana, mimi hapa nilipo hata nikienda Tandika au kwingine nikakuta mwanafunzi wa kike ananyanyaswa na kondakta ama dereva, ni lazima niingilie kati kumsaidia," anasema.

ELIMU

**NA MAGRETH MAGOSSO, KIGOMA**

SIKU 16 GBV....

# Kigoma ilivyosheheni mbinu kutokomeza ukatili kijinsia

BAADHI ya wananchi wilayani Kasulu mkoani Kigoma, wanazo simulizi nyingi kuhusu mabadiliko yaliyofanywa katika dawati la jinsia la polisi linaloshughulikia matukio na kesi zinazohusu ukatili wa kijinsia.

Miongoni mwa mabadiliko yanayotajwa ni kuwapo faragha kwa watu wanaokwenda kutoa taarifa za changamoto wanazokutana nazo, pia jengo jipya kuwa na mazingira yenye sura ya kiraia tofauti na awali ambako lilikuwa na mazingira ya kipolisi na ya kuwaogofya.

Ofisa wa Dawati la Jinsia Kasulu, Maimuna Abdul, akizungumza na Nipashe, anasema maboresho yaliyofanywa yameongeza idadi ya waathirika wanaotoa taarifa za ukatili wa kijinsia. Sasa wamefikia asilimia 35 kwa mwaka 2011 na kufikia asilimia 48 kwa huu, 2019.

Wananchi wanalizungumzia dawati hilo wakisema limezaliwa upya na sasa ni msaada mkubwa kwa waathirika wa matukio ya ukatili wa kijinsia. Mfanyabiashara wa soko la Sofi, Nicodemas Kibona, anasema kabla ya maboresho utoaji taarifa ulikuwa na mwitikio mdogo kutokana na mazingira ya jingo.

Kibona anasema kuna faragha ambayo imewazesha watoa taarifa kuongeza kujiamini na kuwa na hakika ya kuwa salama hata wanapotoa taarifa zinazowagusa jamaa zao wa karibu.

"Unamshtaki mumeo, halafu ukirudi utaishi kwa nani? Familia zitapasuka lakini leo waathirika wanajua jinsi ya kutumia dawati la jinsia la polisi na waathirika wanaunganishwa na watoa haki," anasema Kibona.

Mkazi wa Mtaa wa Kimwoba, Tatu Mussa , anasema kumekuwa na manufaa makubwa kwa jamii kwani jengo lenye dawati la jinsia sasa lina mazingira huru hivyo wana ujasiri wa kwenda kutoa taarifa juu ya matukio yenye sura ya ukatili.

"Tangu uhuru mwaka 1961, tuliishi kwa kufuata mila na desturi ambazo nyingi zina viashiria vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake, na mwanamke hathubutu kwenda kituo cha polisi kumshtaki mumewe ilikuwa kazi lakini mabadiliko ya sasa yametujengea ujasiri,"anasema Tatu.

Philemon Herman, pamoja na kusifia jengo na huduma zinazowaweka pamoja polisi na maofisa ustawi wa jamii, anasema dawati limejenga mazingira huru yenye usiri wa mazungumzo .

"Dawati limekuwa msaada kwa wanawake na watoto ambao hulitumia kuelezea adha na vitendo vya ukatili dhidi yao, pia wanaume wengi wanakwenda pale kwa ajili ya kutafuta suluhu za kutatua changamoto za familia hasa zinazojitokeza kwenye ndoa,"anaeleza Herman.



Wanawake wakiwa kwenye kambi ya wakimbizi mkoani Kigoma. Kinamama hawa wanahitaji ulinzi ili kuepushwa na vitendo vya udhalilishaji.

> Unamshtaki mumeo, halafu ukirudi utaishi kwa nani? Familia zitapasuka lakini leo waathirika wanajua jinsi ya kutumia dawati la jinsia la polisi na waathirika wanaunganishwa na watoa haki.




Kinamama wakishiriki katika maandamano ya kupinga ukatili wa kijinsia. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

## MABORESHO

Maboresho ya dawati la jinsia la polisi lililounganishwa na Idara ya Ustawi wa Jamii mkoani Kigoma, yalifanywa chini ya Programu ya Pamoja ya Kigoma (Kigoma Joint Program - KJP).

Inatekelezwa na mashirika 16 ya Umoja wa Mataifa kama hatua ya kupunguza athari zilizosababishwa na wakimbizi mkoani humo.

Januari hadi Julai mwaka huu takwimu za Ofisi ya Ustawi wa Jamii zinabainisha kuwa zaidi ya wathirika 160 wa ukatili wa kijinsia walipatiwa matibabu ya aina mbalimbali kwenye vituo vya afya katika wilaya za Kigoma, Uvinza, Buhigwe, Kasulu na Kibondo.

Utekelezaji wa mpango wa maboresho ya dawati la jinsia ulizinduliwa rasmi Septemba mwaka 2017 na kukamilika kwake kunaongeza thamani ya utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (National Plan of Action for Violence against Women and Children - VAWC).

Mratibu wa KJP, Evance Siangicha anasema chini ya programu hiyo, mashirika 16 ya Umoja wa Mataifa yalitoa Sh. bilioni 2 katika Halmashauri za Wilaya za Kasulu, Kibondo na Kigoma kwa ajili ya kuimarisha madawati ya jinsia na uendeshaji wa shughuli za ulinzi kwa waathiriwa wa matukio hayo.

Mwaka 2016, serikali ilianzisha dawati la jinsia na watoto ndani ya vituo vya polisi, ikiwa ni sehemu ya kuboresha huduma ya makosa ya jinai yenye viashiria vya ukatili wa kijinsia, Siangicha alisema.

Siangicha anasema hata hivyo, kutokana na ukosefu wa usiri katika majengo yanayotumiwa na wasimamizi wa madawati ya jinsia, kumekuwa na mwitikio mdogo wa utoaji wa taarifa za matukio husika hivyo kuathiri ufanisi wa kitengo hicho. Kadhalika, kumekuwapo na taarifa kwamba waathirika wa matukio hayo wamekuwa wakishindwa kufika polisi na kutoa taarifa kwa hofu kwamba ndugu au wanafamilia wao watakamatwa.

Walihofia kuwa wangefunguliwa na mashtaka, tofauti na utaratibu wa sasa wilayani Kasulu ambao unatoa fursa kwa baadhi ya changamoto kumalizwa kwa sura ya usuluhishi.

Kabla ya jengo la kisasa la dawati la jinsia na watoto, wathirika wa vitendo hivyo walishindwa kupata haki zao kutokana na hofu ya kutengwa na familia na hata jamii hasa pale mhalifu alipobainika.

Kadhalika dawati halikuwa linatoa elimu ya jinsi ya kushughulikia kesi husika na hakukuwa na takwimu sahihi kuhusu vitendo hivyo, anaeleza Siangicha.

Mratibu anasema chini ya mradi huo msisitizo umewekwa katika maeneo matatu ya usalama kwa watoa taarifa hasa wanawake na watoto wanaofanyiwa ukatili, elimu kwa jamii ili ipate uelewa kuhusu madhara ya vitendo vya ukatili wa kijinsia na kuhamasisha malezi bora kwa familia na uwajibikaji katika mfumo wa sheria.

## KUONGEZEKA TAARIFA

Ofisa wa Dawati la Jinsia Kasulu, Maimuna Abdul akizungumza na Nipashe, anakiri kwamba jengo jipya limekuwa msaada mkubwa na kuongeza ufanisi wa kushughulikia kesi za ukatili wa kijinsia na waathirika kupata haki stahiki kisheria.

Anasema ongezeko la wanaotoa taarifa ni kubwa kutoka asilimia 35 mwaka 2011 hadi asilimia 48 mwaka 2019 na kwamba limechangiwa kwa kiasi kikubwa na jamii kuelewa athari ya vitendo hivyo na kuviripoti.

Alisema mwaka 2017 yaliripotiwa matukio 356 katika ofisi hiyo ambapo makosa ya ubakaji yalikuwa 53, kulawiti watoto 15, kuoa wanafunzi kesi tatu, mimba kwa wanafunzi matukio 22, ubakaji kwa kikundi ziliropotiwa kesi sita na kesi 278 zilikuwa za vipigo na shambulio dhidi ya wanawake .

Kwa mwaka 2018, Maimuna anasema kulikuwa na matukio ya ubakaji 46, vipigo 254, mimba kwa wanafunzi 22, kuoa wanafunzi manane na matukio ya kulawiti yaliripotiwa mawili.

Aidha anasema :"Mwaka huu 2019 kati ya Januari na Mei, yaliripotiwa matukio ya ubakaji 24, kulawiti sita, mimba kwa wanafunzi 21, kuoa wanafunzi kesi tatu na matukio 78 ya vipigo kwa wenza wa ndoa."

Ofisa Masaidizi wa Dawati , Tatu Juma, anasema pamoja na huduma nyingine, dawati hilo hutoa fomu namba tatu (PF3) ya polisi kwa ajili ya matibabu na ushauri kwa wanandoa pale wanapokwazana katika maslahi ya malezi ya watoto kwa kuwaelimisha ili, kupunguza migogoro ambayo inaweza kusababisha madhara na kuepusha kutokea kwa ukatili.

Tatu anaeleza kuwa Wilaya ya Kasulu inakabiliwa umaskini wa kipato unaochangiwa na ushirikina wenye madhara kwa familia. Anasema mfano halisi ni tukio la mwaka 2017 wakati binti mwenye umri wa miaka 11 alipopata ulemavu kwa kutolewa kizazi, baada ya kubakwa na baba yake mazazi ambaye alifanya hivyo kwa nia ya kupata utajiri kupitia biashara ya dagaa.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Kasulu, Godfrey Kapaya, anaeleza kuwa kabla ya dawati kuboreshwa, hawakuwa na ushirikiano ya uwajibikaji kati ya idara yake na maofisa wa dawati la polisi jinsia na watoto na kwamba hali hiyo ilichangiwa na mazingira na elimu duni juu ya kushughulikia matukio ya ukatili wa kijinsia.

"Sasa tunashirikiana kwa kila hatua ya shauri la mwathirika, utoaji wa taarifa umeongezeka na takwimu ya matukio yanashamiri kuongezeka,"anasema Kapaya.

Anaeleza kuwa ufanisi unachangiwa na maboresho ya mchakato mzima wa kushughulikia matukio ya ukatili kuanzia usiri au faragha, uharaka, weledi wa maofisa katika hatua zote za dawati na elimu kwa jamii kuhusu madhara ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Kapaya anataja mabadiliko ya mfumo wa sheria kuwa umeongeza kasi ya utoaji wa hukumu kwa wahalifu wa makosa ya ukatili wa kijinsia na kwamba kati ya Machi 2018 na Julai 2019, kesi 164 za ukatili dhidi ya watoto zilifikishwa mahakamani.

Anasema 68 kati ya hizo ziliwahusu watoto wa kiume na 96 ziliwahusu watoto wa kike.

Anasema kati ya hizo, kesi mbili washtakiwa walitiwa hatia na nyingine ziko katika hatua mbalimbali za usikilizwaji.

Septemba mwaka huu, dawati hilo imepokea kesi 49 za ukatili wa kijinsia zikiwamo 19 za vipigo kwa wanawake na kesi moja ya mwanamume kumwingilia mkewe kinyume cha maumbile, anasema.

Uzoefu unaonyesha wanawake wanaoingiliwa kinyume na maumbile na wenza wao, vipigo na ubakwaji, huripoti tukio katika dawati hilo kwa ajili ya kupewa fomu namba 3 (PF3) kwa ajili ya tiba tu, huku waathirika wakikwepa kusonga mbele kisheria kwa kufikisha mahakama wakikwepa 'aibu'.

Kifungu cha 131 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu (CAP 16 2006) kinatoa adabu ya kifungo cha maisha jela, pamoja na kuchapwa viboko kwa mtu anayepatikana na hatia ya kulawiti.

# Haki ya mtoto duniani ni daima ya leo na kesho



Watoto ambao ni sehemu ya jamii, wanastahili haki ya kutunzwa, kulindwa na kujaliwa katika misingi yote ya kibinadamu. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Padre Richard A.**

**Mjigwa, Vatican**

BARAZA Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 1989 lilipitisha makubaliano ya haki msingi za watoto duniani. Haki hizo ni pamoja na kutobaguliwa, haki ya kuzaliwa na kuishi, haki ya kukua na haki ya kusikilizwa.

Jumuiya ya Kimataifa haina budi kubainisha: sera na mikakati itakayotumika kuwalinda, kuwatetea na kuwaendeleza watoto, ili kupunguza vifo vya watoto wadogo pamoja na kuwakinga dhidi ya nyanyaso mbali mbali wanazokabiliana nazo katika maisha, malezi na makuzi yao.

Ili kufikia lengo hilo, kuna haja kwa Jumuiya ya Kimataifa kuendelea kuwekeza zaidi katika lishe bora, maji safi na salama pamoja na uhakika wa elimu bora na wala si bora elimu pamoja na kuwaandalia mazingira bora yatakayosaidia malezi na makuzi yao endelevu.

Jumuiya ya kimataifa iendelee kusimama kidete kulinda, kutetea na kuendeleza haki msingi za watoto, utu na heshima yao kama binadamu.

Watoto wajengewe mazingira mazuri ya maisha, kwa ajili ya ustawi na maendeleo yao kiroho na kimwili. Hizo ni changamoto zilizotolewa wakati wa kuadhimisha Siku ya Haki za Mtoto Duniani kwa mwaka 2018.

Ikumbukwe kwamba, watoto ni matumaini ya binadamu leo na kesho, umuhimu wa kuwalinda watoto mwaka 2017 ulitangazwa "Mwaka wa Kulinda na Kudumisha Utakatifu wa Watoto"

Vita, kinzani, migogoro na mipasuko ya kijamii, matokeo yake ni maafa na majanga makubwa katika utu na heshima ya binadamu; ukosefu wa usawa na haki jamii.

Watoto wa sehemu mbalimbali za dunia wanajikuta wakiwa wamezungukwa na madhara ya vita, dhuluma, nyanyaso, ubaguzi, magonjwa, njaa na umaskini wa kutupwa.

Ni matarajio Jumuiya ya Kimataifa italinda haki msingi za watoto ikiwa ni pamoja na uhai wao, elimu, afya na malezi bora, ili kuwa na matumaini ya leo na kesho iliyo bora zaidi.

Siku ya Mtoto Duniani huadhimishwa kila mwaka ifikapo tarehe 20 ya mwezi Novemba, ili kukuza uelewa na kudumisha haki za msingi za mtoto, ambazo ni kuishi, kuendelezwa, kushirikishwa na kulindwa.

Katika athari za mabadiliko ya tabianchi, ustawi, maendeleo na makuzi ya watoto sehemu mbali mbali za dunia, kimsingi watoto ndio waathirika wakuu wa mabadiliko hayo.

Ukosefu wa maji safi na salama una madhara makubwa kwa afya ya watoto wengi duniani, kama ilivyo pia kwa ukame wa kutisha na baa la njaa inayosababisha utapiamlo wa kutisha kwa mamilioni ya watoto duniani.

Inakadiriwa, kuna watoto zaidi milioni 500 wanaoishi katika maeneo yaliyokumbwa na mafuriko sehemu mbali mbali za dunia; wengine milioni 160 wanaishi katika maeneo yaliyokumbwa na ukame wa kutisha na wengine zaidi ya milioni 115 wanaishi katika mazingira hatarishi yanayoweza kukumbwa na tufani.

Takwimu zinaonyesha kila mwaka, athari za mabadiliko ya tabianchi zinatishia usalama na maisha ya watoto zaidi ya milioni 1.7.

Ikumbukwe kwamba, athari za mabadiliko ya tabianchi ni kati ya sababu kubwa zinazochangia uwepo wa idadi kubwa ya wakimbizi na wahamiaji wanaotafuta: usalama, hifadhi na maisha bora zaidi.

**Kwa mujibu wa mtandao wa vaticannews.va.**

SAYANSI

NA DK FELICIAN B. KILAHAMA, WCT



Misitu ni rasilimali muhimu kwa vile ndicho chanzo cha mvua, hewa safi na nishati kuni. Bila ulinzi wa misitu kuna hatari ya taifa kugeuka jangwa. **PICHA: MTANDAO.**

# Bila urafiki na mazingira majanga, maafa hayataisha

KUNA usemi usemao "hakuna lisilowezekana chini ya jua". Huwa najiuliza chimbuko la usemi huo ni nini? Jibu kamili sina, pengine kilichomanishwa ni kuwa na ari ya kutaka kufanikisha kile cha muhimu katika maisha. Vilevile, ni kama kusema "penye nia pana njia" kwa msingi kwamba ukiwa na uthubutu wa kweli utafanya na kufanikiwa.

Yote heri isipokuwa tujitahidi tukimtanguliza Mwenyezi Mungu au kwa maneno mengine "Mungu Kwanza" kabla ya yote. Hii ni muhimu sana maana yeye ndiye aliyetuumba na binadamu bila kuwapo nguvu ya Mungu au Uwezo wa Kimbingu juu yetu ni sawa na kazibure.

Namshukuru sana Mungu kwa kutofautisha binadamu na viumbe wengine kwanza, kwa kutuumba kwa sura na mfano wake, hii ni heshima kubwa kwetu. Mungu amewapa wanadamu uwezo wa kumiliki na kutawala rasilimali zote duniani isipokuwa kukatazwa kula matunda ya mti uliokuwa katikati ya "Bustani ya Edeni".

Hata hivyo binadamu alishindwa kutii amri hiyo na kusababisha udhaifu kwenye kumiliki na kutawala hivyo kupelekea laana kumwandama binadamu mpaka leo.

> Kwa miaka ya nyuma mvua zilikuwa zinanyesha za kutosha nakumbuka nikiwa kijana miaka ya 1950s na 1960s mvua za masika zilikuwa nyingi kiasi cha kushindwa kupata kuni za kupika chakula.

### ATHARI ZA EDENI

Halihalisi tunayoishuhudia nyakati hizi zenye maafa mengi dunia ni matokeo ya udhaifu uliojengeka miaka mingi sana kutokana na kutotii pamoja na kujengeka ubinafsi zaidi kuliko kuwapo mtazamo halisi wa kutumia rasilimali tulizopewa na Mwenyezi Mungu kwa misingi endelevu na kwa faida ya wanajamii wote au kwa maslahi mapana ya taifa letu.

Kwa hali hiyo shughuli nyingi za kibinadamu mijini na vijijini; zimekuwa na matokeo hasi kwa mazingira. Mathalani, ukataji ovyo wa miti na ufyekaji wa misitu ya asili bila kufuata kanuni za Uhifadhi wa Mazingira, kuchoma mapori moto au kutotekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi vijijini: kumesababisha misitu ya asili na uoto juu ya ardhi kutoweka.

### WAKATI WA UHURU

Kabla na baada ya kupata uhuru hali ya mazingira nchini ilikuwa ni ya kijani sana ukilinganisha na ilivyo sasa. Ingawa idadi ya watu ilikuwa chini ya milioni 10 wakati unapatikana na mwaka 1961 sasa inakadiriwa kuwa milioni zaidi ya 55 na mifugo zaidi ya milioni 35; hatuwezi kusema ongezeko hilo ndiyo sababu kubwa ya kupelekea uharibifu wa mazingira kuwa mkubwa kiasi hicho.

Ukweli ni kwamba kushindwa kumiliki na kutawala vyote kwa kutumia njia endelevu. Kukosekana utayari wa kutumia rasilimali asilia ikiwamo misitu; wanyamapori; ardhi, maji, samaki na kadhalika, kwa misingi endelevu.

Ndicho chanzo kikubwa kupelekea maafa kuongezeka. Sasa tunalia na athari za mabadiliko ya tabianchi kumbe kisababishi ni kazi za mikono yetu na kupelekea ongezeko kubwa la joto duniani, matokeo ni maafa kila mahali ikiwemo bara la Afrika kukumbwa na njaa, ukame, mafuriko, kupoteza uhai na mali kama nyumba kubomoka au kuezuliwa paa.

### MISITU KUTOWEKA

Uoto wa asili kwenye nchi za Afrika ikiwemo Tanzania umetoweka kwa kasi kubwa sana. Tanzania kwa mfano, inakadiriwa kupoteza misitu ya asili kwa kiwango cha hekta kati ya 370,000 na 470,000 kwa mwaka kutegemea hali halisi ya mahalia (locality).

Hivyo maeneo mengi nchini hayana uoto wa asili kama ilivyokuwa miaka iliyopita. Kila kukicha uoto wa asili: nyasi, mimea, miti na misitu vinapotea kwa kiwango kikubwa. Ndiyo maana kwa nyakati hizi, tofauti na zamani, mvua ikinyesha baada ya muda mfupi tu mafuriko yanatokea. Vilevile, msimu wa mvua ukiisha baada ya muda mfupi upatikanaji wa maji unakuwa wa shida (chemichemi zinakauka na mito mingi kuwa na maji kidogo).

Kwa nini kumekuwepo na athari hizo nyakati hizi kuliko zamani? Binadamu, pamoja na idadi ya watu kuongezeka, hatuishi kirafiki na Mazingira au hatumiliki na kutawala kwa kuzingatia misingi sahihi, na badala yake tumekuwa waharibifu kwa Mazingira na sasa yanatugeuka na kutuangamiza.

Kwa miaka ya nyuma mvua zilikuwa zinanyesha za kutosha nakumbuka nikiwa kijana miaka ya 1950s na 1960s mvua za masika zilikuwa nyingi kiasi cha kushindwa kupata kuni za kupika chakula.

Kaya nyingi zililazimika kuweka kuni za kutosheleza mahitaji nyakati za masika kinyume cha hapo "mtapiga miayo" kutokana na njaa kwa kukosa nishati ya kupikia kisa mvua nyingi wakati wa masika.

Wakati hali ni hivyo mafuriko makubwa au kubomoka madaraja ilikuwa nadra sana tofauti na hali ilivyo sasa. Hali ilikuwa salama zaidi kuliko sasa maana tulikuwa bado tunaishi kirafiki na mazingira hivyo uoto wa asili ulikuwapo wa kutosha.

Kwa maneno mengine, kukiwapo na uoto wa asili wa kutosha maji ya mvua huingia ardhini taratibu na hatimaye kutiririka kwenye mito hata nyakati za kiangazi lakini pia ardhi au udongo kuhifadhiwa. Hivyo kutokuwapo uoto wa asili wa kutosha kumeleta athari kwa ardhi na upatikanaji maji nyakati za kiangazi ni kubwa sana.

Ongezeko la watu au mifugo kwa mtazamo wangu havijawa tishio kwa maisha yetu na hasa tukizingatia kuwa Tanzania Bara inayo aneo kubwa takribani hekta zaidi ya milioni 88. Kwa idadi ya watu milioni 55 ni sawa na kila mtu kumiliki hekta taribu 1.6 na familia ya watu 10 watakuwa na hekta 16.

Kwa idadi ya mifugo takribani milioni 35 ni sawa na mtu mmoja kuwa na mfugo mmoja. Hii inaonyesha kuwa kiuhalisia bado ardhi inatosha isipokuwa matumizi yake siyo endelevu.

Sehemu mbalimbali nchini tunalima kwa kufyeka misitu ya asili (kilimo cha kuhamahama), hatufugi tunachunga mifugo; ardhi inatumika kama haitakiwi kwa vizazi vijavyo.

Matokeo yake ni kutoweka uoto wa asili na hivyo maji ya mvua kusababisha mmomonyoko mkubwa wa udongo. Matokeo yake ni ukame na njaa kutokama na kilimo duni. Maji ya mvua yakishindwa kuingia taratibu ardhini husomba udongo na kila aina ya takataka na kupelekwa mabondeni na kwenye mito.

Madaraja na barabara kubomoka ni matokeo ya maji ya mvua kutoingia ardhini na badala yake kujaza mito haraka. Isitoshe njia za asili ambazo maji ya mvua hupita zimezibwa hivyo kusababisha maji kuzagaa sehemu ambazo hayastahili kuwapo. Maji yanapokuwa mengi ana nguvu sana na yanapofika kwenye madaraja na kwa sababu kina cha mto kimepungua sana maji hupita kwa shida hivyo kusambaa juu ya daraja na wakati huo yakimomonyoa udongo ulioshikilia nguzo za madaraja hatimaye hubomoka na kusababisha hasara kubwa sana.

### ATHARI/KUJIANGAMIZA

Tukubali kuwa sasa hali siyo rafiki maana matokeo ya kutoishi kirafiki na mazingira yanakuwa mwiba kwetu kiasi cha kusababisha madhara makubwa kwa jamii na taifa zima. Tujirudi turekebishe tulikokosea.

Tuzingatie matumizi sahihi ya rasilimali ardhi; tulime kitaalam na kilimo kiwe kijani (green faming), kingo za mito zihifadhiwe na sheria zisimamiwe ipasavyo.

Tuwe wafugaji bora badala ya mazoea ya kuchunga mifugo na tuhakikishe tunazalisha mazao ya kilimo au mifugo kwa tija kubwa kwa kutumia eneo dogo la ardhi. Kwa ufupi: tufanye yote kwa kuzingatia umuhimu wa kuishi kirafiki na mazingira ili tuepuke vifo na kupoteza mali kwa sababu mazingira yakiharibiwa yanalipiza kisasi bila huruma. Tuchukue hatua sasa na kutimiza wajibu wetu ipasavyo kwa kufanya kazi kwa bidii huku tukitunza mazingira kwa faida yetu na vizazi vitakavyofuata.

***Dokta Felician B. Kilahama ni Mwenyekiti, Taasisi ya Uhifadhi wa Maliasili na Mazingira (WCST).***

ELIMU

NA ANIL KIJA

# Utolewe ufafanuzi zaidi kuhusu mahakama Afrika




Majaji wa Mahakama ya Afrika wakiwa kwenye makao makuu ya taasisi hiyo yaliyoko Arusha. **PICHA: MTANDAO.**

WASEMAJI wa masuala ya sheria na katiba nchini wamekuwa na kazi ya ziada hivi karibuni ya kutofautisha kati ya serikali na wasimamizi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Wananchi.

Suala ni licha ya kuwa mahakama hiyo iliundwa na maskani yake yakawa Arusha mapema miaka ya 1980, zipo tofauti kati ya mpangilio wake na utendaji wake.

Mara nyingine utendaji hufuata mawimbi ya kiitikadi yanayovuma wakati huo na siyo mpangilio halisi wa kuundwa kwake karibu miaka 40 iliyopita. Ndicho anachojaribu kueleza Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro, kupitia vyombo vya habari, wakati suala hilo linavuma safari hii.

Anasema kanuni ya msingi ya mahakama hiyo ni kufuata mlolongo wa kisheria katika nchi halafu ikiwa imeukamilisha na kuna malalamiko au rufani inatakiwa, ndipo mhitaji anaweza kufungua shauri katika mahakama hiyo.

Kinachotokea ni kuwa wahusika wanaotaka kupeleka kesi mahakamani dhidi ya serikali wanaeleza kutokuwa na imani na sheria au hata mahakama za nchi na kwa maana hiyo mahakama hiyo ya kimataifa inakuwa kimbilio halisi.

Anayejua diplomasia inavyoendeshwa anaelewa kuwa Mataifa ya Umoja wa Afrika (AU) hazingeweza kuunda mahakama mbadala wa mfumo wa mahakama wa nchi zao ila kuweka chombo kingine ambacho kinaendana kwa kiasi kikubwa na mifumo yao.

Kwa vile Mahakama ya Afrika ina kitu kama nafasi ya uhakiki na mapitio ya kile kinachofanyika na mahakama za wanachama wa AU tofauti katika mausala yanayaogusa haki za binadamu, ni lazima kuwe na misingi au angalau marejeo ya pamoja ya kiitikadi.

Wakipishana sana inakuwa vigumu kuendesha mazungumzo, ndiyo hapo nchi inaamua kujitoa katika utaratibu huo kwa muda, hadi tofauti hizo zitakapoangaliwa upya.

Kipengele kimoja cha kufikisha kesi kwenye Mahakama ya Afrika bila kupitia Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani kinaweza kuwa ni kupewa uwezo msajili wa kesi au Msajili wa Mahakama kuwa na uwezo wa kuamua kupokea kesi au kuikataa.

Ina maana kuwa halazimiki kuhitaji mrejesho wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani kwanza.

Hatua nyingine ya kuanzia ni lazima iendana na ile ya kwanza pale mlalamikaji anapokubaliwa na mahakama kuwa sheria za nchi husika, kwa ujumla wake au katika kipengele maalum kinachogusa haki za binadamu, ni kinyume dhana au itikadi ya kuundwa kwa Mahakama ya Afrika.

Ina maana shauri likipelekwa huko ni sawa na bure kwani halitasikilizwa kwa kanuni zinazotambuliwa na mahakama hiio. Siyo za nchi tena.

Unaweza kujiuliza ni vipengele gani vilikuwepo wakati Mahakama ya Afrika inaanzishwa, na kukubaliwa (akiwa mwenyeji) na Waziri wa Sheria na Katiba wakati huo, Joseph Warioba, na miaka kadhaa baadaye akiwa amemaliza kipindi chake cha uwaziri mkuu akawa jaji katika mahakama hiyo. Sasa ni kwa msingi wa sheria zipi Jaji Warioba alikuwa mwenyeji katika uanzilishi wa mahakama hiyo na baadaye kuwa jaji, halafu mmoja wa warithi wake baadaye anaona hana njia ila kulishauri Baraza la Mawaziri kuwa Tanzania ijitoe kwa muda hadi mfumo wa kisheria umewekwa sawa?

Jibu rahisi ni kuwa yako mabadiliko, ya mwelekeo wake kiitikadi. Kuwekwa kipengele cha kumaliza mfumo wa kisheria au mahakama ndani ya nchi kabla ya kuhitaji msaada katika mahakama ya kimataifa ni jambo la kawaida, lakini mahakama hizo kwa kawaida pia zinakuwa na uhuru wa kukubali kesi bila mrejesho unaokubalika kutoka mahakama za nchi husika.

Kutaka mrejesho ni kama kuomba kibali kuwa shauri hilo lipokelewe, wakati kila mahakama au jopo la kisheria huwa na mifumo ya kisheria ya kukubali au kukataa shauri kutoka popote.

Ina maana kuwa nchi inaweza kutia saini 'protokali' ya kuundwa kwa mahakama kama hiyo (ya kimataifa) na huku ina mashaka na vipengele kadhaa. Endapo haitatokea mikwaruzano dhahiri, nchi hiyo inaendelea na uanachama ikijua mahakama hiyo iko huru na endapo itafikia mahali kutokuelewana kunaongezeka, inaweza kuondoa saini yake kwa muda kwa tafakuri zaidi.

Katika lugha ya kisheria na kidiplomasia, nchi inapoitaka mahakama ya kimataifa ijitafakari kuhusu jinsi inavyofanya kazi, inachosema ni kuwa yenyewe imejitafakari imeona kuwa kuna tofauti za kina kati ya matazamio yake na utendaji wa mahakama. Dhana hiyo pia haitofautiani na kusema kuwa kilichokuwa kinatazamiwa kuwa ni suala lisilotarajiwa kutokwa ,yaani mhusika kufungua madai dhidi ya serikali bila kupitia mfumo wa mahakama, au kutotaka maamuzi yake kwa kina) sasa imekuwa ndiyo kawaida. Kujitoa katika hali hiyo siyo kuikana mahakama bali ni kueleza hitaji la kujitafakari, waangalie kama wanaweza kuoanisha itikadi, matazamio, viwango.

Kwa jumla katika mazingira kama hayo inabidi muda upite kwanza na licha ya kuwa hivi sasa ni serikali inayoiambia Mahakama ya Afrika ijitafakari imesimama wapi kuhusiana na kanuni za awali za kuanzishwa kwa mahakama hiyo, hali halisi inaweza kuwa tofauti kiasi fulani.

Moja ya sababu zilizofikia mabadiliko katika utendaji wa mahakama hiyo ni kuwa ilikosolewa kwa muda mrefu kuwa haina meno, yaani bila kesi kukubaliwa, kusikilizwa kwanza na nchi mwanachama haipokelewi.

> Isitoshe, mwaka 1994 iliundwa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai kuhusu Rwanda, ikifuatia ile nyingine kuhusu Yugoslavia ya zamani, ambako ni mahakama inaunda kesi, si nchi.

Isitoshe, mwaka 1994 iliundwa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai kuhusu Rwanda, ikifuatia ile nyingine kuhusu Yugoslavia ya zamani, ambako ni mahakama inaunda kesi, si nchi.

Ina maana kuwa kuhitilafiana kati ya kanuni za awali za Mahakama ya Afrika ambayo Tanzania ilisaidia kuundwa kwake na kuwa mwenyejii wake karibu miaka 40 iliyopita ni kielelezo cha historia, kuwa kuna mazingira tofauti wakati ule ukilinganisha na wakati huu.

Hali hiyo inafanya kazi pande zote mbili kwa maana kuwa enzi zile Afrika ilikuwa inaamini inaweza kuunda chombo cha ngazi ya juu kusaidia kuunganisha Afrika kisheria kuwa na jopo la rufani kwa kesi zinazosikilizwa bila kutengemaa kikamilifu katika nchi wanachama.

Hapakuwa na mazingira ya mahakama za Umoja wa Mataifa zenye madaraka ya kukamata watuhumiwa na kuwafikisha kwa mfano The Hague. Hivi sasa kuna mahakama ya kimataifa ya aina hiyo, wengine wanachota vielelezo vipya huko.

Kwa upande wa pili, enzi hizo mfumo wa vyama vingi ulikuwa bado kwa muongo mmoja, na baada ya hapo ikachukua miaka 20 ya uchaguzi wa kidemokrasia kuona jinsi ufisadi serikalini unavyojenga hema la pamoja na uhuru wa mtu binafsi kwa upande mmoja na uhuru mpana wa bunge na vyama vya siasa.



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

## Ufaulu wa masomo ya Kiingereza na Hisabati unaendelea kuwa tatizo kwa wanafunzi wengi wa shule za msingi na sekondari Nini kifanyike waweze kuyamudu? Wadau wanajadili.



### CHARITY MANOKO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

NI vyema jamii ikaelewa kwamba kufundisha somo na kutozungumzwa kama lugha ya mawasiliano shuleni ndicho chanzo cha baadhi ya wanafunzi kushindwa kumudu lugha hii ya Kiingereza au kumudu somo la Kiingereza na pia walimu kutopewa mafunzo yanayolenga kuwapa mbinu za ufundishaji ni chanzo kingine cha kuwafanya wanafunzi kutomudu somo la Hisabati.

Na imejengeka dhana kwamba masomo hayo ni magumu kueleweka kwa wanafunzi, lakini mimi siamini katika hilo, bali ubunifu kwa walimu ndiyo haupo na umekuwa chanzo cha wanafunzi kufanya vibaya. Mambo yanakwenda yakibadilika, lakini ufundishaji ni ule wa zamani, ambao binafsi ninauona kama hauna tija kwa walimu na wanafunzi kwa ujumla.

Kwa mazingira ya sasa, ninadhani ipo haja kwa serikali na wadau wa elimu kuona tatizo hilo na kulifanyia mabadiliko, ili kuboresha elimu ya Tanzania na hasa kwa kuzingatia kwamba baada ya elimu ya msingi huwa kuna mabadiliko pale mwanafunzi anapokwenda sekondari, ambako anakuta Kiingereza kinakuwa ni lugha ya mawasiliano licha ya kwamba ni somo, sasa kama hatakuwa na msingi mzuri tangu chini atakwama.

Kwa upande wa somo la Hisabati ni kwamba nalo linafundishwa kwa lugha ya Kiingereza na kama mwanafunzi hatakuwa na msingi wa lugha hiyo atakwama hata kama atakuwa anahitaji kuuliza maswali, ambayo anadhani yangemsaidia kujua mambo mengi hataweza kufanya hivyo kwa vile hajui lugha.

Mimi ningeshauri wahusika kuliangalia suala hili kwa kina badala ya kupapasa tu kama ilivyo sasa ili lipatiwe ufumbuzi kwani linalenga kupata wasomi wazuri.



### ERNEST PAUL (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

BAADA ya kuhitimu kidato cha nne, niliwahi kufundisha shule mbalimbali za msingi wakati nikisubiri matokeo na niligundua kuwa watoto wamejengewa hofu kuwa masomo hayo ni magumu na kujikuta hawayapendi.

Kwa mtazamo wangu ni kwamba hiyo inaweza kuwa sababu kubwa inayochangia baadhi yao kufanya vibaya.

Ni vyema wakaambiwa kuwa Hisabati ni somo la kawaida na hata Kiingereza ili watambue kuwa yanafundishika na kueleweka.

Tatizo kwa upande wa somo la Kiingereza ni kwamba hakizungumzwi kama lugha ya mawasiliano shuleni tofauti za shule binafsi, ambazo zimekuwa zikitumia lugha hiyo kama ya mawasiliano ambapo wanafunzi wao wamekuwa wakiimudu wangali wadogo, lakini kwa shule za serikali Kiingereza kinachukuliwa kama somo tu huku baadhi ya walimu wakiwa hawana uwezo wa kumudu kufundisha somo hilo.

Yaani kwenye shule zetu wataalamu wa lugha hiyo ni wachache na ukija kwenye somo la hisabati ni kwamba nako matatizo ni kama yanafanana ikiwa ni pamoja na walimu kujengwa katika misingi duni ikiwa ni pamoja na kukosa mafunzo kazini ambayo yangewaongezea mbinu za ufundishaji ambazo zingewafanya wanafunzi waelewe zaidi.

Matatizo hayo na mengine mengi yakifanyiwa kazi, masomo yatakuwa rahisi kuanzia ufundishaji hadi kwa wale wanaofundishwa na hivyo kuwafanya wayafurahie.



### DAVID NACK (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

KWA hali kama hii tutaendelea nyuma kwenye ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia na ikumbukwe kuwa dunia ya leo imekuwa kama kijiji, hivyo ipo haja ya kukazania somo la Kiingereza kuanzia elimu ya awali ili wanafunzi wawe na mwanga nalo na hata wanapoingia sekondari lisiwe geni kwao.

Lugha hii iwe ni ya mawasiliano kuanzia huko nilikosema hadi sekondari, kwani ni moja ya lugha za kimataifa, ambayo inaweza humfanya Mtanzania kuwasiliana na watu wa mataifa mengine bila matatizo.

Ugumu uliopo hapa kwetu ni kulifanya kama somo badala ya kuwa lugha ya kufundishia kuuwafundisha.

Nikijija kwenye Hisabati, ni kwamba lina vipengele vingi, ambavyo vimekuwa vikiwapa taabu walimu na hasa kutokana na uchache wao kwenye shule za serikali na uchache huo umekuwa ukichangia baadhi yao kufundisha masomo, ambayo hawana uwezo nayo na matokeo yake hawawezi kuwapa wanafunzi kile wanachokihitaji badala yake wanapitia juu juu tu.

Pamoja na hayo, ninapenda kuiambia jamii kuwa masomo hayo yanafundishika na kueleweka, kinachotakiwa kufanywa hapa ni serikali kupitia wizara husika kuendelea kuboresha elimu kwa kuifanyia mabadiliko ikiwamo kuajiri walimu wa kutosha wenye ujuzi, ili waweze kufundisha watoto wetu kama inavyotakiwa na watakuwa wamewasaidia kumudu masomo yao.



### MARIAM MAKANGE (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

TATIZO kubwa linalochangia kuwapo kwa hali hii ya baadhi ya wanafunzi kushindwa kumudu masomo hayo ni serikali yenyewe kutokuwa na nia ya dhati ya kuboresha elimu hapa nchini. Nasema hivyo kwa sababu kila Mtanzania anajua ni jinsi gani elimu inavyozidi kuporomoka kila kukicha kwa wanafunzi wengi kufanya vibaya katika mitihani yao ya kidato cha nne.

Siyo kwamba hawana akili, bali serikali haijaamua kuwekeza kwenye elimu kama inavyotakiwa. Unakuta shule ina walimu wawili, watatu ama saba, katika mazingira hayo unaweza kukuta kati yao hakuna hata mwalimu wa somo la Hisabati ama Kiingereza, kama hali yenyewe ndiyo wanafunzi watakuwa mbinu gani za kumudu masomo hayo kama siyo kuwaonea?

Nimejaribu kutoa mifano hiyo michache tu, lakini ukweli ni kwamba sekta ya elimu ina matatizo mengi ambayo yamekuwa yakichangia elimu ya Tanzania kuporomoka. Ukweli ni kwamba mabadiliko makubwa yanahitajika ikiwa ni pamoja na serikali kuboresha maslahi ya walimu ili wengi wajitokeze kuajiriwa kwani naamini wapo wenye uwezo, lakini wamekimbilia kwenye shule binafsi baada ya kugundua kuwa maisha yao yatazidi kuwa magumu iwapo wataendelea kufundisha katika za serikali.

Siyo siri wapo baadhi ya walimu ambao wanafundisha masomo, ambayo hawana uwezo nayo kutokana na shule kuwa na walimu wachache na matokeo ni wanafunzi kufanya vibaya na hasa kwenye masomo ya Kiingereza, Hisabati na mengine.



### IBRAHIM BWANA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

MASOMO ya Hisabati na Kiingereza hayajashindikana na siamini kama wanafunzi hawawezi kuyamudu, ila ninachokiona ni ukosefu wa mafunzo, semina na warsha kwa walimu, ambazo zingewasaidia kumudu ufundishaji kulingana na mabadiliko ya mitaala.

Bahati mbaya hatufundishi kulingana na mabadiliko hayo, kwani yanapokuja walimu hawapati nafasi ya kupewa semina ambayo ingesaidia kufanya vizuri kazi hii ya ufundishaji.

Lakini kiukweli ni kwamba masomo haya ni kawaida, yanafundishika na wanafunzi wanaweza kuelewa vizuri, ila tatizo linalochangia kuwapo kwa ugumu wa uelewa unaowakabili baadhi ya wanafunzi na hata walimu wenyewe wanaofundisha. Katika hili naweza kusema pia kuwa waakati mwingine wanafunzi nao wanakuwa wagumu kwa kutotilia maanani masomo yenyewe na hasa hili la Kiingereza, kwani hata sisi tumesoma kwenye shule hizo hizo lakini baada ya kufika sekondari tulibadilika na kumudu vizuri somo hilo ikiwamo kuongea ingawa shule ya msingi lilikuwa somo la kawaida kama mengine, lakini kwenye sekondari huwa Kiingereza kinatumika kama lugha ya mawasiliano.

Ukija kwenye Hisabati utagundua kuwa ina topiki nyingi, ambazo mwalimu asipokuwa makini anaweza kuwafundisha wanafunzi kinyume. Hapa nina maana kwamba semina, warsha na mafunzo kwa walimu ni ya muhimu ili kuwajengea uwezo wa kumudu masomo.

# Wachimbaji washauriwa kuwekeza

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MKUU wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, amewaomba wachimbaji wa madini na wafanyabiashara wa wilaya hiyo kuwekeza mali wanazochuma kwenye huduma za jamii ikiwamo elimu.

Alitoa ombi hilo alipokuwa mgeni rasmi kwenye mahafali ya kwanza ya shule ya awali ya mchepuo wa Kingereza ijulikanayo kwa jina la Baba Mzazi English Medium School.

Alisema ni vizuri watu hao kuwekeza miradi yao ndani ya wilaya hiyo ili wananchi wanaoishi jirani nao wanufaike badala ya kuchuma Chunya na kwenda kuwekeza maeneo mengine.

"Nampongeza mwenzetu Lawena (Lawena Nsonda) ameamua kujenga shule hii ambayo ni miongoni mwa shule chache zinazomilikiwa na watu binafsi ndani ya wilaya yetu… sasa na wengine wanatakiwa waige mfano huu ili tuinogeshe Chunya yetu," alisema Mahundi.

Alisema serikali iko tayari kushirikiana na watu wote wanaotaka kuwekeza kwa kuwapatia maeneo ya kuwekeza, na kwamba maeneo hayo yapo ya kutosha.

Akizungumzia mipango yake ya uwekezaji ndani ya Wilaya hiyo, Nsonda alisema ni kuanzisha shule ya sekondari na shule ya msingi ili kuwarahisishia wanafunzi ambao walikuwa wanasafiri umbali mrefu.

Alisema shule hiyo ni sehemu ya lengo lake la kurudisha sehemu ya kile anachokipata kwenye biashara zake kwa jamii ili nayo inufaike kwa kupunguza gharama za kuwasafirisha watoto wao.

Aliishukuru serikali kwa kumpatia ushirikiano katika kuhakikisha shule hiyo inafikia hatua nzuri.

# KKKT yajitosa vita dhidi ukatili wa watoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KANISA la Kiinjili la Kirutheri Tanzania (KKKT), limewataka Watanzania kuungana kupiga vita vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ili kukomesha vitendo hivyo ambavyo vinaharibu ustawi wa kundi hilo.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa wanawake na watoto wa kanisa hilo nchini, Faustina Losai, wakati wa maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia zilizoandaliwa na kanisa hilo na kufanyika kitaifa jijini Mbeya.

Alisema takwimu za ukatili dhidi ya watoto nchini zinaonyesha asilimia 60 ni ubakaji kitendo ambacho alieleza kinawaathiri watoto kimwili na kiakili pamoja na kuwa katika hatari ya kuambukizwa magonjwa.

Alisema ili kukomesha vitendo hivyo kila Mtanzania kwa nafasi yake anatakiwa kushiriki kukemea badala ya kuiachia serikali na vyombo vya dola kwa kuwa wanaotekeleza unyama huo wanaishi kwenye jamii.

Faustina aliwataka wazazi na walezi kuwalinda watoto wao kwa kuhakikisha wanashinda na watu wanaoaminika na kuepuka kuwatuma nyakati za usiku ambao ndio muda mbaya.

"Tunaipongeza serikali kwa kuendelea na vita hii, lakini ili kushinda vita hii ni lazima Watanzania wote tushiriki kwa kuwafichua wabakaji na watu wengine wanaotekeleza vitendo vya ukatili dhidi ya watoto," alisema Faustina.

Alisema KKKT linaungana na Serikali kupiga vita vitendo hivyo, huku akisisitiza kuwa vinarudisha maendeleo ya taifa nyuma kutokana na kutumia rasilimali kubwa kupambana na vitendo hivyo.

Aidha, katika maadhimisho hayo kanisa hilo lilimwalika Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ambaye aliwakilishwa na Mwenyekiti wa Chama cha Riadha cha Mkoa wa Mbeya, Tes Nchimbi, ambaye alilipongeza kanisa hilo kwa uamuzi huo.

Akisoma hotuba ya Dk. Tulia, Nchimbi alisema kama vitendo hivyo vitaendelea bila kupingwa kuna hatari taifa likawa na maendeleo duni kutokana na nguvu kazi kuwa ndogo kwa kuwa waathirika wa unyanyasaji huwa wanakata tamaa.

"Naupongeza uongozi wa kanisa kwa kubuni hili tukio na mnatakiwa kuigwa na makanisa mengine ili tupate nguvu zaidi ya kupambana na matukio haya, sisi viongozi ndio dira ya watu wengine maana huwa wanatuangalia sisi tunafanya nini," alisema Nchimbi.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Jiji la Mbeya, Habiba Ibrahim, alisema ukatili dhidi ya watoto unaathiri sekta nyingi ikiwamo elimu kwa maelezo kuwa mtoto aliyeathirika na ukatili hata maendeleo yake shuleni yanakuwa mabaya.

Alisema wao wanaendelea kutoa elimu ili wananchi wawe na uelewa wa kutosha kuhusu matukio hayo.




Wafanyakazi wa moja ya daladala zinazofanya safari zake kati ya Stendi Kuu na Igawilo jijini Mbeya, wakihangaika kuikwamua gari hiyo baada ya kuteleza na kutumbukia kwenye mtaro katika eneo la Bustani ya Jiji la Mbeya karibu na Uwanja wa Sokoine mwishoni mwa wiki. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Wadau elimu wataka chakula shuleni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU wa elimu mkoani Mbeya wamezitaka halmashauri zote za mkoa huo kusimamia upatikanaji wa chakula cha mchana katika shule zote za msingi na sekondari ili kuinua kiwango cha ufaulu wa wanafunzi.

Walitoa ushauri huo wakati wa kikao cha wadau kilichokuwa kinalenga kutoa taarifa ya uchaguzi wa wanafunzi wanaotakiwa kujiunga kidato cha kwanza mwakani pamoja na kujadili changamoto zinazoikabili sekta ya elimu mkoani humo.

Naibu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Jeremiah Minja, aliagiza ajenda hiyo kuwa ya kudumu kwenye vikao vya mabaraza ya madiwani wa halmashauri zote pamoja na vikao vya kata kwa maelezo kuwa upatikanaji wa chakula ni takwa la sera ya elimu ya mwaka 2014.

Alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa ambayo inaongoza kwa uzalishaji wa mazao ya chakula, lakini wananchi wake ni wagumu kuchangia chakula kwa ajili ya watoto wao shuleni.

Alisema katika baadhi ya mikoa suala hilo lilianza kutekelezwa muda mrefu na matokeo yake yanaonekana, lakini Mbeya zoezi hilo linasuasua na hivyo kuathiri ufaulu wa wanafunzi katika ngazi zote.

"Mkoa wa Kilimanjaro unafanya vizuri sana kwenye jambo hili, mimi natokea huko na nilijua kuwa suala la chakula shuleni ni sheria, nimekuja kujua baadaye sana kuwa sio jambo la lazima, sasa kwa kuwa tunayaona matokeo kwenye shule zinazotoa chakula cha mchana hili liwe jambo la lazima," alisema Minja.

Aliwataka wakuu wa wilaya kwa kushirikiana na wakurugenzi pamoja na maofisa elimu kutoa elimu kwa wazazi na walezi ili wachangie chakula, huku akisisitiza kuwa kiasi ambacho mtoto anakula shuleni ndio kiasi kilekile ambacho angetakiwa kula kama angeshinda nyumbani.

Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, alisema endapo suala la chakula cha mchana litafainikiwa, kuna uwezekano mkubwa wa vita dhidi ya udumavu kufanikiwa pia kwa maelezo kuwa mkoa huo ni miongoni mwa mikoa yenye kiwango kikubwa cha udumavu.

Alisema hakuna sababu ya watoto wa shule katika mkoa huo kukosa chakula kwa kuwa kila aina ya chakula kinapatikana kwa wingi mkoani humo.

Alisema atashiriki katika kuhamasisha jamii kuchangia chakula, na kwamba lazima matokeo chanya yatatokea endapo chakula kitakuwa kinapatikana kwa kuwa wakati mwingine baadhi ya watoto wanashindwa kusoma vizuri kutokana na njaa.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Cloudia Kitta, alisema katika wilaya yake kuna baadhi ya shule utaratibu wa wanafunzi kupata chakula cha mchana ulianza muda mrefu na kwamba matokeo yake yanaonekana kwa wanafunzi kufanya vizuri.

Alisema sio rahisi mtoto mwenye njaa akamsikiliza kwa umakini mwalimu lakini akiwa na matumaini ya kula ni lazima asikilize na aelewe vizuri anachofundishwa.

Kaimu Ofisa Elimu wa Mkoa, George Mbijima, alisema kiwango cha ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba katika Mkoa huo kimekuwa kikipanda kila mwaka, hali ambayo alisema inaleta matumaini.

Alisema katika matokeo ya mtihani wa darasa la saba mwaka 2017 mkoa ulishika nafasi ya 17 kitaifa, mwaka 2018 ukapanda na kushika nafasi ya 13 na mwaka huu umeshika nafasi ya saba kati ya mikoa 26.





# Polisi yakabidhiwa jengo lake

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Maji imetekeleza agizo la Rais John Magufuli la kukabidhi jengo lake kwa Jeshi la Polisi, baada ya taratibu za kisheria kukamilika.

Hivi karibuni, Rais Magufuli akiweka jiwe la msingi ujenzi wa makazi ya askari wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) Dodoma, aliagiza wizara hiyo kutoa jengo lake ili iwe Makao Makuu ya Jeshi hilo.

Akizungumza baada ya makabidhiano, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Meja Jenerali Jacob Kingu, alisema Jeshi la Polisi linapaswa kutumia jengo hilo kama chachu ya ufanisi ya kufanya kazi zao za kulinda usalama wa raia.

Alisema wizara hiyo imetekeleza agizo la Rais na wao wanapaswa kulitendea haki kwa kuwajibika ipasavyo katika majukumu yao ya kila siku.

Alisema lengo lao ni kuona polisi wanafanya kazi kwa mujibu wa taratibu za kisheria.

Alimhakikishia Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, kuwa jengo hilo litakuwa salama kama walivyokabidhiwa na wizara hilo.

Prof. Mkumbo alisema jengo hilo lililokuwa la Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) kwa jeshi hilo ili kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

"Sisi hatuna deni na Jeshi la Polisi naimani mambo yetu yatakuwa sawa tumekuwa marafiki," alisema Prof. Mkumbo.

Alisema lengo lao ni kuona wanalitumia jengo hilo, huku likiendelea kukamilishwa kwenye baadhi ya maeneo madogo.

Naye Katibu wa Kamati ya kitaifa ya kuratibu serikali kuhamia Dodoma, Meshack Bandawe, alisema askari viongozi na maofisa wa juu 6,800 wa vyombo vya ulinzi na usalama wamehamia Dodoma.

"Hii inaonyesha jinsi gani kila mmoja anatekeleza agizo hilo kwa wakati na tutaendelea kufanya kazi kwa pamoja kwa kutekeleza maagizo yanayotolewa na serikali kwa ujumla," alisema.

Jengo hilo mpaka kukamilika limegharimu Sh. bilioni 12.5.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, akifundisha wakulima wa Kijiji cha Ipumbulya, wilayani Igunga jana kanuni 10 za kilimo cha pamba katika ziara yake ya kuhamasisha kilimo cha zao hilo. **PICHA: TIGANYA VINCENT**

# Wenye ulemavu 625 wasajiliwa shule msingi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Tanzania Cheshire Foundation (TCF), limesajili watoto wenye ulemavu 625 kwenye shule za msingi za wilaya za Chamwino na Dodoma.

Hayo yalibainishwa na Meneja wa mradi wa Elimu jumuishi shuleni, Menance Mhombwe, alipokuwa akiwakilisha mada kwenye maadhimisho ya Siku ya Watu wenye Ulemavu Duniani yaliyofanyika wilayani Kondoa.

Alisema waliweka lengo la kusajili watoto 1,000, lakini hadi sasa wamefanikiwa kusajili 625 na wamewapatia visaidizi vya shule ikiwamo fimbo na vitabu vya kujifunzia.

Aidha, alisema baadhi ya shughuli zinazofanywa na shirika hilo ni kuwatambua watoto hao na kuwafanyia tathmini ya hali zao kwa kuwasajili na kuanza darasa la kwanza katika shule za msingi.

Mhombwe alitaja misaada mingine ambayo shirika hilo linatekeleza kwa wanafunzi hao pia pamoja na kutoa miwani, baskeli, sare ya shule madaftari na peni.

"Tunahakikisha pia watoto hawa wanapoungua tunawapeleka hospitali ya rufani kwa ajili ya matibabu kulingana na ushauri wa madaktari," alisema.

Sambamba na hilo, alisema wanatoa mafunzo kwa walimu na maofisa elimu kata kwa lengo la kuwapatia ujuzi wa ufundishaji katika mfumo wa elimu jumuishi.

"Shirika linafanya marekebisho ya mazingira ya kujifunzia, kuwapa watoto wenye ulemavu mahitaji ya msingi hasa wale wanaotokana katika familia fukara na kuwasaidia wazazi wa watoto hao kuwa katika vikundi vya ujasiriamali," alisema.

Mshauri wa mradi wa elimu jumuishi kutoka Leonard Cheshire, Theofory Mwalongo, alisema utekelezaji wa mradi unazingatia sera ya Taifa ya ulinzi wa mtoto na matamko yote ya kimataifa juu ya watu wenye ulemavu la 2006.

Alisema baadhi ya haki za mtoto ni pamoja na ulinzi, elimu, kucheza, kuthaminiwa na mahitaji yote ya msingi ili waweze kukua vizuri, kimwili, kiakili, kiroho na kimaadili.

# Tarura yarahisisha barabara Mpwapwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura), kumewezesha wananchi kupata huduma za kijamii kwenye maeneo ambayo yalikuwa hayapitiki kipindi cha masika katika Wilaya ya Mpwapwa.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, wakati akizungumza na wananchi kuhusu kazi iliyofanywa na Tarura ya kujenga barabara ya kupanda mipangano ya milima kilometa 2.2 kwenda Kata ya Galigali iliyopo umbali wa kilometa 100 kutoka Mjini Mpwapwa.

Alisema Tarura imefungua maeneo mapya ya kiutawala ambayo awali yalikuwa hayapitiki na hayafiki wakati wa masika na hivyo wananchi wa maeneo hayo kukosa huduma muhimu za serikali na za kijamii.

Shekimweri alisema kata hiyo iliyopo milimani ni maarufu kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali ilikuwa haifikiki wakati wa masika.

"Kuanzishwa kwa Tarura kumesaidia kufungua eneo hili kwa kujenga barabara ya zege na sasa inapitika wakati wote hivi sasa," alisema.

Shekimweri alisema haikuwa kazi rahisi kiongozi wa ngazi yoyote ya wilaya kufika katika maeneo hayo wakati wa masika kutokana na barabara hiyo ya kupanda milima kuwa mbaya na hatarishi kwa binadamu na magari.

Meneja wa Tarura Wilaya ya Mpwapwa, Emmanuel Lukumay, alisema barabara hiyo iliyotumia Sh. bilioni 1.23 na ina urefu wa kilometa 2.2 katika maeneo ya miteremko ya milima imekamilika kutokana na juhudi za taasisi hiyo.

Lukumay alisema kazi ilichelewa kukamilika kutokana na mkataba kuchelewa ni kutokana na sababu nyingi zikiwamo za magari kushindwa kufikisha vifaa vya ujenzi katika milima hiyo kwa kuhofia magari kuporomoka au kupotea mabondeni.

Alisema kutokana na kukamilika kwa barabara hiyo, kutasaidia wananchi ambao ni wazalishaji wa mahindi, maharage na viazi vitamu kusafirisha mazao yao katika maeneo mengine ya wilaya hiyo na nje ya wilaya.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alimpongeza mkandarasi na msimamizi wa mradi huo kutoka kampuni ya Proavtive Independent Group and Ibra Contractor, Maida Waziri.

Dk. Mahenge alisema bila jitihada za mkandarasi barabara hiyo isingekamilika.

"Wakati nilipotembelea nilikuta ikichimbwa sikuamini kama leo ingekuwa imewekwa zege na inapitika," alisema.

Aliwataka Tarura kuomba fedha kwa ajili ya kutunza barabara hiyo kwa kuweka kingo.



# Juisi ya tende yahusishwa ukatili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ASASI za Kiraia (Azaki) zimesema yapo mambo yanayoonekana kuchochea vitendo vya ukatili wa kijinsia bila jamii yenyewe kufahamu.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya asasi hizo, Jamila Mahmoud kutoka Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (Zafela), aliyataja mambo hayo kuwa ni pamoja na matangazo ya biashara ya dawa za kuongeza nguvu, juisi za tende zenye viagra na kahawa (Alkasuus), zote zikiwa ni vichocheo vya kumfanya mtu ahemukwe kingono.

Alisema vitu hivyo vinachangia watu kuingia katika ngono na vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

"Jamii haijafikiria, kundi la vijana wanaohamasishwa kununua dawa za kurefusha maumbile, dawa za kuongeza nguvu za kiume na kadhalika. Je, nguvu hizo wakazimalizie wapi?

"Tunaziomba mamlaka husika kufuatilia dawa na matangazo hayo na kwa bahati mbaya zaidi dawa hizi hutangazwa misikitini.

"Jamii ya Zanzibar ya sasa imezama katika fasiki (mwenendo mbaya, hasa uasherati) wa kila aina, hivyo kunahitajika hatua za haraka ili kuirekebisha jamii ili irudi katika maadili mema," alishauri.

Alibainisha kuwa kwa mujibu wa takwimu zilizokusanywa na mahakama zote za mikoa ya Unguja na Pemba kuanzia Julai 2018 hadi Juni 2019, kesi za udhalilishaji zilizofikishwa mahakamani ni 224 ambazo ni za kubaka, kulawiti, kukashifu, kutorosha, kuingilia maharimu (ndugu kuoana) na shambulio la aibu.

"Kati ya kesi hizo 224, za kubaka ni 192, hiyo ndiyo kusema kuwa asilimia 85 ya kesi zote za udhalilishaji zinazofikishwa mahakamani ni za kubaka," alisema.

Hawra Shamte, Meneja wa Sera na Utetezi kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), alisema asasi hizo zimetoa maazimio mbalimbali ikiwamo kuzitaka mamlaka husika kusimamia madrasa za dini ili ziwe na mwongozo maalum wa ufundishaji na walimu wawe na viwango vya kuridhisha, wasajiliwe na wafanyiwe ukaguzi.

"Kutokana na utoaji wa mawaidha yanayokwenda kinyume cha taratibu zetu na silika (tabia za kuzaliwa alizonazo mtu) zetu, ipo haja Ofisi ya Mufti na Jumuiya ya Maimamu kusimamia mawaidha ili yasitolewe mawaidha yanayokwenda kinyume cha maadili," alisema.

Pia aliitaka Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) kufungia mitandao michafu na kudhibiti video zinazorushwa ambazo zina maudhui yaliyo kinyume cha maadili.

Aliwataka wazazi waache kuwapa watoto simu janja sambamba na kufuatilia jinsi watoto wanavyotumia simu, wafuatilie nyendo za watoto wao kiujumla na watoe ushirikiano pale maadili yanapokiukwa.



Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Muhammed Ramia, akimkabidhi cheti Ali Sultan, mdau wa mambo ya utalii, wakati akitoa vyeti vya ushiriki bora wa Tamasha la Utalii lililofanyika Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wizara yawapa mbinu wasanii kulinda kazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WASANII wa sanaa za maigizo Zanzibar wametakiwa kuzisajili kazi zao katika Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar (Cosoza) ili kuzilinda na kupata stahiki zao.

Rai hiyo ilitolewa na Katibu Mkuu, Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Omar Hassan Kingi, katika kikao cha viongozi wa wasanii wa maigizo mwishoni mwa wiki.

Alisema iwapo wasanii hawatazisajili kazi zao katika taasisi hiyo, itakuwa vigumu kwa taasisi kuwa na nguvu ya kuzitetea na kupata haki stahiki.

Alisema kumekuwapo na malalamiko ya wasanii kukosa haki zao, akieleza kuwa hali hiyo imechochewa na wasanii wenyewe kutojisajili kazi zao katika ofisi hiyo.

Katibu Mkuu pia alisema sanaa ya maigizo Zanzibar imeshuka, hivyo kuna haja ya kuchukua hatua kwa kuhakikisha inainuika.

Aliwataka wasanii wa Zanzibar kuwa na umoja wa wasanii ili kuwatambua wasanii wa zamani na wapya.

Alisema kwa sasa, wasanii wa Zanzibar wamekuwa hawana umoja, jambo ambalo limekuwa vigumu kuwasaidia pale inapotokea wanahitaji misaada ya kiserikali.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha wasanii wa Zanzibar wanafaidika na kazi zao kwa kuutambua mchango wao waliotoa katika kazi ya tasnia hiyo.

Katika kikao hicho, viongozi wa wasanii wa maigizo walisema watahakikisha wanazisajili kazi zao na kufuata maadili na silika katika kazi zao za sanaa ili kutoa elimu kwa jamii.

**Alisema kwa sasa, wasanii wa Zanzibar wamekuwa hawana umoja, jambo ambalo limekuwa vigumu kuwasaidia pale inapotokea wanahitaji misaada ya kiserikali.**

# Ataja cha kuibeba CCM uchaguzi ujao

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania, Ofisi ya Zanzibar, Tunu Juma Kondo, amesema utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa njia ya vitendo, utasaidia kuimarisha chama na kuendelea kushika madaraka.

Akikabidhi vifaa na fedha zilizotolewa na Mwakilishi wa Viti Maalum, Sada Ramadhani Mwendwa, Ofisi za CCM Amani, Unguja, Kondo alisema chama kimeimarika kutokana na uimara wa viongozi walioko madarakani kwa kutekeleza kwa vitendo vya ilani yake.

Alisema wapo baadhi ya viongozi hushindwa kutekeleza ilani ya chama kwa vitendo, jambo ambalo hudhorotesha maendeleo ya wananchi.

"Chama hakitosita kumchukulia hatua za kisheria kiongozi yeyote atayekwenda kinyume cha maadili ya chama," alisema.

Aliwataka viongozi wa vyama vya siasa kushirikiana na serikali kutatua kero za wananchi na kuwaletea maendeleo badala ya kutoa kauli zinazoashiria uchochezi.

Vilevile, aliwaomba wananchi kutunza na kuthamini amani na utulivu wa nchi uliopo na kuwataka kutokubali kurubuniwa na baadhi ya viongozi wasiopenda maendeleo ya nchi.

Mwakilishi wa Viti Maalum wa MKOA Wa Mjini, Sada Ramadhan Mwenda, aliwataka viongozi na wanachama wa umoja huo kujitolea kwa hali na mali bila kujali maslahi yao binafsi.

Aliwataka wavilinde na kuvitunza vifaa hivyo ili kuwasaidia na kuondokana na hali ya utegemezi.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Amani, Juma Resi, alimpongeza mwakilishi huyo kwa kutekeleza kwa vitendo ilani ya chama hicho na kuahidi kuvitunza vifaa hivyo.

# DC aagiza baraza ardhi kijijini kuvunjwa

**Na Friday Simbaya,** KILOLO

MKUU wa Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa, Asia Abdallah, amewataka viongozi wa vijiji katika wilaya hiyo kutojihusisha na biashara ya kuuza ardhi kiholela, hivyo kusababisha migogoro ya ardhi.

Alisema wapo baadhi ya wenyeviti wa vijiji na watendaji wanaojihusisha na biashara ya kuuza ardhi ya vijiji na ya wananchi kwa wawekezaji.

Abdallah alisema hayo wakati ziara ya kikazi aliyofanya kwa kutembelea vijiji vitano vya Kata ya Ukwega wilayani Kilolo.

Alitembelea vijiji vya Lulindi, Ipalamwa, Ukwega, Makungu na Mkalanga vya Kata ya Ukwega kuhamasisha shughuli za maendeleo na kutoa maelekezo ya serikali.

Alisema Kijiji cha Mkalanga ni moja ya vijiji katika Kata ya Ukwega kilichoathirika na uuzaji holela wa ardhi kwa wageni na kibakia sehemu ndogo ya ardhi ya kijiji na kushindwa kutenga maeneo ya uwekezaji.

Aidha, DC Abdallah aliagiza Baraza la Ardhi ya Kijiji cha Mkalanga livunjwe kwa sababu ndio chanzo cha kuzalisha migogoro ya ardhi kijijini.

Mzee Obedi Kasuga (89), mkazi wa Kijiji cha Mkalanga ni mmoja wa wananchi walioathirika na changamoto ya kuchukuliwa ardhi na serikali ya kijiji hicho alitoa kilio chake kwa DC Abadalla, ambaye aliagiza alirejeshewe ardhi yake.

Katika hatua nyingine, DC Abdallah aliwataka wananchi wa vijiji hivyo kutumia vyema mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo yao kwa kuzalisha chakula cha kutosho.

Alisema Mkoa wa Iringa hasa Wilaya ya Kilolo unakabiliwa na changamoto ya udumavu kwa watoto kutokana na lishe duni pamoja na wilaya za mkoa huo kuzalisha chakula cha kutosha.

Pia Abdallah alipiga marufuku wajawazito na wanaonyonyesha kushinda vilabu vya pombe usiku na kusahau majukumu yao ya kuhakikisha wanatoa chakula chenye lishe bora ili kupunguza tatizo la udumavu.

Vijiji vya Lulindi, Ipalamwa, Ukwega, Makungu na Mkalanga vya Kata ya Ukwega vinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo miundombinu ya barabara isiyopitika kipindi cha mvua, changamoto ya maji na umeme wa REA ambao bado vijiji hivyo havijafikiwa.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Amina Khamis Shaabani, akimkabidhi Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Benki ya CRDB Tuzo ya Benki Bora katika utayarishaji wa ripoti za kifedha kwa mwaka 2018, iliyotolewa na Bodi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu (NBAA). Hafla ya kukabidhiwa tuzo ilifanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Meneja Mwandamizi Idara ya Fedha, Hemed Mkuu na Mkuu wa Idara ya Fedha na Utawala wa Kampuni Tanzu ya Bima, Abdallah Mrisho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# UVCCM waonywa kughushi umri

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

VIJANA ambao ni wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Masasi mkoani Mtwara wameshauriwa kuachana na tabia ya kughushi umri wanapogombea nafasi za uongozi ndani ya chama hicho hususan Jumuiya ya Vijana (UVCCM).

Ushauri huo ulitolewa na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Wilaya ya Masasi, Twahili Saidi, alipokuwa akizungumza na gazeti hili kuhusu uchaguzi wa nafasi ya mwenyekiti wa UVCCM wilayani Masasi utafanyika baada ya mwenyekiti wa awali katika nafasi hiyo kutenguliwa kwa madai ya kughushi umri.

Alisema CCM Wilaya ya Masasi imepokea kwa masikitiko taarifa ya kuondolewa kwa Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Masasi, Azizi Mrope, baada ya baraza la jumuiya hiyo taifa kutangaza kuwa mwenyekiti huyo kupoteza sifa yake kutokana na kubainika kuwa wakati akiomba nafasi hiyo mwaka 2017 alighushi umri.

Saidi alisema Desemba 3, Baraza la Vijana Taifa lilitangaza kumuengua mwenyekiti huyo na kuitaka CCM Wilaya ya Masasi kutangaza upya uchaguzi wa mwenyekiti wa UVCCM ili kujaza nafasi hiyo.

Alisema kutokana na hali hiyo, CCM Wilaya ya Masasi inawataka vijana wote ambao ni wanachama wa chama hicho kuhakikisha wanapoomba nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya chama hicho kuacha kudanganya umri.

Alisema ni vema wanapojaza fomu kuomba nafasi hizo wakajaza umri sahihi badala ya kudanganya kwa lengo la kutaka kuchaguliwa.

"Kwanza tunaupongeza umoja wa vijana taifa kwa kukaa na kupitia baadhi ya kanuni na kuziboresha, lakini tunapongeza kwa kuchunguza na kubaini mwenyekiti huyu wa umoja wa vijana wilaya ya Masasi alikuwa ameghushi umri wake," alisema Saidi.

Alisema CCM wilaya katika uchaguzi zijazo ikiwamo ya nafasi ya uenyekiti umoja wa vijana itahakikisha inasimamia kikamilifu suala la umri kwa wagombea wa nafasi hiyo.

Aidha, katibu huyo wa Itikadi na Uenezi wa CCM Wilaya ya Masasi aliwataka vijana wa chama hicho wilayani humo kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi hiyo pale itakapotangazwa rasmi kwa uchaguzi.

Saidi alisema kitendo cha mwenyekiti huyo wa UVCCM Wilaya ya Masasi kughushi umri na kusababisha kuenguliwa, limekuwa funzo kwa vijana wengine wa chama hicho.

# Waagizwa mitambo ya kuchuja hewa viwandani

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Musa Sima, amewataka wamiliki wa viwanda kufunga mitambo ya kuchuja hewa ili kutunza mazingira na afya za wananchi.

Alitoa maelekezo hayo wakati wa mkutano wa majadiliano kati ya serikali, wawekezaji na wafanyabiashara uliofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, majadiliano ambayo yanaangazia changamoto na hatua za kuchukua ili kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji hapa nchini.

Sima alisema ofisi yake imechukua hatua mbalimbali za kurahisisha upatikanaji wa vibali na cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA) vinavyotolewa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

"Kwa sasa tumepunguza vikwazo vingi ambavyo vilitokana na sababu ambazo zilikuwa hazina ulazima na kila kitu kinaenda sawa, hata hivyo kama mwakilishi wa wizara, nawataka wafanyabiashara na wawekezaji kote nchini kufunga mitambo ya kuchuja hewa ili kuepuka athari hasi zinazotokana na hewa zenye sumu kutoka viwandani," alieleza.

Sima alisema kuwa pamoja na hatua za kufunga mitambo hiyo, wenye viwanda wanatakiwa kuwa na vitalu vya bustani ya miti ambayo itapandwa kuzunguka eneo la kiwanda na mingine kugawa kwa wananchi kuzunguka maeneo ya karibu ya uzalishaji ili waendelee kupata hewa safi.

"Azima ya serikali ni kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025 na kama wizara inayohusika na mazingira tumejipanga vizuri kuhakikisha yote yanatekelezwa, tunaweka mazingira mazuri juu ya taratibu za kufuata na kuangalia ustawi wa mazingira kwa faida ya sasa na vizazi vijavyo, hivyo nawataka wenye viwanda kupanda miti katika maeneo ya viwanda vyao ili kupunguza athari za hewa zenye sumu zinazotoka viwandani," alisema Sima.

Alitoa wito kwa wawekezaji na wafanyabiashara kutembelea Ofisi za NEMC makao makuu au ofisi zao za kanda zilizopo nchi nzima ili kupata ufafanuzi wa mambo yanayohusu vibali na ufanyaji wa EIA kabla hawajajenga viwanda.

"Kumekuwa na hoja kadhaa kutoka kwa wawekezaji za malalamiko ambazo majibu yake yanakuwa rahisi kupatikana kama wataonana na maofisi wetu wa NEMC. Hivyo natoa wito kwa wawekezaji kutembelea ofisi za NEMC za kanda au Makao Makuu ili kupata ufafanuzi juu ya hatua za kufuata," alisema.

HABARI KIMATAIFA

# Chanjo ya pili dhidi ya ebola yaanza kutolewa

**KINSHASA,** Congo

SERIKALI ya Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zimezindua kampeni ya utoaji chanjo ya ugonjwa wa ebola iitwayo 'Johson and Johnson' kwenye mji wa Rubavu kwa lengo la kupambana na maambukizi ya ugonjwa huo.

Shirika la Afya Duniani (WHO) limesema kwamba raia wasiopungua 200,000 wilayani Rubavu na Rusizi ndio watakaopewa chanjo hiyo na maelfu mjini Goma.

Ibrahim Soce mwakilishi wa WHO nchini humo, alisema hatua hiyo ni muhimu sana katika vita dhidi ya ugonjwa huo.

"Tunawashukuru viongozi wa DRC na Rwanda ambao kwa pamoja wameendelea kuunga mkono mapambano dhidi ya ebola katika nchi zao," alisema Soce.

Chanjo hiyo inaanza kutolewa kutokana na ushauri wa WHO na kwamba imezitaka nchi zote zilizoko hatarini kupata maambukizi ya ebola kutumia chanjo hiyo.

Mkurugenzi wa kituo cha magonjwa ya mlipuko nchini Rwanda, Dk.Sabin Nsanzimana, alisema chanjo hiyo itasaidia katika maambukizi mapya ya ugonjwa huo hatari.

Tangu kuzuka kwa ugonjwa huu mashariki mwa DRC, watu zaidi ya 1,800 wameripotiwa kupoteza maisha, huku nchi jirani zikitajwa kuwa kwenye hatari ya kupata maambukizi ikiwa hazitachukua tahadhari. **RFI**

# Mgogoro wa Rwanda na Uganda wazidi kutokota

**KIGALI,** Rwanda

UHUSIANO baina ya Rwanda na Uganda unaendelea kuwa mbaya huku upande wa Rwanda katika maeneo ya mpakani na Uganda mikakati ya kuwazuia raia wake wanaotaka kuingia Uganda ukiimarishwa.

Wananchi wa Rwanda kwenye mpaka wa Gatuna walisema kwamba mikakati hiyo ni pamoja na kuwapiga risasi wanaojaribu kuvuka na kujihusisha na biashara haramu.

"Angalia huu mfereji wa maji hapa hapa...ukivuka hivi unaingia Uganda. angalia yule mtu anayependa akija hapa yuko upande wa Rwanda, soko la kimataifa lilikuwa pale..." alisema mmoja wa raia, karibu na mpaka wa Gatuna.

**ukivuka hivi unaingia Uganda. angalia yule mtu anayependa akija hapa yuko upande wa Rwanda, soko la kimataifa lilikuwa pale...**

Raia huyo alimwonesha mwandishi wa BBC jina la soko lililopo kwenye mpaka, upande wa Uganda, zamani lilikuwa linawajumuisha wananchi wa pande mbili. Lakini sasa hakuna raia wa Rwanda anayeweza kuthubutu kukanyaga kwenye soko hilo.

"Natokea karibu tu ya hapa sitoki Uganda kwani siku hizi tulikatazwa kwenda huko." Alisema mama aliyekutana na mwandishi barabarani akiwa na begi tupu la kubebea chakula.

Aliongeza kuwa hawezi kuthubutu kukanyaga huko tena kwa sababu aliingiwa na uoga baada ya kwenda na aliporudi alinyang'anywa unga wake na kutupwa kizuizini kwa siku mbili.

BBC ilifika eneo lenye njia haramu zinazotumiwa na wanaotaka kuvuka kuingia Uganda na kugundua kuwa kwa sasa ni hatari.

"Wanaothubutu kwenda huko wanapigwa risasi, nawafahamu watu kama wanne hivi waliopigwa risasi hivi karibuni wakitaka kuvuka na kwenda Unganda," alisema mmoja wa wakazi katika eneo la mpakani.

Alisema kuwa ni wazi kwamba watu hao hawapigwi risasi na raia kwa sababu raia hawana silaha.

Hapo nyuma polisi ya Rwanda ilitangaza kwamba mtu yeyote atakayekiuka sheria za mpakani hatavumiliwa.

Ni dhahiri kwamba mikakati ya kuzuia wanaotaka kwenda Uganda imeimarishwa sana katika maeneo karibu na mpaka wa Uganda.

"Mimi naishi hapa nayajua maeneo yote ya hapa, sijaona askari katika maeneo haya ya karibu na mpaka. kilichopo sisi wenyewe raia tunafanya doria pamoja na askari wastaafu ambao pia wanatembea bila silaha. lengo letu ni kuzuia wanaotaka kuvuka na pia wafanyabiashara haramu," alisema kijana huyo.

Mkutano wa pili uliopangwa kukutanisha wajumbe wa nchi mbili mjini Kampala chini ya upatanishi wa Angola uliahirishwa na haijafahamika utafanyika lini ili kusuluhisha mgogoro huu. **BBC**



Spika wa Bunge la Marekani, Nancy Pelos. **PICHA ALLIANCE**

# Spika wa bunge atoa idhini Trump kushtakiwa

**WASHINGTON,** Marekani

SPIKA wa Bunge la Marekani, Nancy Pelosi ametoa ruhusa ya kutayarishwa kwa ibara za mashtaka dhidi ya Rais Donald Trump, hatua muhimu katika mchakato wa kujaribu kumwondoa madarakani Rais huyo wa chama cha Republican.

Katika mkutano wake na waandishi habari mjini Washington Spika Pelosi alisema atawaomba viongozi wa Bunge kuendelea na mipango ya kutayarisha orodha ya mashtaka dhidi ya Rais Trump ambayo itajumuisha ushahidi uliopatikana kuhusiana na jinsi alivyojishughulisha na suala la Ukraine.

Pelosi alisema matendo ya Rais Trump katika suala la msaada wa ulinzi kwa Ukraine yamekiuka kwa sehemu kubwa misingi ya taifa na kiapo cha ofisi.

"Taarifa zilizopo hazina ubishi, ukweli ni kwamba Rais alitumia madaraka yake vibaya kwa maslahi binafsi na manufaa ya kisiasa kwa kuweka rehani usalama wetu wa taifa alipozuia msaada wa kijeshi na kutoa nafasi ya mkutano muhimu kwenye ofisi ya rais ili litolewe tangazo la kumchunguza hasimu wake wa kisiasa." alisema Pelosi.

Uamuzi wa Pelosi umekuja siku moja baada ya wanazuoni watatu wa masuala ya katiba kuwaarifu wabunge kwamba wanaamini Rais Trump alifanya makosa ya kiwango cha kuweza kushtakiwa na kuondolewa chini ya katiba ya nchi hiyo.

Pelosi alisema ushahidi uliotolewa hauna shaka kwamba matendo ya kiongozi huyo ni ukiukwaji mkubwa wa imani ya umma na uvunjaji wa kiwango cha juu wa misingi ya katiba.

Rais Trump anatuhumiwa kutumia madaraka yake vibaya kwa kuendesha kampeni iliyowahusisha washirika wake wa ndani ya kuishinikiza Ukraine ipekue uozo dhidi ya mpinzani wake wa kisiasa kutoka chama cha Democratic, Joe Biden.

Rais Trump anashutumiwa kumtaka rais mpya wa Ukraine Volodymyr Zelensky atangaze kuanzisha uchunguzi dhidi ya mtoto wa Biden, aliyefanya kazi na kampuni ya nishati nchini Ukraine kama sharti la kupatiwa msaada wa ulinzi na kukaribishwa kwa ziara rasmi mjini Washington.

Mashtaka dhidi yake yanaweza kujumuisha matumizi mabaya ya madaraka, rushwa na kuzuia utoaji wa haki.

Rais Trump mwenyewe amejibu uamuzi huo wa bunge kwa kusema kupitia ukurasa wa Twitter kuwa Wademocrats wanataka kumwondoa madarakani bila kuwako sababu ya msingi na kwamba matumaini ya kushinda kwa sababu chama chake cha Republican kimeungana vya kutisha dhidi ya mchakato huo.

Baraza la Seneti linalodhibitiwa na Republican ndiyo litakuwa na uamuzi wa mwisho kuhusiana na mashtaka ya rais na sharti ni kwamba theluthi mbili ya kura za maseneta inahitajika kuweza kumwondoa Rais Trump madarakani.

Warepublicans wameshasema kuwa hakuna ushahidi wa kutosha kwamba Rais Trump alifanya makosa yanaweza kumtoa madarakani na kwamba Wademocrats wanaoendesha mchakato huo wameruhusu hisia na chuki dhidi ya kiongozi huyo kutawala maamuzi wanayofikia. **DW**

# Wawekezaji wazawa watakiwa kuchangamkia fursa EPZA

**Na Mwandishi Wetu**

WAWEKEZAJI wa ndani wamehimizwa kutumia fursa zinazotolewa na Mamlaka ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji (EPZA), kuanzisha viwanda ili kuchangia ukuaji wa uchumi.

Mpaka sasa asilimia 43 ya viwanda katika Mamlaka ya EPZA vinamilikiwa na wawekezaji wazawa ikichangiwa kwa kiasi kikubwa na uboreshaji wa mazingira ya biashara na serikali.

"Mamlaka ya EPZA inatoa fursa na huduma mbalimbali kama kuwezesha uwekezaji, kutoa leseni na vivutio mbalimbali ambavyo vitamsaidia mwekezaji mzawa kuwekeza katika viwanda," alisema Ofisa Mwandamizi Uhamasishaji wa EPZA, Panduka Yonazi, wakati wa maonyesho ya viwanda yanayofanyika katika viwanja vya Sabasaba vilivyopo kandokando ya Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam.

Alisema mamlaka inatoa huduma kwa wawekezaji kabla ya uwekezaji, wakati na baada ya uwekezaji ili kuwapatia taarifa muhimu za namna ya kuwekeza katika maeneo ya ukanda maalum wa kiuchumi ya EPZ na SEZ.

Vile vile, alisema EPZA inatumia maonyesho ya viwanda kuwapa wawekezaji na watu wengine taarifa za fursa mbalimbali na vivutio vinavyotolewa na mamlaka. Maonyesho haya ya viwanda yanawapa ujasiri wawekezaji wa ndani ili kuanzisha na kushiriki kwa karibu kujenga uchumi wa viwanda.

Alisema maonyesho haya ya viwanda yamekuwa ni fursa muhimu kwa wawekezaji wazawa kutembelea banda la EPZA na kujifunza mambo mengi yanayoelekeza na kutoa mwanga namna bora zaidi ya kuanzisha viwanda.

"Tuliwaambia wawekezaji juu ya mazingira wezeshi yanayowekwa na serikali yenye lengo la kuvutia zaidi uwekezaji katika viwanda na kuchangia katika ukuaji wa uchumi," alisema.

Pia mamlaka ya EPZA inatangaza vivutio mbalimbali vya nchi hasa kwenye upande wa viwanda kupitia maeneo maalum ya kiuchumi SEZ.

Takwimu kutoka mamlaka zinaonyesha kuwa uwekezaji kupitia maeneo maalum ya kiuchumi imefikia Dola za Kimarekani bilioni 2.6 na kuingizia nchi fedha za kigeni kiasi cha Dola bilioni 1.3 hadi kufikia Januari, mwaka huu.




Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya K-Finance inayotoa mikopo na ushauri wa kibiashara kwa wafanyabiashara na watu binafsi, Devotha Minzi (katikati), akimpa maelekezo mteja (kulia) aliyetembelea banda hilo, wakati wa Maonyesho ya Siku ya Ushindani Duniani jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa K-Finance, Judith Minzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kanuni kukabiliana majanga ya moto shuleni kuandaliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amesema serikali ipo mbioni kuandaa kanuni zitakazosambazwa shuleni kukabiliana na majanga ya moto hasa katika shule za mabweni nchini.

Pia amelitaka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji nchini kuanzisha klabu za marafiki wa zimamoto katika shule za msingi, sekondari na vyuo kwa ajili ya kutoa elimu ya kukabiliana na majanga hayo.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki katika mashindano ya klabu za marafiki wa zimamoto Shule ya Dodoma Sekondari.

Mashindano hayo yalilenga washiriki kujifunza mbinu mbalimbali za kukabiliana na majanga ya moto hususan wanafunzi.

Waziri Lugola alisema klabu hizo zitasaidia wanafunzi kukabiliana na majanga ya moto katika hatua za awali na kuwaokoa na mali zao.

Alisema klabu hizo ni nzuri na kumwagiza Kamishna wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengenye, kuanzisha klabu hizo kwenye shule zote za msingi, sekondari na vyuoni.

Waziri Lugola alisema atatayarisha kanuni haraka ili zisambazwe kwenye shule zote na vyuoni.

"Tunataka kuwakinga watoto wetu na majanga ya moto ambayo huleta madhara makubwa ikiwamo vifo na uharibifu wa mali, kwa mamlaka niliyonayo nitatayarisha kanuni haraka ili zisambazwe kwenye shule zote na vyuoni," alisema.

Waziri Lugola alisema elimu ya kujikinga na majanga ya moto itawasaidia, si wao tu bali hata jamii inayowazunguka.

Kwa upande wake, Andengenye alisema mpaka sasa kuna klabu 327 zenye wanachama 15,232, lengo ni kuanzisha klabu hizo nchi nzima.

"Mpango wetu ni kuanzisha klabu nchi nzima ili tuweze kutoa elimu kwa wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuoni," alisema.

# Hofu yatanda maporomoko Kalambo kukauka

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MAPOROMOKO ya Mto Kalambo wilayani Kalambo mkoani Rukwa huenda yakakauka kabisa katika kipindi cha miaka 15 ijayo kama serikali ya haitachukua hatua madhubuti kukabiliana na uharibifu wa mazingira katika maeneo unapopita mto huo.

Wajumbe wa kikao cha Kamati ya Ushauri (RCC) mkoani Rukwa walitoa ushauri huo wakati wakichangia mada kuhusu uharibifu wa unaotishia maeneo ya utalii yaliyopo mkoani humo.

Mmoja wa wazee maarufu na mwanasiasa mkongwe mkoani humu,Chrisant Mzindakaya, alisema kuwa uharibifu wa mazingira uliopo hivi sasa ni janga kwani unatishia kuharibu maeneo ya utalii yakiwamo maporomoko hayo.

Alisema uharibifu wa mazingira unaofanyika katika vijiji unakopita mto Kalambo unasababisha kupungua maji katika mto huo na kuathiri maporomoko ya mto Kalambo yaliyopo mpakani mwa Tanzania na Zambia.

"Kadiri miaka inavyozidi kuongezeka hali inazidi kuwa mbaya zaidi, na ninahofu ndani ya kipindi cha miaka 15 huenda maporomoko hayo yakakauka kabisa na ikabaki historia tu kuwa kulikuwa na maporomoko ya Kalambo kama jitihada ya kuyanusuru zisipofanyika," alisema Mzindakaya.

Alisema kuna kila sababu ya kuweka mikakati ya kukabiliana na uharibifu uliokithiri ili kuyalinda maporomoko hayo, ambayo ni ya pili kwa urefu barani Afrika baada ya Victoria Falls, ambapo pia yamekuwa kivutio kikubwa cha utalii ndani na nje ya nchi.

Naye mzee Zeno Nkoswe kutoka taasisi isiyo ya kiserikali ya Rukwa Environment Management Society (REMSO) inayojishughulisha na uhifadhi wa mazingira mkoani humu, alisema ni lazima serikali na wadau wa mazingira washirikiane ili kutunza mazingira yasiharibike na mito isikauke kipindi chote cha mwaka.

Mkuu wa mkoa wa Rukwa ambaye alikuwa mwenyekiti wa kikao hicho, Joachim Wangabo, aliziagiza halmashauri zote za mkoa huo pamoja na tasisi zisizo za kiserikali zinazojishugulisha na utunzaji wa mazingira ziongeze jitihada katika kupanda miti.

Pia aliagiza kuchukuliwa hatua kali kwa baadhi ya watu wanaoharibu vyanzo vya maji kwani hao ndio wamekuwa wakichangia kukauka kwa mito mingi, na wananchi kujikuta wakikabiliwa na uhaba wa maji pamoja na kutishia uharibifu katika maeneo ya utalii yaliyopo mkoani humu.

Alisema kuwa utalii na mazingira ni watoto pacha, hivyo ni lazima kila mkazi wa mkoa huo ahakikishe anapanda miti na kuitunza ili tatizo la uhaba wa maji hasa kipindi cha kiangazi liishe katika mkoa huo na wananchi waweze kunufaika na maeneo ya utalii yaliyopo yakiwamo maporomoko ya mto Kalambo.

# Bandari zaidi kuanzishwa

**Na Elizabeth Zaya,** MWANZA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari (TPA), imesema ina mpango wa kuanzisha bandari kubwa kila mkoa na bandari ndogo kila wilaya katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Mwanza jana, Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Deusdedit Kakoko, alisema lengo ni kuhakikisha wanafungua makufuli yaliyofunga uchumi.

Alisema kujenga bandari nyingi kutawezesha pia sekta ya usafirishaji kupitia njia ya maji kufanya kazi zaidi na pia kutasaidia watu kufanya biashara kwa wingi.

Alisema wanaamini bandari nyingi zitasaidia pia bidhaa na mazao mengi kusafirishwa na kuokoa uharibifu wa barabara ambao umekuwa ukisababishwa na kupitisha mizigo mizito.

"Tunaua uchumi kwa kuharibu barabara tunapopitisha mizigo mizito na hata magari yanachoka haraka, lakini kama una vyombo vikubwa kama meli na treni, utachukua mzigo mkubwa na unaokoa barabara.

"Kwa hiyo, tunapojenga bandari nyingi, tunawezesha vyombo vya majini viende sehemu nyingi na kusafirisha sukari, pamba na mazao mengine kutolewa kule yanakolimwa.

"Katika miaka mitano inayofuata, tuna imani kila wilaya itakuwa inabeba boti fulani, tunakua kiuchumi, tutaangalia magati yanayoendana na mahitaji katika kila eneo katika kipindi cha miaka mitano ijayo mradi tuondoe yale makufuli yanayofunga uchumi ambao tayari unaonekana upo, lakini umefungwa hauonekani," alisema.

Aliongeza kuwa mpango huo utakuwa mwarobaini pia wa kuondoa bandari bubu ambazo zimekuwapo kwa kipindi kirefu zikitumika kufanya biashara ya magendo.

"Tayari bandari bubu zote tunaziwekea uchangiaji kwa ajili ya mapato, kodi na kiusalama pia. Bandari zote ni mipaka, kwa hiyo unapopata tishio la usalama, TPA lazima tufanye kazi yetu vizuri ya kuhakikisha bandari bubu tunazisimamia.

"Tunapozisimamia vizuri, tunazidi kuongeza usalama kwa sababu tunakuwa na watu wanaoangalia maeneo yote ya kuingia au kutoka, kwa hiyo kama kuna silaha zinatoka nchi za jirani inakuwa ni rahisi kuziona na ndiyo maana TPA ina idara ya ulinzi na usalama ambayo ina mkurugenzi wake.

"Kazi yetu hiyo ya kuweka bandari hizo bubu kuwa rasmi na kutoza tozo, tutazifanya ndani ya miaka mitano inayokuja na hakuna bandari yoyote itakayobaki na jina la bubu, zote zitakuwa zimepewa ndimi," alisema.

Alisema kwa maelekezo ya serikali, bandari hizo baada ya kurasimishwa, zitakuwa zinatoa tozo nafuu na kwamba na uchunguzi walioufanya hivi karibuni wamebaini kuwapo kwa bandari bubu 163.

Alisema mpaka kufikia Juni mwakani, bandari zote bubu zitakuwa zimeanza kusimamiwa na mamlaka hiyo.

"Kwa sasa, tunaelekea katika mpango wa kuziweka bandari zetu katika ngazi, kwa mfano Bandari ya Dar es Salaam unaipa jina lake, heshima yake na ngazi zake. Bandari za Mtwara na Tanga hivyo hivyo.

"Tunadhani tutakuwa na ngazi kama sita ambazo tayari ziko kwenye majadiliano ili baadaye ziingie kwenye sheria na tutaweka kanuni.

"Kwa hiyo, tunavyozungumza kutambua bandari si tu kwa kujua jina, lakini ni katika kuzipanga kwa viwango ambavyo vina viwango vyake.

"Tutakuwa na viwango au sifa na vigezo vya kila aina ya bandari ili tutakapopanga miundo ya kitaasisi kwa maana ya wafanyakazi unaipanga ukijua ni bandari ya aina hii na inahitaji wafanyakazi wa aina fulani.

"Kigezo kikubwa ni uwezo wa kibiashara ambayo bandari yenyewe inao na uhusiano na wingi wa biashara na ndiyo maana tunasema ni rahisi kwamba kila mkoa kuona kwamba utakuwa na bandari," alisema.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki (kushoto), akiteta jambo na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Musa Sima, katika mkutano wa majadiliano kati ya serikali, wawekezaji na wafanyabiashara wa Mkoa wa Pwani mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Usalama sasa watekelezwa mahali pa kazi

**Na Mwandishi Wetu**

OFISI ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, imefanya ukaguzi wa utekelezaji wa sheria ya usalama na afya mahali pa kazi kwenye idara na taasisi zake, kuhakikisha kuna wafanyakazi wenye afya na walioko salama.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari, maeneo 1,187 idara ya kazi, Wakala wa Usalama Mahali pa Kazi (OSHA), Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Mfuko wa Hifadhi kwa watumishi wa umma (PSSSF) na Mfuko wa Fidia (WCF).

Akipokea ripoti ya ukaguzi huo kwenye kikoa na wakuu wa taasisi na idara hizo jijini Dodoma, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Andrew Massawe, alisema ukaguzi huo ni muhimu kwa kuwa unalinda nguvu kazi kwa taifa.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu huyo, iwapo sheria namba 5 ya mwaka 2003 ya usalama na afya mahali pa kazi itatekelezwa ipasavyo, itasaidia kuleta hamasa na ari ya kazi kwa wafanyakazi.

Kadhalika, kuimarisha mahusiano mazuri na jamii katika kuongeza ubora wa bidhaa au huduma inayotolewa na wizara, idara za serikali, kampuni au taasisi husika.

"Ripoti hii itanisaidia kuweka mikakati ya kuzuia vihatarishi vinavyoweza kujitokeza ili kuzuia wafanyakazi wasipate ajali na magonjwa yatokanayo na kazi," alibainisha na kuongeza:

"Ni vyema waajiri na wafanyakazi na umma kwa ujumla kushirikiana na serikali katika ukaguzi wa utekelezaji wa sheria hii ya afya na usalama mahali pa kazi, ili tuweze kuimarisha afya na usalama kazini na mstakabali wa kazi, kwa kuwa tayari serikali tumefanya juhudi katika kuboresha mazingira ya kazi na kuweka mifumo ya afya na usalama kazini iliyo imara na inayoleta tija katika sehemu za kazi.

# Tehama yarahisisha vitambulisho, vyeti

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

MIAKA tisa ya uongozi wa Rais Ali Mohammed Shein imeleta mageuzi makubwa katika nyanja za Teknolojia, Habari na Mawasiliano (Tehama) na kuleta matokea chanya ambapo wakazi visiwani hapa wanaweza kupata vitambulisho vya ukazi, vyeti vya uzazi na vifo katika ngazi ya wilaya.

Mafanikio ya Tehama yameweza kuchochea maendeleo na ustawi wa sekta mbalimbali za uchumi na kijamii ambapo hilo limewezekana kutokana na ubia na mashirika mbalimbali ikiwamo kampuni kubwa ya Kichina ya mawasiliano ya ZTE Corporation iliyotoa mchango mkubwa.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais Dk. Ali Mohammed Shein, imefanikisha upatikanaji wa huduma za kimtandao, hivyo zote kuunganishwa katika Mkongo wa Taifa na kuimarisha utoaji wa huduma," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano Zanzibar, Mhandisi Shukuru Awadhi Suleiman.

Alikuwa akiongea na waandishi wa habari kutoka Tanzania Bara waliotembelea Zanzibar kujifunza namna miradi mbalimbali ya Tehama ilivyotekelezwa na kuchochea maendeleo ya kijamii.

Alisema serikali kupitia Wakala wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano Zanzibar, imefanikiwa kuziunganisha ofisi 11 za wilaya za Wakala wa Usajili wa Vitambulisho vya Ukazi, Uzazi na Vifo.

"Haya yote yamewezekana kupitia maendeleo ya Tehama ambapo huduma zote hizi zinatolewa ikiwamo vyeti vya ndoa, talaka, kuzaliwa na vitambulisho vya ukazi vinatolewa moja kwa moja katika ngazi ya wilaya," alisema mhandisi Suleiman.

Alisema awali kabla ya awamu ya Rais Shein, huduma hizo zilikuwa zinamlazimu mtu kusafiri mbali hadi makao makuu kwa ajili ya kupata huduma hiyo na kwa sasa imebakia historia tu.

"Katika kuhakikisha watu wanapata huduma bora ya mawasiliano, serikali chini ya Rais Dk. Shein imewekeza katika mkonga wa mawasiliano uliolazwa baharini kutoka Dar es Salaam hadi Unguja na mwingine kutoka Tanga hadi Pemba," alisema.


JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II
(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)
KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO **MJINI TANGA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NAMBA 167/2019**

OMBI LA **DIAMOND RAJABU MUSHI** KUTEULIWA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU **PETER JACOB LUMWE**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA**

WATU WOTE WANAODAI KUWA NA UHUSIANO WOWOTE NA MIRATHI YA MAREHEMU HUYO WANAALIKWA KUJA NA KUHUDHURIA KESI WAKITAKA MNAMO TAREHE 10/12/2019 KABLA HUYO MWOMBAJI HAJATEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI HIYO

WOSIA WA MAREHEMU HUYO UPO MAHAKAMANI WAWEZA KUKAGULIWA

**TAREHE 21.11.2019**

# JOAQUIN AWA MCHEZAJI MKONGWE KUTUPIA HAT-TRICK



**MADRID,** Hispania

GWIJI wa Real Betis, Joaquin amekuwa mchezaji wa kwanza mwenye umri mkubwa zaidi kufunga mabao matatu 'hat-trick' akiwa na miaka 38 na siku 140.

Winga Joaquin alianza kufunga bao la kwanza katika kipindi cha pili dhidi ya Athletic Bilbao timu ambayo imeweka rekodi ya kuwa na safu nzuri ya ulinzi kwenye La Liga.

Alifunga bao la pili baada ya dakika 11, na akafunga la tatu zikiwa zimesalia dakika chache mpira kumalizika.

Na hilo likamfanya kuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kufunga hat-trick kwenye La Liga.

Joaquin alivunja rekodi ya Alfredo di Stefano kwenye ligi hiyo kwa kufunga hat-trick akiwa na umri mkubwa na imedumu kwa kipindi cha miaka 55.

Kwenye Ligi Kuu ya England Teddy Sheringham ndiye anayeshikilia rekodi ya kufunga mabao akiwa na umri mkubwa zaidi wakati akiwa na miaka 40 na siku 268.

Pia Sheringham ana rekodi ya kuwa mwenye umri mkubwa zaidi kufunga hat-trick kwenye Ligi Kuu ya England akiwa na umri wa miaka 37 na siku 146.

Claudio Pizarro bado anashikilia rekodi hiyo kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, huku mshambuliaji wa zamani wa Ligi Kuu ya England, Tony Cascarino akishikilia rekodi hiyo kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.




# *Vardy aifukuzia rekodi yake EPL*

**LONDON,** Engaland

JAMIE Vardy amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga kwenye mechi nane mfululizo za Ligi Kuu tangu alipofanikiwa kufikia rekodi hiyo mwaka 2015.

Vardy aliweka rekodi ya kufunga mara 11 mfululizo wakati Leicester City ikitwaa ubingwa wa Ligi Kuu na sasa yupo katika wimbi la kuipiku tena.

Alifunga bao dakika ya 20 dhidi ya Aston Villa katika mchezo uliopita wa Leicester akiendelea kuongeza nafasi ya kukaa kwenye nafasi ya pili ikiongozwa na vinara Liverpool. Vardy amekuwa kwenye kiwango bora kabisa kwenye Ligi Kuu tangu mchezo wa kwanza wa kocha, Brendan Rodgers kuchukua mikoba ya kuinoa Leicester Machi 3, mwaka huu.

Vardy kwa sasa anaongoza kwenye orodha ya wafungaji bora wa ligi hiyo akiwa na mabao 14 baada ya mechi 16.

# Wenger aitaka Arsenal kugeukia kocha mzoefu

**LONDON,** England

KOCHA Arsene Wenger amewashauri mabosi wa Arsenal kuzingatia uzoefu wakati wa kuteua kocha mpya wa klabu hiyo.

Wenger anawataka mabosi wa Arsenal kuajiri kocha mwenye uzoefu kama kocha wa mpito Freddie Ljungberg atashindwa kurekebisha mambo kwenye timu hiyo.

"Kama Freddie atashindwa kuweka mambo sawa ndani ya mechi tano au sita zijazo, kuna unahitaji wa kupata kocha mwenye uzoefu kunusuru mambo," alisema Wenger na kuongeza.

"Lakini, naamini watakuwa vizuri tu chini ya Freddie."

Arsenal imecheza mechi tisa za michuano yote bila ya kushinda na Alhamisi walikutana na kipigo kutoka kwa Brighton kwenye Ligi Kuu England, kikiwa ni kipigo cha kwanza kwa kocha Ljungberg kwenye mechi zake mbili tangu alipoteuliwa kuwa kocha wa muda wa timu hiyo.

Mechi yake ya kwanza Ljungberg alitoka sare ugenini kwa Norwich City.

Wakati huo huo, Kocha Massimiliano Allegri amesema atasubiri hadi mwisho wa msimu kuamua timu ya kwenda kujiunga nayo huku Arsenal wakitajwa kuhitaji huduma ya kocha huyo wa zamani wa Juventus.

Arsenal wamedaiwa kwamba wanafanya mchakato wa kupata kocha kwa haraka baada ya kuona Ljungberg ameshindwa kufanya kweli kwenye mechi mbili alizowaongoza.

Lakini kauli ya Allegry kwamba hataki kazi kwa sasa hadi mwisho wa msimu ni kama anawakataa Arsenal.

Kocha huyo Mtaliano anawindwa pia na Manchester United.






# GUARDIOLA: MAN CITY HAIWEZI KUSHINDANA NA TIMU KUBWA

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema Manchester City "haina nguvu ya kushindana" na timu bora Ulaya na "wanatakiwa kukubali ukweli huo".

Timu yake ilipoteza 2-1 dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja, Manchester United kwenye mchezo wa Ligi Kuu Jumamosi na wanaendelea kuburuzwa na Liverpool kwa tofauti ya pointi 14.

Msimu uliopita, City ilishinda mataji matatu ya nyumbani na ilitetea taji la Ligi Kuu na ilipoteza mechi nne msimu huu wa 2019-20.

"Tunatakiwa kuimarika na kukubali hilo ili tusonge mbele," alisema Guardiola.

"(Manchester) United wana ubora wa kulinda na kushambulia kwa kushtukiza na unatakiwa kukubali hilo," aliongeza.

"Na hilo ndilo tunalokabiliana nalo dhidi ya Liverpool, Manchester United, Barcelona, Real Madrid na Juventus. Ni timu bora unazotakiwa kukabiliana nalo na hatuna uwezo wa kushindana nao.

"Pengine tunahitaji kuimarika, tunatakiwa pia kukubali ukweli huo."

Manchester City ilishinda kwa mara ya kwanza mara mbili mfululizo taji la Ligi Kuu msimu wa 2017-18 kwa rekodi ya kupata pointi 100, lakini walifungwa kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Liverpool.

# Ninaimani kubwa na Keita-Klopp

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema kamwe hajawahi kutilia shaka uwezo wa kiungo wake, Naby Keita.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Guinea alijiunga na timu hiyo akitokea Leipzig kwa ada ya pauni milioni 52.7 kipindi cha majira ya joto mwaka 2018, lakini hajatumika kwa mechi nyingi na Klopp, hasa kwa msimu huu.

Lakini Keita alifunga bao lake la kwanza kwenye ligi mismu huu wakati Liverpool ikiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Bournemouth Jumamosi, akifunga la pili kabla ya kumtengenezea pasi Mohamed Salah aliyefunga la tatu baada ya Alex Oxlade-Chamberlain kufunga la ufunguzi.

Klopp alisisitiza kuwa na imani na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, na kwamba majeraha ndiyo yaliyomfanya muda mwingi akae benchi.

"Naby alikuwa na majeraha, kwa uhakika timu ipo katika hali nzuri, hivyo unahitaji mabadiliko?" Alisema Klopp.

"Sisi hatupai, si kama tulishinda mechi zote 4-0, au 5-0, hivyo tunahitaji kuwaleta wachezaji ambao watatusaidia.

"Halafu Naby alikaa benchi na kufikiria, 'kwa nini sichezeshwi?' Nitapata nafasi tu. Hivyo tulikuwa tunazungumza kila wakati, na tulizungumza kwa kina kuhusu hilo."







# Rakitic asema Barca bora kwake

**BARCELONA,** Hispania

IVAN Rakitic amepaita Barcelona "mahali bora zaidi kwangu" baada ya kuanza kwenye mchezo wake wa tatu mfululizo kwenye ushindi wa 5-2 dhidi ya Real Mallorca Jumamosi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia mwenye umri wa miaka 31, alionekana kama aliyekaribia kuondoka hapo Barcelona baada ya kukosa kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara.

Alianza mara moja Septemba wakati wakifungwa na Granada kabla ya kupewa nafasi dhidi ya Borussia Dortmund Novemba 27 kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia kwenye ushindi wa 3-1 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Rakitic aliendelea kupata nafasi kwenye LaLiga dhidi ya Atletico Madrid na Mallorca.


Rakitic alijiunga na Barcelona akitokea Sevilla mwaka 2014 na ameshinda mataji manne ya Ligi Kuu na Kombe la Mfalme [Copa del Rey] na hana mpango wa kuondoka kama ataendelea kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara katika kikosi cha kwanza.

"Mambo mengi yametokea ndani ya miezi michache iliyopita," alisema Rakitic.

"Wakati mwingine, kuna vitu vinatokea hata huwezi kuelewa, lakini unatakiwa kukubali.

"Ilinitokea mimi. Hakuna aliyenipa nafasi."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MAGUIRE AIONA NNE BORA MAN UNITED

Tumeshinda mfululizo dhidi ya Spurs na City, hilo sasa lipo machoni mwetu, lakini...

**MANCHESTER,** England

USHINDI wa mabao 2-1 dhidi ya mahasimu wao, Manchester City, umeanza kuwafungua mdomo Manchester United baada ya beki wa kati wa timu hiyo, Harry Maguire kueleza kuwa sasa wanauona uwezekano wa kumaliza nafasi nne za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu England msimu huu.

**Kabla ya ushindi huo walioupata Jumamosi, United ilianza kwa kuibuka na ushindi kama huo tena Jumatano dhidi ya Tottenham ambayo ipo chini ya kocha wao wa zamani, Jose Mourinho.**

Ushindi katika 'dabi' hiyo 179 ya Manchester, uliiwezesha United kupanda hadi nafasi ya tano ikiwa pointi tano nyuma ya nafasi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya ilipo Chelsea ambayo ilishindwa kufurukuta dhidi ya Everton.

"Nadhani unahitaji kutazama baada ya matokeo yako mwenyewe, usitazame kokote, endelea kushinda mechi," Maguire alisema.

"Tumeshinda mfululizo dhidi ya Spurs na City. Sasa tuna mechi nyingine kubwa wiki ijayo.

"Nne bora ipo machoni mwetu lakini tunatazama tu baada ya matokeo yetu binafsi, kuendelea kujaribu kuvuna pointi tatu na kuendelea kujizatiti."

Mabao kutoka kwa Marcus Rashford na Anthony Martial yaliwasaidia kuibuka na ushindi kwenye mechi hiyo ya 'dabi' - huo ukiwa ni ushindi wa tatu ugenini kwa United dhidi ya City kwenye ligi katika misimu mitano iliyopita.

Maguire, ambaye alikuwa beki ghali zaidi duniani baada ya uhamisho wake wa pauni milioni 80 akitokea Leicester majira ya joto yaliyopita, alisema kujiimarisha kwa United kumekuwa nguzo ya mafanikio.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 26, aliiambia tovuti ya United: "Zaidi ya mwezi mmoja, ninajisikia kama beki ninatazama washambuliaji na ninadhani wanakwenda kufunga mabao.

"Mwanzoni mwa msimu, ukweli hatukufunga zaidi ya bao moja kwenye mechi, lakini sasa ni mechi chache ambazo tumerejea kufunga mabao."

## ZISIKUPITE

### YAONGOZA KWA SMALLING

ARSENAL inaongoza dhidi ya Everton na Leicester katika vita vya kuiwania saini ya beki wa Manchester United, Chris Smalling, 30, pindi mkataba wake wa mkopo wa muda mrefu pale Roma utakapomalizika. ***(Mirror)***

### PEDRO AIVUTIA ASTON VILLA

ASTON Villa inavutiwa kuinasa saini ya Pedro katika dirisha la usajili la Januari, wakati huu winga huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 32, akipoteza nafasi Chelsea. ***(Telegraph)***

### JUVE YAJITOSA KWA HAALAND

JUVENTUS imetoa ofa kulimpa Erling Braut Haaland, pauni milioni 2.5 kwa mwaka kama mshahara baada ya kubaini mshambuliaji huyo wa Red Bull Salzburg na Norway ana kipengele katika mkataba wake kinachomruhusu kuuvunja kwa pauni milioni 25.3. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

### WANUKIA EVERTON

KOCHA wa zamani David Moyes na wa Shanghai SIPG, Victor wanaongoza katika mbio za kuteuliwa kuinoa Everton kwa kurithi mikoba ya Marco Silva, wakati Kocha Mkuu wa Monaco, Leonardo Jardim naye yumo. ***(Mirror)***

### HUGHTON KUMRITHI PELLEGRINI

DAVID Moyes na Chris Hughton wanapewa nafasi ya kwenda kuinoa West Ham kama Manuel Pellegrini atatimuliwa. ***(Express)***

### ARTETA AONGOZA ARSENAL

KOCHA msaidizi wa Manchester City, Mikel Arteta kwa sasa anaongoza katika mbio za kuchukua mikoba ya Unai Emery pale Arsenal baada ya Brendan Rodgers kujifunga zaidi Leicester na nahodha wa zamani wa 'Gunners' hao, Patrick Vieira kufanya hivyo Nice. ***(Express)***

### KOVAC ATAJWA ARSENAL

KOCHA wa zamani wa Bayern Munich, Niko Kovac pia anataka kuinoa Arsenal na jana alitarajiwa kuhudhuria mechi ya Ligi Kuu dhidi ya West Ham. ***(Goal)***

### SPURS KUMREJESHA FELLAINI

KIUNGO wa zamani wa Manchester United, Marouane Fellaini, ambaye kwa sasa anaichezea Shandong Luneng Taishan ya China, anaweza kujiandaa kurudi Ligi Kuu England. Mbelgiji huyo mwenye umri wa miaka 32, anawindwa na Tottenham. ***(DH Net - in French)***

### IBRAHIMOVIC HATIHATI SERIE A

LICHA ya kuhusishwa na AC Milan, Bologna na Napoli, mshambuliaji wa zamani wa Sweden, Zlatan Ibrahimovic, 38, labda anaweza asirudi Serie A baada ya kuondoka LA Galaxy, amesema wakala wake Mino Raiola. ***(La Gazzetta dello Sport - in Italian)***

### ALONSO ATAKIWA INTER

INTER Milan inavutiwa kumsajili beki wa kushoto wa Chelsea na Hispania, Marcos Alonso, 28, katika dirisha la Januari. ***(Calciomercato - in Italian)***

### RAKITIC AANZA KUNOGEWA

BAADA ya kuanza mechi tatu mfululizo, kiungo wa Mcroatia Ivan Rakitic, 31, amesema Barcelona ni sehemu sahihi kwake, licha ya kuhusishwa na Juventus na Inter Milan. ***(Goal)***

HABARI MICHEZO

# YANGA KUTAFUTA KASI KWA MWAMGONGO, MBAO FC

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuendelea kujiimarisha kuelekea Kombe la Shirikisho la Soka nchini maarufu FA Cup, na mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya watani zao Simba, Yanga itafanya ziara ya kimichezo mkoani Kigoma na kucheza mechi mbili za kirafiki.

Yanga ambayo inatarajia kutua Kigoma keshokutwa, Alhamisi ikiwa mkoani humo, Ijumaa itacheza mechi ya kwanza ya kirafiki dhidi ya Mwamgongo FC kabla ya Jumapili kuvaana na Mbao FC, mechi zote zikipigwa katika Uwanja wa Lake Tanganyika.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli akizungumzia ziara hiyo alisema mbali na kuendelea kuiimarisha timu yao kuelekea mechi zilizopo mbele yao, lakini lengo lingine ni kuwapa fursa mashabiki wao mkoani Kigoma kukishuhudia kikosi hicho kutokana na kutofika mkoani humo kwa muda mrefu sasa.

"Tutaondoka na wachezaji wote wa ndani isipokuwa wale waliopo timu ya Taifa (Kilimanjato Stars) na wale wa kigeni kwani tuliwapa mapumziko mafupi kwenda kuziona familia zao kipindi hiki ligi ikiwa imesimama," alisema.

Kabla ya kuivaa Simba Januari 4, mwakani kwenye mechi ya Ligi Kuu, kati ya Desemba 20 hadi 22, mwaka huu Yanga itaikaribisha Iringa United kwenye mechi ya raundi ya 64 ya Kombe la FA wakati watani zao, Wekundu wa Msimbazi wakiwa na kibarua kigumu dhidi ya Arusha United.

Yanga inayonolewa na Kaimu Kocha Mkuu, Boniface Mkwasa kufuatia kutimuliwa kwa Mwinyi Zahera, kwa sasa ipo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 17, nane nyuma ya vinara Simba.

Hata hivyo, Simba imeshuka dimbani mara 10, michezo miwili zaidi ya Yanga ambayo hata kama ikishinda mechi hizo mbili itafikisha pointi 23.

MAVETERAN...



Wanaumoja wa Kitunda Veteran kwa kushirikiana na Kiyombo Veteran, wakifanya usafi katika Zahanati ya Kitunda jijini Dar es Salaam kusherehekea miaka 13 tangu kuanzishwa kwao sambamba na kusherehekea miaka 58 ya Uhuru jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wasichana Tz wang'ara, hat-trick 4 zatupiwa U-17

**Na Mwandishi Wetu, JINJA**

TIMU ya soka ya Wasichana ya Tanzania Bara ya umri chini ya miaka 17, imeanza vema kampeni ya kuwania ubingwa wa Kombe la Chalenji kwa vijana baada ya kuifunga Eritrea mabao 5-0 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Njeru, mjini hapa jana, huku mshambuliaji wake, Joyce Charles akishuhudiwa akifunga hat-trick.

Hat-trick hiyo ya Joyce ilifuatiwa na nyingine tatu katika mechi ya pili ya michuano hiyo wakati Kenya ikiichapa Djibouti 14-0, ambapo Anna Harusi alicheka na nyavu mara nne sawa na Fasila Adhiambo na Viola Khalali huku Lavin Anyango na Dorine Achieng kila mmoja akipachika bao moja.

Hadi mapumziko, kikosi hicho cha wasichana cha Tanzania Bara ambacho mechi yake ilichezwa kuanzia saa 5:00 asubuhi, kilikuwa kinaongoza kwa mabao 3-0.

Mbali na Joyce aliyefunga hat-trick ya kwanza kwenye michuano hiyo, mabao mengine yalifungwa na Aisha Masaka.

Hata hivyo, katika msimamo wa mashindano hayo yanayochezwa kwa mtindo wa ligi, Tanzania Bara imeshika nafasi ya pili baada ya wenzao wa Kenya kupata ushindi mnono wa mabao 14-0 dhidi ya Djibouti.

Wafungaji wa timu ya Kenya ni Anna Harusi aliyefunga mabao manne sawa na Fasila Adhiambo na Viola Khalali huku Lavin Anyango na Dorine Achieng kila mmoja akipachika bao moja.

Mashindano hayo yanayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), yataendelea tena kwa Tanzania kuivaa Burundi wakati Kenya itacheza dhidi ya Eritrea na wenyeji Uganda watawakaribisha Djibouti.

Michuano hiyo inayofanyika kwa mara ya kwanza itamalizika Desemba 17, mwaka huu na timu itakayovuna pointi nyingi ndiyo itaibuka bingwa wa kwanza.

Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa) na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), ndio wadhamini wa michuano hiyo yenye lengo la kuendeleza soka la wanawake katika ukanda huu.

## Zanzibar Heroes yaahirisha mechi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KUFUATIA mechi kati ya Zanzibar Heroes na Kilimanjaro Stars nchini Uganda leo, Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), imesogeza mechezo mitatu mbele ya Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja ambayo ilipangwa kuchezwa leo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kamati hiyo, Hussen Ahmada, alisema lengo la kusogezwa mbele kwa michezo hiyo ni ili kutoa nafasi kwa mashabiki wa soka kuangalia timu yao ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes) ambayo itashuka dimbani dhidi ya Tanzania Bara katika michuano ya Kombe la Chalenji inayoendelea nchini Uganda.

Alisema Wazanzibar wengi wamekuwa wakiifuatilia timu yao hiyo tangu ikiwa haijasafiri hadi iliposafiri, hivyo si vema siku ya mechi ya Zanzibar Heroes ZFF ikaendelea na ratiba nyingine viwanjani, na badala yake wametoa fursa kwa wapenzi wa soka kuifuatilia timu yao.

Aidha, alisema kutokana na mabadiliko hayo, michezo hiyo ya sasa itachezwa keshokutwa, Alhamisi katika viwanja vilivyopangwa awali ambavyo ni Uwanja wa Mao A, Mao B pamoja na Amaan.

Timu ambazo zitashuka dimbani Alhamisi baada ya mechi zao za leo kuahirishwa ni Ngome dhidi ya Bweleo katika Uwanja wa Amaan, Uhamiaji dhidi ya Kikwajuni mechi itakayopigwa Dimba la Mao A na Miembeni dhidi ya Mchangani kwenye Uwanja wa Mao B

## Ruvu Shooting walia na ratiba kuwabana

**Na Shufaa Lyimo**

KUFUATIA Ruvu Shooting kutakiwa mkoani Tabora kuivaa Mirambo FC kwenye Kombe la Shirikisho la Soka nchini maarufu FA Cup, mchezo utakaopigwa Desemba 21, mwaka huu, huku siku nne baadaye ikitakiwa mkoani Pwani Uwanja wa Mabatini kuikaribisha Kagera Sugar kwenye mechi ya Ligi Kuu, uongozi wa klabu hiyo umeingiwa na hofu ya kushindwa kufanya vizuri.

Msemaji wa timu hiyo, Masau Bwire aliliambia gazeti hili kuwa baada ya kumaliza mchezo wao wa FA wataanza safari Desemba 22, mwaka huu kurejea jijini Dar es Salaam kwa ajili ya mchezo huo.

"Timu inaendelea vizuri lengo ni kufanya vizuri kwenye Kombe la Shirikisho japo tutakuwa ugenini.

"Ratiba imebana wachezaji watachoka kwa sababu tutarudi Desemba 22 usiku halafu tarehe 24 tuna mchezo," alisema.

Michezo
Jumanne Desemba 10, 2019
Nipashe

## Maguire aiona nne bora Man United


HABARI UK. 30

# Kili Stars, Zanzibar zaidi ya vita leo

**Na Somoe Ng'itu, KAMPALA**

BAADA ya kuanza vibaya mashindano ya Kombe la Chalenji, timu ya Soka ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), itashuka dimbani leo kuvaana na "ndugu zao" Zanzibar Heroes katika mchezo wa pili wa Kundi B utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa KCCA (Lugogo) jijini hapa.

Kilimanjaro Stars itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Kenya wakati Zanzibar Heroes yenyewe ilipata sare ya bao 1-1 dhidi ya Sudan.

Mabingwa hao wa Kombe la Chalenji kwa mwaka 2010, Kilimanjaro Stars, watahitaji ushindi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele kwenye mashindano hayo yanayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa).

Akizungumza na gazeti hili jijini hapa jana, Kocha wa Kilimanjaro Stars, Juma Mgunda, alisema amewekeza nguvu kubwa katika mchezo wa leo ili kurejesha matumaini ya kusonga mbele kwenye mashindano haya.

Mgunda alisema amewaandaa nyota wake kutumia mbinu mpya ili kuhakikisha kikosi chake kinaibuka na ushindi na kwamba amerekebisha makosa yaliyofanywa katika mechi ya kwanza na anaamini hayatajirudia ingawa anafahamu mchezo wa leo hautakuwa rahisi kwa dakika zote 90.

"Upungufu uliotokea katika mechi ya kwanza hayatotokea tena, tumewaona Zanzibar Heroes na wao wametuona, hivyo naamini utakuwa mchezo wenye ushindani, kila mmoja atahitaji ushindi katika mechi hii kwani zimebaki mechi mbili tu za kuamua hatima ya kundi, tutarajie mechi nzuri," alisema Mgunda.

Hemed Morocco, beki wa zamani wa Taifa Stars na Kocha Mkuu wa Zanzibar Heroes, alisema ameona upungufu wa kikosi chake na wataingia wakiwa makini zaidi.

"Katika mechi iliyopita tumeona upungufu ikiwamo kuruhusu bao katika dakika za mwisho, hivyo anaamini halitojirudia, naamini kikosi changu kitacheza vema mechi hiyo ya kesho (leo), ili kujiweka vizuri katika kundi," alisema Morocco.



Jembe la Liverpool, Mohamed Salah likiwa mazoezini. Leo anatarajiwa kuiongoza safu ya ushambuliaji ya timu hiyo kwenye mechi ya mwisho ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Red Bull Salzburg itakayopigwa Uwanja wa Red Bull Arena nchini Austria. **PICHA: MTANDAO** .

# YANGA YAISHTUKIA SIMBA KWA LAMINE

## Yapania kumbakisha huku Wekundu wa Msimbazi wakielezwa kutaka acheze na Nyoni, lakini...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI wachezaji watano wa kimataifa wa Yanga wakielezwa kuandika barua kwa uongozi wakitaka kuvunja mikataba yao na klabu hiyo kutokana na baadhi kudai kutolipwa mishahara kwa kipindi cha miezi mitatu, imefahamika miongoni mwao wapo wanaowindwa na upande wa pili na wapo tayari kuchepukia huko.

Nipashe imenasa barua ya beki kisiki wa timu hiyo, Mghana Lamine Moro, inayoonyesha kupokelewa na uongozi wa Yanga, akiomba taratibu za kuvunja mkataba na klabu hiyo kwa mujibu wa Kanuni za Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa) kufuatia kutolipwa mishahara yake kwa kipindi cha miezi mitatu sasa.

Kadhalika, mshambuliaji nguli wa klabu hiyo, Mkongomani David Molinga naye ni miongoni mwa wachezaji watano wa klabu hiyo ambao barua zao zinasambaa katika mitandao ya kijamii zikionyesha kuomba kuondoka kutokana na tatizo hilo la kutolipwa mishahara.

Wachezaji wengine ambao wanaelezwa kuandika barua ya kuomba kuvunja mikataba yao kutokana na tatizo hilo ni Mnamibia Sadney Urikhob, Mnyarwanda Issa Bigirimana na Mzambia Maybin Kalengo.

Hata hivyo, kuelekea usajili wa dirisha dogo kufunguliwa Jumatatu ijayo, chanzo chetu kilichopo ndani ya Klabu ya Simba kililieleza gazeti hili kuwa kati ya wachezaji hao watano, Lamine amewavutia Wekundu wa Msimbazi hao na wanaona anaweza kuwa mbadala mzuri wa Pascal Wawa ambaye umri unamtupa mkono.

"Unajua Lamine aliwahi kufanya majaribio Simba na hakuonekana kufiti wakati huo, lakini baada ya kuonekana kucheza vizuri akiwa na Yondani [Kelvini] pale Yanga, washauri wa benchi la Ufundi Simba wanaona anaweza pia kuunda safu nzuri ya ulinzi akicheza na Nyoni [Erasto]," kilieleza chanzo chetu.

Kiliongeza: "Si tatizo tena kumpata Mghana huyo, kwani kikanuni Yanga imeshavunja mkataba naye kutokana na kutomlipa kwa kipindi cha miezi mitatu."

Kwa mujibu wa mtoa taarifa wetu, inaelezwa tayari Lamine yupo katika mazungumzo na Simba na kinachosubiriwa kwa sasa ni beki huyo kumalizana kwanza na Yanga.

**Lakini kwa upande wa Yanga, inaelezwa ipo tayari kuwaachia wachezaji wengine wote waliomba kuvunja mikataba yao kuondoka lakini si Lamine na Molinga.**

Akizungumzia msimamo wa uongozi kuhusu taarifa ya wachezaji hao kuandika barua ya kuomba kuvunja mikataba yao kwa kutokulipwa, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema Yanga ni taasisi kubwa na kila kitu wanakifanya kwa utaratibu hivyo uongozi utalitolea ufafanuzi baadaye.

Bumbuli alisema hawezi kujibu taarifa za mitandaoni na kwamba Yanga kama taasisi kubwa ina utaratibu wake wa kufanya kazi jambo ambalo alitaka subra kwanza na uongozi utalitolea ufafanuzi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042